# Nipashe

Jumatano Januari 23, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579821

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Aua mke kisa kutaka ada ya mtoto shuleni

UKURASA 8



Ukurasa 18

MAMBO YATAJULIKANA 2020 KAMA NAWANIA UBUNGE AU SIVYO

MAKALA: Rais Ramaphosa kuibuka shujaa ama kukiangusha chama ANC?

Ukurasa 14

KIMATAIFA:

Ujerumani yaadhimisha miaka 100 tangu kuanzishwa demokrasia

Ukurasa 20

siasa

JUMATANO JANUARI 23, 2019 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

'Utanashati' wa kujitoa EU walea ugaidi Ireland Kaskazini, uzalendo Scotland

Ukurasa 15

DRC yapuuzia upinzani kutoka nje, yajiandaa kumwapisha Tshisekedi

Na Michael Eneza

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imedhihirisha mfumo wake wa kidemokrasia kwa kungoja uamuzi wa Mahakama ya Kikatiba nchini humo kuhusu tangazo la matokeo ya uchaguzi wa rais hapo Desemba 30 ambalo kiongozi wa upinzani Felix Tshisekedi alitangazwa mshindi.

Mgombea wa 'pamoja' wa upinzani, Martin Fayulu, alisema kulikuwa na ujanja katika kujumlisha kura na Kanisa Katoliki lililokuwa na waangalizi wa kura zaidi ya 40,000 kote nchini lilisema linatilia shaka tangazo hilo la aliyeshinda na kuashiria kuwa ni Fayulu aliyepata kura nyingi zaidi.

Uamuzi wa mahakama hiyo


ENDELEA UK 16

Rais Joseph Kabila wa DRC

UKURASA 13

# Mdau atoboa siri utoroshaji madini

• **Kabichi**, tikiti maji, vioo vya magari vyatajwa kutumika • **JPM** aanika chanzo kumwondoa Kairuki, ampa neno Biteko... *Endelea ukurasa 2*



Rais John Magufuli akihutubia Mkutano Mkuu wa Kisekta wa Wizara ya Madini jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### WADAIWA KUINGIZIWA CHUPA SEHEMU NYETI

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, kimedai watuhumiwa watano...

UKURASA WA 5

### UJENZI DARAJA LA KISASA WANUKIA

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, imetia saini mkataba wa ujenzi wa daraja la Gerezani lenye urefu wa mita 40 na upana...

UKURASA WA 8

### DC AMSWEKA NDANI DIWANI WA CHADEMA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amemsweka ndani Diwani wa Kata ya Isyesye, katika Jiji la Mbeya, akimtuhumu...

## Mkuranga yashamiri ulawiti wa wanafunzi

UKURASA 3



## Dakika 145 za Mdee kikaangoni

UKURASA 3

**MICHEZO** **AL AHLY YAMTESA AUSSEMS, SIMBA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais John Magufuli, akiagana na wadau wa madini baada ya kuhudhuria na kuhutubia Mkutano Mkuu wa Kisekta wa Wizara ya Madini jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Mdau atoboa siri utoroshaji madini

**Na Gwamaka Alipipi**

MFANYABIASHARA wa dhahabu mjini Geita, Solomon Mihayo, ameeleza mbele ya Rais John Magufuli mbinu hatari zinazotumika kutorosha madini kwenda nchi jirani.

Amezitaja mbinu hizo kuwa ni pamoja na kuficha madini ndani ya vioo vya pembeni vya magari (side mirror), kuweka ndani ya kabichi, tikiti maji na mataili ya akiba.

Mihayo aliyedai kuwa ni mtoto wa mchungaji, alifichua mbinu hizo jana kwenye mkutano mkuu wa kisekta uliowakutanisha wafanyabiashara wadogo wa madini na vito jijini Dar es Salaam kwa lengo la kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya madini nchini.

"Mheshimiwa Rais, naomba nikueleza baadhi ya mbinu zinazofanywa na baadhi ya watu kutorosha dhahabu kwenda nje ya nchi," Mihayo alisema, "kwanza, asilimia 95 ya dhahabu inaibwa, na leo (jana) nitakueleza ukweli kwa kuwa mimi ni mtoto wa mchungaji.

Alimweleza Rais Magufuli kuwa kuna watu wanapakia dhahabu ya kilo 20 kwenye kabichi, wanafunga dhahabu ya kilo tano kwenye vioo vya pembeni vya magari na kupakia kilo 30 za dhahabu kwenye tikiti maji kisha wanazisafirisha kwenda nchi jirani bila walinzi kutambua kilichomo ndani ya magari yao.

Alisema njia nyingine inayotumika kutorosha dhahabu na madini mengine kupitia viwanja vya ndege ni watoroshaji kufunga dhahabu kwenye karatasi maalum ambayo mashine za kiulinzi na utambuzi za uwanja wa ndege haziwezi kubainisha kilichomo ndani ya karatasi hizo.

"Zile mashine zilizopo Airport (uwanja wa ndege), ukienda na karatasi maalumu (siwezi kulitaja) ambalo linauzwa Sh. 5,000, ukifunga madini, hakuna mtu yeyote wala mashine itakayogundua," Mihayo alisema na kuongeza:

"Niliwahi kuwapo kwenye kamati iliyoundwa na Naibu Waziri (Stanslaus) Nyongo, nikauliza watu namna wanavyotorosha madini, wakanieleza, nikaenda kujaribu pale Uwanja wa Ndege wa Mwanza na ni kweli nilipita nayo bila kugundulika, karatasi ya Sh. 5,000 inafunga almasi ya Sh. bilioni 20," alisema Mihayo.

Alisema kwa nchi zingine, dhahabu hulindwa na mwenye dhahabu, lakini nchini madini hayo yanalindwa na Jeshi la Polisi ambalo halifahamu baadhi ya mbinu zinazotumiwa na watu katika kuyatorosha.

"Muda mwingine tunawalaumu askari wetu bure, mbinu zinazotumiwa na watu hawa ni kubwa sana. Kwanza, mipakani hakuna mahusiano mazuri, hivyo ni vema serikali ikashirikiana na wazawa wa maeneo husika ili wawaeleze mbinu zinazotumika," alisema Mihayo.

### SABABU ZA UTOROSHAJI

Mihayo aliweka wazi kuwa kuwapo kwa utitiri wa kodi na tozo za biashara ya madini nchini kunaathiri wachimbaji na wafanyabiashara wengi wa madini na ndicho kiini cha utoroshaji.

Alizitaja baadhi ya kodi na tozo hizo kuwa ni gharama za uendeshaji asilimia 0.3, mrabaha asilimia sita, kodi ya ukaguzi asilimia moja, kodi ya zuio asilimia tano na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) asilimia 18.

### KAULI YA RAIS

Katika mkutano huo, Rais Magufuli alisema serikali imeshaanza kuchukua hatua kuimarisha sekta ya madini kwa kujenga ukuta eneo la Mirerani.

Rais Magufuli pia aliagiza wizara zinazohusika kukaa na kuangalia namna ya kushughulikia tozo na kodi zinazokuwa kero kwa wadau wa sekta ya madini.

"Tumeshatoa leseni 15,209 kwa wachimbaji wa madini, pia tumeshatoa Sh. bilioni 7.616 kwa ajili ya ruzuku kwa wachimbaji wadogo," alisema Rais Magufuli.

Alisema serikali imeanza kupata mapato kutoka katika sekta ya madini, akibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba, mwaka jana, serikali ilipanga kukusanya Sh. bilioni 160 kutoka kwenye sekta hiyo, lakini hadi sasa imeshakusanya Sh. bilioni 167.

Akijibu baadhi ya hoja zilizotolewa katika mkutano huo, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alisema changamoto zilizozungumzwa na wadau hao wa sekta ya madini ni za kweli, lakini hadi sasa wizara imeshaanza kuchukua hatua ya kurudisha uhusiano na wafanyabiashara wakubwa, wa kati na wadogo.

Biteko pia alisema ameshaunda timu ya wataalamu ambao wapo mjini Dodoma wanatunga kanuni kuhusu kuanzishwa kwa soko la madini.

# JPM ataja sababu kumwondoa Kairuki Wizara ya Madini

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli ameweka wazi sababu iliyomsukuma kumwondoa aliyekuwa Angellah Kairuki, kwenye Wizara ya Madini na kumhamishia wizara nyingine.

Januari 8, mwaka huu, Rais Magufuli alifanya mabadiliko madogo ya baraza lake la mawaziri, akimtoa Waziri Kairuki kwenye Wizara ya Madini na kumpeleka kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Uwekezaji.

Hata hivyo, Rais Magufuli siku hiyo hakuweka wazi sababu za kumwondoa waziri huyo katika Wizara ya Madini ambayo mawaziri wake wamekuwa hawakai kwa muda mrefu.

Akifungua mkutano wa kisekta uliowakutanisha wafanyabiashara wadogo wa madini na vito jijini Dar es Salaam jana, Rais Magufuli alisema alimwondoa Kairuki Wizara ya Madini kutokana na kuwa mpole.

"Nataka Dotto (Biteko - Waziri wa Madini) ukawe mkali, mwenzako aliyekutangulia hakuwa mkali na ndiyo maana nikamtoa na kumhamishia Ofisi ya Waziri Mkuu ili akapumzike huko," alisema Rais Magufuli.

Mbali na kumtaka kuwa mkali, Rais Magufuli pia alimpa Waziri Biteko mwezi mmoja kuhakikisha kamera za ulinzi zinafungwa kwenye ukuta wa Mirerani. Vilevile, Rais Magufuli pia alimtaka Biteko kuwaondoa bila kusita watu ambao watakuwa kikwazo kwake katika kutimiza wajibu wa kikazi.

"Rais (Benjamin) Mkapa aliponiteua kuwa Waziri wa Ujenzi, nilipofika tu nilifukuza mainjinia 261, nikaenda kwa Waziri Mkuu, Frederick Sumaye, akawa anapingapinga, akinieleza si vizuri kuwafukuza mainjinia wote hawa, nikaamua kumfuata Rais Mkapa ambaye naye akanipa kibali cha kuwafukuza na kuanzia hapo barabara zikaanza kujengwa, mainjinia walikuwa wanatembea na 'vi-note' kwenye soksi," alisema Rais Magufuli.

Aliongeza kuwa mapato yatokanayo na madini yameanza kuongezeka, akibainisha kuwa mwaka 2017 sekta hiyo iliingiza Sh. milioni 166.094, lakini mwaka jana yaliongezeka na kufikia Sh. bilioni 1.436. Alisema mchango wa sekta hiyo katika Pato la Taifa umezidi kuongezeka, akieleza kuwa mwaka 2015, sekta hiyo ilichangia asilimia nne, lakini mwaka 2017 ilipanda hadi asilimia 4.8.

"Ila bado hatujafika tunapopataka, lengo letu ni ichangie asilimia 10 katika Pato la Taifa," alisema Rais Magufuli, huku akiagiza kuwekwe utaratibu maalum wa watu kuingia ndani ya machimbo ya Mirerani baada ya kupewa taarifa kuwa vijana wanaruka ukuta kuingia machimboni kusaka ajira.

Rais Magufuli aliitaka Wizara ya Madini kuhakikisha inafunga mashine maalum ya ukaguzi wa madini kama ulivyo utaratibu kwa wageni wanaoingia Ikulu.

"Sasa nakuagiza Biteko, ndani ya mwezi mmoja kuanzia sasa uwe umefunga kamera Mirerani, usipofanya hivyo nakufukuza, kwa maana watu wanarusha tanzanite nje ya ukuta halafu kunakuа na mtu mwingine nje anayejifanya anakokota punda lakini anaokota tanzanite hiyo," alisema Rais Magufuli.

Alimwagiza Waziri Biteko kuhakikisha anafuta umiliki wa maeneo ya uchimbaji madini ambayo yapo wazi na hayajaendelezwa.

Rais Magufuli alisema ununuzi wa dhahabu miaka ya nyuma uliokuwa unafanywa na Benki Kuu (BoT), ulishindikana kwa sababu kulikuwa na mchezo mchafu uliokuwa unafanywa na baadhi ya wafanyakazi wa BoT.

# Dakika 145 Mdee kikaangoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, akiwa mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, katika ofisi za Bunge jijini Dodoma jana, akiitikia wito wa tuhuma zinazomkabili za kulidhalilisha Bunge. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

KAMATI ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, jana imetumia saa 2:25 kumhoji Mbunge wa Kawe (Chadema), Halima Mdee, kutokana na wito wa Spika Job Ndugai wa kumtaka kufika kwenye kamati hiyo.

Mdee aliitwa mbele ya kamati hiyo kutokana na kuunga mkono kauli iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, ya kuliita Bunge ni dhaifu.

Mahojiano hayo kati ya Mdee na kamati yalifanyika jana katika ukumbi wa Spika wa Bunge, chini ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka.

Mdee aliwasili viwanja vya bunge saa 4:41 asubuhi akiwa amesindikizwa na Mbunge wa Bunda (Chadema), Ester Bulaya, ambaye alikuwa amembebea vitabu vya ripoti za CAG na nyaraka mbalimbali.

Kabla ya kuingia ukumbini, Mdee alikuwa ameketi nje ya ukumbi huku akipitia nyaraka mbalimbali katika vitabu hivyo.

Saa 5:03 asubuhi, Mdee aliingia kwenye ukumbi kwa ajili ya kohojiwa akiwa amebebewa vitabu na Bulaya na baada ya kumfikisha ndani ya ukumbi, alitoka na kuendelea na majukumu yake.

Akizungumza baada ya Mdee kuwasili kwa ajili ya kuhojiwa, Mwenyekiti Mwakasaka alisema: “Waandishi tunawashukuru, tunaomba tuendelee na kikao chetu.”

Pamoja na mahojiano hayo kufanyika kwa awamu kama ilivyo kuwa kwa CAG, kamati hiyo ilihitimisha saa 7:28 mchana.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, alisema kamati bado inaendelea na shauri la Mdee na itakapokamilisha itawasilisha ripoti kwa Spika kwa ajili ya hatua zingine.

Januari 7, mwaka huu, Spika Ndugai alimtaka CAG kufika mbele ya kamati kutokana na kauli aliyoitoa wakati akihojiwa na Kituo cha Televisheni cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa akiwa New York, Marekani, alikokuwa akihudhuria mkutano.

Sambamba na CAG, Ndugai alimtaka Mdee kuhojiwa na kamati kutokana na kuunga kauli ya CAG kwa madai kuwa imelidhalilisha Bunge.

# Kamati yabaini vitendo vya wanafunzi kulawitiana

**Na Futuna Seleman,** MKURANGA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani, imebaini kukithiri kwa vitendo vya kulawitiana kwa watoto wa kiume katika baadhi ya shule zilizopo wilayani humo.

Kufuatia hali hiyo, kamati hiyo imewataka wazazi, walezi na wadau wa elimu wilayani humo kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao.

Hayo yamebainika katika kikao cha wadau wa elimu kilichokuwa kikijadili changamoto za elimu wilayani humo, ushauri mapendekezo ya nini kifanyike kutatua changamoto zinazoikabili wilaya.

Kikao hicho kiliitishwa na Serikali ya Wilaya ya Mkuranga chini ya Mwenyekiti wake, Fillberto Sanga, kwa kuwashirikisha wadau wa elimu wakiwamo walimu, waratibu kata elimu, watendaji, madiwani viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa na watendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

"Kuweni makini na watoto wasioingia darasani, wakiulizwa wanasema na kutajana majina, nawaombeni sisi ni wazazi tuwe makini, mmepewa majukumu ya kulea watoto wafuatilieni,"...alisema mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo, ambaye hakupenda jina lake liandikwe gazetini.

Alisema ametokea Siha mkoani Kilimanjaro mchezo huo ulikuwapo, lakini wazazi walikuwa wakali vitendo hivyo vikamalizika.

"Muwe wakali muwachunguze na kutoa taarifa kwa walimu sitotaja shule naomba tujirekebishe kuweni makini na watoto wa kiume...(why) kwanini watoto hawaendi shuleni hali ni mbaya sana majina tunayo," alisema mjumbe huyo.

Alisema wanafunzi wanaofanyiana vitendo hivyo hufanyiana mazoezi ya darasani na kuyasahihisha ili waonekane wanahudhuria masomo yao.

"Huwezi kuamini wanafanyiana mazoezi wanasahihisha waonekane wanahudhuria darasani," alisema na kuwasisitiza wazazi kushirikiana na walimu kujua maendeleo ya watoto shuleni kwa kukagua kazi wanazofanya.

Awali Mwenyekiti wa kikao hicho Mkuu wa wilaya hiyo Fillberto Sanga, alikiri kuwapo kwa wimbi kwa vitendo vya kulawitiana kwa watoto wa kiume ndani ya wilaya hiyo katika baadhi ya shule.

Aliwasisitiza wazazi kulifuatilia suala hilo kwa undani kwa kuwa si jambo la kupuuzwa kwavile linaathiri kizazi cha leo.

Aidha, alipiga marufuku mashine za kuchezea kamari ndani ya wilaya hiyo ambazo alidai zinachochea uhalifu na matumizi ya madawa ya kulevya.

"Operesheni ondoa mashine isiwe chanzo cha mapato katika wilaya yetu, naagiza utoaji wa vibali inatosha kuendesha mashine hizi katika wilaya yetu, michezo hiyo inarudisha nyuma maendeleo ya elimu kwa vijana, madawa ya kulevya yanaenda sambamba na kamari," alisema Sanga.

Aidha alikemea tabia ya walimu wa kike kuwa na uhusiano na wanafunzi wa kiume na wa kiume kuwa na uhusiano na wanafunzi wa kike kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na maadili ya utumishi.

Wakitoa maoni mapendekezo katika kikao hicho baadhi ya wadau waliomba vijiwe vya wahuni vinavyochipua maeneo ya vijijini ambavyo vinaashiria vitendo vya uvunjifu wa amani na kusababisha vijana wengi kushinda huko badala ya kuhudhuria masomo vidhibitiwe kabla havijaendelea kuleta madhara kwa wanafunz na vijana wilayani humo.


LAWCASTLES

(Advocates and Project Lawyers)

**ENEO LINAUZWA LIKO SONGEA, RUVUMA TANZANIA**

**Nafasi Nzuri Kwa Wawekezaji Kupata Eneo Sehemu hii Ya Tanzania.**

Kwa niaba ya mteja wetu tunauza eneo ambalo liko katika vitalu namba 89 na 91 katika eneo law viwanda, Songea mjini. Pia eneo linafaa kwa shughuli zingine zilizoidhinishwa na mamlaka za serikali.

Eneo hili lina haki miliki (right of occupancy) ya miaka 33 likiwa na ukubwa wa mita za mraba 17,243.

**ENEO LILIVYO**

Eneo lote limezungushiwa uzio wa waya ukiunganishwa na nguzo imara za zege kuufanya uzio kuwa madhubuti, geti kubwa la chuma lenye magurudumu kwa ndani limeendelezwa kama ifuatavyo:-

- Ghala moja kubwa likiwa na ujazo wa mita za mraba 4,000, limejengwa kwa Saruji likiwa na nguzo imara, sakafu yake inazege rasharasha, limeezekwa kwa bati likichagizwa na mbao madhubuti na chuma.
- Choo cha kawaida kikiwa na mita za mraba 17.98
- Choo cha wafanyakazi kikiwa na mita za mraba 5.00
- Kibanda cha walinzi kikiwa na mita za mraba 6.00
- Chumba cha jenereta kikiwa na mita za mraba 9.00
- Eneo hili limeunganishwa na huduma za maji na umeme.

**Geneneta lipo kwa matumizi ya dharura panapotokea tatizo la umeme wa TANESCO.**

**NAMNA YA KUPAONA/MAWASILIANO**

**Mtu yeyote mwenye nia ya kununua anaweza kuwasiliana na wanasheria wanaomwakilisha muuzaji kwa kutumia namba za simu zifuatazo: - 022 22 2124127 / +255 688 943380 au kwa kutumia barua pepe kwenye e-mail hii info@lawcastles.com**

TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 31.12.2019

Imetolewa chini ya kanuni ya 32 kifungu namba 3 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2006

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 Decemba 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 31-Dec-18 | Robo Mwaka ya 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,844 | 1,481 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,879 | 3,915 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 41,310 | 41,517 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,017 | 2,014 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 10 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 40,737 | 59,044 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 34,386 | 27,347 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,565 | 4,740 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,203 | 1,207 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **130,941** | **141,276** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 44,720 | 40,303 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 8,757 | 8,675 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 6 | 24 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,650 | 1,562 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 238 | 505 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,053 | 2,474 |
| 28 | Madeni | 55,215 | 68,906 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **111,639** | **122,449** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **19,302** | **18,827** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (39,378) | (39,393) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (2,168) | (2,595) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 276 | 290 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **19,253** | **18,827** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 5,969 | 6,173 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,327 | 1,341 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,471 | 1,639 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15% | 13% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4% | 4% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 67% | 63% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 26% | 19% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89% | 91% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 9% | -25% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -7% | -23% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 Decemba 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-18 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 2,095 | 2,365 | 8,567 | 10,109 |
| 2 | Gharama za Riba | (542) | (886) | (2,872) | (4,839) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,553** | **1,479** | **5,696** | **5,270** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (32) | (5) | (37) | - |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,901** | **1,439** | **5,298** | **3,502** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 505 | 213 | 1,105 | 845 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,152 | 1,080 | 3,425 | 2,113 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 243 | 145 | 768 | 544 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(2,995)** | **(3,446)** | **(13,125)** | **(12,167)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (1,513) | (1,671) | (6,068) | (5,206) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (300) | (367) | (1,332) | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,183) | (1,408) | (5,724) | (6,960) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **427** | **(534)** | **(2,168)** | **(3,395)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **427** | **(534)** | **(2,168)** | **(3,395)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **427** | **(534)** | **(2,168)** | **(3,395)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 104 | 105 | 105 | 90 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 68 | (85) | (345) | (540) |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | 4 | 4 | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.31% | -0.51% | -1.49% | -1.79% |
| | (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 2.24% | -3.99% | -11.18% | -12.82% |
| | (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 74.95% | 101.40% | 94.66% | 85.04% |
| | (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.27% | 1.03% | 4.87% | 3.29% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 Decemba 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 31-Dec-18 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **427** | **(534)** | **(2,168)** | **(3,395)** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 289 | 232 | (2,306) | 359 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (7,039) | 1,446 | (7,039) | 6,194 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | 429 | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 4,499 | (16,426) | 12,526 | (16,313) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 207 | (419) | 207 | 4,212 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,421) | (401) | 9,749 | 101 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 174 | 1,155 | (6,644) | 6,452 |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | 1,397 | - |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | 568 | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(2,864)** | **(14,946)** | **6,720** | **(2,389)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (60) | (105) | (60) | (225) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 1 | - | 1 | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | (445) | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(60)** | **(105)** | **(504)** | **(225)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (13,691) | (23,760) | (3,457) | 29,916 |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **(13,691)** | **(23,760)** | **(3,457)** | **29,916** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(16,615)** | **(38,811)** | **2,759** | **27,302** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 42,483 | 81,294 | 81,294 | 79,673 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **25,868** | **42,483** | **84,053** | **106,975** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 Decemba 2018

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2018** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,454) | - | 351 | - | 21,421 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | (2,168) | - | - | - | (2,168) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | 76 | - | (76) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(41,546)** | **-** | **276** | **-** | **19,253** |
| **Mwaka uliopita 2017** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 28,125 | 21,194 | (33,995) | 290 | 407 | - | 16,021 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | (5,805) | - | - | - | (5,805) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 3,296 | 7,909 | - | - | - | - | 11,205 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | 290 | (290) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | 56 | - | (56) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | | | | | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(39,454)** | **-** | **351** | **-** | **21,421** |

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Usman Isiaka<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | ***Imesainiwa*** | ***23 Januari 2018*** |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | ***Imesainiwa*** | ***23 Januari 2018*** |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ***Imesainiwa*** | ***23 Januari 2018*** |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | ***23 Januari 2018*** |
| 2 | Emeke Iweriebor<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | ***23 Januari 2018*** |

215020302

UBA Africa's global bank

# Wadaiwa kuingiziwa chupa sehemu nyeti

**Na Salome Kitomari**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu, kimedai watuhumiwa watano waliokamatwa na polisi wilayani Ngorongoro waliteswa, kupigwa na kuingiziwa chupa sehemu za siri.

Aidha, watu hao waliteswa kwa madai ya kuiba mali za watalii kwenye kampuni ya Simba B, ambayo baadhi wanafanyia kazi na walikaa kwenye kituo cha polisi kwa siku 15.

Watuhumiwa hao ambao walirekodiwa kwa video wakieleza yaliyowakuta na kuonyeshwa mbele ya waandishi wa habari ni Peter Orkery, Musa Yahya, Kayanda Kisoki, Zakaria na Francis Arusha.

Kutokana na hali hiyo, wanaharakati hao wametangaza kuanzisha mpango wa kuwasaidia watuhumiwa wote wanaoteseka kwenye vituo vya polisi, kupaza sauti kupitia mitandao ya kijamii, ili kuwashinikiza polisi kuacha unyanyasaji wa raia.

Wakizungumza na waandishi wa habari, Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, Ofisa Programu wa LHRC, Paulo Mikongoti na Mtafiti wa LHRC, Tito Magoti, walisema matukio ya watu kuteswa, kujeruhiwa, kuuawa na kunyimwa haki zao wakiwa mikononi mwa polisi, yanaongezeka kila siku nchini.

"Tukichukua mfano wa tukio la Loliondo awali watu sita waliteswa na walikaa kituoni kwa zaidi ya siku saba na kuachiwa bila kufunguliwa kesi. Sasa kuna watu watano wamekaa vituo tofauti vya polisi kwa siku 15 na hawajafikishwa mahakamani na sasa wanauguza majeraha makubwa yaliyogharimu afya zao," alisema Mikongoti.

Alisema walipokamatwa na polisi walichukuliwa kwa ajili ya kutoa maelezo walipofika kituoni walifungwa kamba mikononi na miguuni kisha wakatundikwa juu na kuanza kupigwa hadi miguu kupasuka.

"Baada ya mahojiano watuhumiwa walidai kufanyiwa ukatili wa kutisha kwa kuingiziwa rungu za polisi na chupa sehemu za haja kubwa na kutakiwa kunusa. Hali zao ni mbaya na wengine bado wanauguza majeraha yaliyotokana na vipigo na ukatili waliofanyiwa na askari wa polisi kituo cha Loliondo," alisema Mikongoti.

Alisema baada ya kukamatwa Desemba 21, mwaka jana na kukaa mahabusu kwa siku 15 bila kuonana na ndugu zao, miguu ya baadhi ya watuhumiwa ilianza kuoza wakapelekwa mahakamani Januari 4, baadaye walilazwa hospitali ya Wasso kwa ajili ya matibabu na walifanyiwa upasuaji kwenye miguu na kutolewa usaha uliokuwapo kwenye miguu.

"Jeshi la Polisi limeundwa nchini kwa ajili ya kulinda amani, kusimamia sheria, kuzuia na kugundua uhalifu, kukamata wahalifu na kulima. Katika kuzuia uhalifu, kukamata na kuwaweka kuzuizini wahalifu, Jeshi la Polisi linapaswa kuongozwa na sheria imeweka haki mbalimbali za watuhumiwa," alisema.

Alizitaja haki hizo ni kuambiwa kosa analotuhumiwa nalo, kupewa dhamana, kuonana na ndugu, kupatiwa matibabu, kuhojiwa bila shuruti, kuhojiwa mbele ya mwanasheria, kupelekwa mahakamani kwa wakati pamoja na kuelezwa haki yake ya kupata msaada wa kisheria.

Nyingine kukaa mahabusu muda usiozidi saa 24, kupewa dhamana ya polisi muda wowote hata siku za Jumamosi na Jumapili, kulala mahali salama na safi, kutokupigwa au kufanyiwa ukatili wowote na kutendewa kibinadamu na kujali utu.

"Mara nyingine polisi wameshindwa kusimamia na kutekeleza kwa vitendo vipengele muhimu vilivyopo kwenye sheria na kusimamia haki za mtuhumiwa wakati wa ukamataji na wakiwa mahabusu," alisema Olengurumwa.

Alisema taarifa ya ufuatiliaji ya THRDC inaonyesha watuhumiwa wanafanyiwa ukatili mwingi wakati wa ukamataji, wakiwa vituoni na wakati wa mahojiano na polisi na kwamba ukatili unaoongoza ni kipigo, kukaa njaa, kulazwa mahala pasipo na utu na vitisho vya maneno.

Alisema wako watuhumiwa wameteseka mikononi mwa polisi kwa muda mrefu kinyume cha sheria na wengine kufariki, huku akimtaja Chacha Sagutu, aliyefia mikononi mwa polisi mwaka 2018 kutokana na kukiukwa taratibu za kisheria za kuwakamata na kuwaweka kuzuizini watuhumiwa.

# Ujenzi daraja la kisasa Gerezani wanukia

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, imesaini mkataba wa ujenzi wa daraja la Gerezani lenye urefu wa mita 40 na upana 30.4 wenye kutosha barabara sita za magari utakaogharimu Sh. bilioni 25.28.

Fedha za ujenzi huo ni msaada kutoka Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la Ushirikiano wa Kimataifa (JICA) na itajengwa na Kampuni ya Sumito Mitsui Construction ambayo pia ilijenga barabara ya juu ya Mfugale katika eneo la Tazara jijini Dar es Salaam.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (Tanroads), Mhandisi Patrick Mfugale, akielezea utekelezaji wa mradi huo jana, alisema utachukua miezi 24 na kwamba lengo ni kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam.

"Mradi wa ujenzi wa daraja la Gerezani ni sehemu ya miradi mingi ya mikakati ya kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji la Dar es Salaam ukiwamo mradi wa barabara za Kilwa kuwa njia nne," alisema Mhandisi Mfugale.

Alisema daraja hilo litapita juu ya treni ya kisasa ya umeme ambalo litakuwa na urefu wa mita saba kwenda juu na litakuwa na njia barabara sita za magari zikiwamo mbili za mwendokasi na njia za watembea kwa miguu.

Alisema usimamizi wa mradi huo utafanywa na Kampuni ya Kihandisi ya Ingerosec Corporation ya Japan kwa gharama ya Sh. bilioni 2.86 kati ya Sh. bilioni 25.28 ya mradi wote.


## UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED
## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES

| S/N | ITEM/TRANSACTION | | |
|---|---|---|---|
| SECTION A | SAVINGS ACCOUNTS | RETAIL | CORPORATE |
| 1 | FREEDOM SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 5,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | NIL | |
| 2 | GENERAL SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 | |
| | Minimum operating balance | TZS 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| 3 | EMPLOYEE SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS15,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 2,000 USD 10 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Adhoc statement request | TZS 1,000/ PAGE | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 4 | SAVINGS ACCOUNT INDIVIDUALS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 5 | SAVINGS ACCOUNT SALARY | | N/A |
| | Required minimum opening balance | 15,000 | |
| | Minimum operating balance | 5,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges @ Counter | TZS 1,000 | |
| 6 | SAVINGS ACCOUNT DOMICILARY | | |
| | Required minimum opening balance | USD10 | |
| | Minimum operating balance | USD 5 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | 1% per Transaction | |
| | Closing account | USD 5 | |
| 7 | U-CARE CHILDREN SAVINGS | | N/A |
| | Required minimum opening balance | TZS 20,000 USD 15 | |
| | Minimum operating balance | TZS 20,000 | |
| | Monthly maintanance fee | NIL | |
| | Withdrawal Charges | TZS 1,000 | |
| SECTION B | CURRENT ACCOUNTS | | |
| 1 | INDIVIDUAL CURRENT ACCOUNT | | BUSINESS CURRENT ACCOUNT |
| | Required minimum opening balance | TZS 30,000 | TZS 100,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 10,000 | TZS 100,000 |
| | Monthly maintenance fee | TZS 10,000 | TZS 12,000 |
| | Cash withdrawal at counter | 1 PER MILLE | TZS A/C 1 PER MILLE |
| | Closing account | TZS 10,000 | TZS 10,000 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 10% | TZS A/C PLR + 10% |
| 2 | DIPLOMAT ACCOUNTS | | |
| | Required minimum opening balance | USD 200 | N/A |
| | Minimum operating balance | USD 100 | N/A |
| | Monthly maintenence fee | NIL | N/A |
| | Cash withdrawal at counter | NIL | N/A |
| | Closing account | NIL | N/A |
| | Penalty for overdrawn account | NIL | N/A |
| | Outward fund transfers(TTs) | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 200 | N/A |
| | Inward fund transfers(TTs Incoming) | NIL | N/A |
| | FOREX exchange | Favourable rates will be applied | N/A |
| 3 | DOMICILIARY CURRENT ACCOUNT | | |
| | Required minimum opening balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Minimum operating balance | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 | USD 100/ EUR 100/ GBP 100 |
| | Monthly maintenence fee | USD 12 or its equivalent | USD 15 or its equivalent |
| | Minimum search fees | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 | USD 25/ EUR 25/ GBP 25 |
| | Cash withdrawal | 1% per Transaction | 1% per Transaction |
| | Cheque book - 25 LEAF | USD 10 or its equivalent | N/A |
| | Closing account | USD 10 | USD 10 |
| | Penalty for overdrawn account | PLR + 2% | PLR + 2% |
| | Transfer From TZS to DOMICILIARY/ DOMICILIARYto TZS | NIL | NIL |
| SECTION C | DEPOSIT ACCOUNTS | | |
| 1 | Call Accounts | | Call Accounts |
| | Minimum opening balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum operating balance | TZS 1,000,000 | TZS 10,000,000 |
| | Monthly Average balance requirement | Negotiable | Negotiable |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| 2 | Term Deposits | | Term Deposits |
| | Minimum deposit - local currency | TZS 500,000 | TZS 10,000,000 |
| | Minimum deposit - USD | USD 1,000 | USD 10,000 or equivalent |
| | Interest Rates | Negotiable | Negotiable |
| SECTION D | ELECTRONIC BANKING | | |
| 1 | E-Banking | | E-Banking |
| | Internet banking monthly subscription | TZS 2,000 Per Month. | TZS 10,000 per Month |
| | Internet banking ( Re issue pin) | TZS 5000 | TZS 5000 |
| | U - Direct (Reversal of transaction) | TZS 4000 | TZS 4000 |
| | E-statement (self downloaded) | FREE | FREE |
| | POS purchase (Local) | FREE | N/A |
| | POS purchase (International) | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| | ATM reversal | TZS 1,000 per transaction | N/A |
| | Fund transfer/ company load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Card Load | TZS 1,000 per transaction | TZS 1,000 per transaction |
| | Manual pin change | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per transaction |
| | U-MOBILE(mobile banking-Bank to wallet) | TZS 1,000 (0 - 200,000/=) and TZS 2,000 (200,001 - 400,000/=) | N/A |
| | Card to card transfer | TZS 1,500 per transaction | TZS 1,500 per tr |
| | Africash | TZS 6000 + 1.5% of the amount sent/USD 4.45 + 1.5% | N/A |
| 2 | Visa Debit Card | | N/A |
| | Issuance fees | TZS 10,000 | |
| | Re-issuance fee | TZS 10,000 | |
| 3 | Visa Perapid Cards | | N/A |
| | Issuance fees for instant card | TZS 12,000 | |
| | Issuance fees for personalized card | TZS 16,000 | |
| | Re-issuance fees | TZS 12,000 | |
| | Online Passcode reset fee | TZS 1,500 | |
| | ATM Pin reset fee | TZS 1,500 | |
| | Loading fee | TZS 1,000 | |
| | Online shopping fee - Local transactions | FREE | N/A |
| | Online shopping fee/Web - Int. transactions | TZS 6000 (up to 1000$) TZS 10,000 ($1001 - $2000) TZS 20,000 (Above $ 2000) | N/A |
| 4 | ATM Withdrawals | | N/A |
| | At UBA ATMs (On us) | TZS 500 | |
| | ATM Balance inquiry(Local) | TZS 200 | |
| | ATM Balance inquiry(international) | TZS 1000 | |
| | To other banks ATM (On others/OFF US)Local | TZS 2,500 | |
| | international ATM withdraw | TZS 6000 | |
| SECTION E | ASSET BANKING | | |
| 1 | LOANS | | |
| | Processing fee | negotiable | 2% |
| | Insurance for personal loans | N/A | 1.50% |
| | Legal fees | 0.5% minimum of TZS 300,000 | 0.5% minimum of TZS 300,000 |
| 2 | TEMPORARY OVERDAFT (TODs) | | |
| | Processing fee | 2% | 2% |
| SECTION F | TRADE FINANCE | | |
| 1 | Guarantees | | Guarantees |
| | Facility Commission | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qrt. | 2% p.a (0.5% per qtr). Min USD 250 per qtr. |
| | Arrangement fees | 2% | 2% |
| | Cash Covered | 0.5% per qtr Min 250 per qtr | 0.5% per qtr Min 250 per qtr |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| | Extension to next quarter | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) | 0.5% per qtr ( Or % of the agreed rate) |
| | Amount increase | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) | 0.5% /qtr on the diff ( Or % of the agreed rate) |
| 2 | Letters of Credit - Imports | | Letters of Credit - Imports |
| | Issuance commision | 0.5% per quarter. Min USD 150. | 0.5% per quarter. Min USD 150. |
| | Handling Fees | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Amendment | USD 100.00 flat | USD 100.00 flat |
| 3 | Letters of Credit - Exports | | Letters of Credit - Exports |
| | LC Advising Commission | USD 200 flat | USD 200 flat |
| | Amendment advising commision | USD 100 Flat | USD 100 Flat |
| | Correspondences Swift charge | USD 50 flat | USD 50 flat |
| | Documents handling and examination fee | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 | 1.5% of invoice amount ,min usd 200 |
| | Courier charge | USD 100 flat | USD 100 flat |
| | LC confirmation charges | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) | 1.5% per quarter (only for confirmed usance lcs) |
| 4 | Letters of Credit Refinancing | | Letters of Credit Refinancing |
| | Interest on refinance | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on refinance | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 5 | Discounting on LC/Invoice/Cheque | | |
| | Interest on discounting | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 | LIBOR + 8% p.a of value. Min USD 100 |
| | Commission on discounting | USD 50 flat | USD 50 flat |
| 6 | Bills Discounting (Bills of exchange including cheques) | | |
| | Interest on discounting | PLR +3%-local; International Lobor+8% | PLR +3%-local; International Lobor+8% |
| 7 | Documentary Collection - Export | | |
| | Handling charge | 0.25% of the invoice min USD 100 flat | 0.25% of the invoice min USD 100 flat |
| | Courier charge | USD 100 | USD 100 |
| | Corespondence commission | USD 50 Per tracer | USD 50 Per tracer |
| 8 | Documentary Collection - Import | | |
| | Handling Commission | 0.25%. Min USD 100 | 0.25%. Min USD 100 |
| | correspondence Swift charge | USD 50 | USD 50 |
| 9 | Outward Bills for Collection (clean collections & TCs) | | |
| | Handling Commision | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent | 0.25% of value, min USD 75 or its equivalent |
| | Dhl charges | usd 75 flat | usd 75 flat |
| | Returned foreign cheques | claimed charges + locally un re-covered charges | claimed charges + locally un re-covered charges |
| 10 | Inward Bills for Collection | | |
| | Handling Commission | USD 50 flat per collection | USD 50 flat per collection |
| | Swift charged | USD 40 flat per collection | USD 40 flat per collection |
| 11 | Local Currency Transactions | | Local Currency Transactions |
| | Outward remittances (TISS) | TZS10,000 PER TRANSACTION | TZS10,000 PER TRANSACTION |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT | TZS 10,000.00 OR ITS EQUIVALENT |
| | Inward Swift Transfers (TISS) | NIL | NIL |
| 12 | Foreign Currency Transactions | | Foreign Currency Transactions |
| | Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50 in between 0.25% MAX USD 500 |
| | Telegraphic Overseas Charges/ OURS | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) | USD/EUR/GBP 35 FLAT (OURS) |
| | Amendment fee for Outward remittances / Swift / Telegraphic Transfers by customer or by bank | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | Inward Swift Transfers | USD 10 FLAT | USD 10 FLAT |
| | International Money Order (IMO) | USD 30 per IMO | USD 30 per IMO |
| | Foreign cheques for collection | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; | 0.25% of value. USD 75 min; USD 250 max; |
| SECTION G | OTHERS | | |
| 1 | Statements | | Statements |
| | Monthly | FREE | FREE |
| | Adhoc requests | TZS 1,000/ PAGE | TZS 1,000/ PAGE |
| 2 | Cheque Books Issuing | | Cheque Books Issuing |
| | - 25 Leaf | TZS 15,000; USD 10 | N/A |
| | - 50 Leaf | TZS 30,000; USD 20 | N/A |
| | - 100 Leaf | TZS 45,000; USD 30 | TZS 45,000; USD 30 |
| | Counter cheque request | TZS 20,000; USD 10 | TZS 20,000; USD 10 |
| | Cheque Stop payment instructions | leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; | Leaf lost: TZS 20,000; Book lost: TZS 40,000; |
| | Issuance of Manager's cheque | TZS 25,000; USD 20 per item | TZS 25,000; USD 20 per item |
| | Managers cheque cancellation charges | FREE | FREE |
| 3 | Standing order | | Standing order |
| | Standing order set-up | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Standing order maintanance | NIL | NIL |
| | Standing order/Foreign Bank (TT charge) | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 | MIN USD 50; 0.25% MAX USD 500 |
| | Amend / Stop standing Order | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent | TZS 10,000; USD 10 or its equivalent |
| | Unpaid standing order | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent | TZS 40,000; USD 40 or its equivalent |
| 4 | Insufficient funds/effects not cleared | | Insufficient funds/effects not cleared |
| | Effects not cleared | **ITEM REMOVED** | **ITEM REMOVED** |
| | Insufficient Funds (Refer to drawer) | TZS 50,000; USD 50 | TZS 50,000; USD 50 |
| 5 | Other services/charges | | |
| | Retriving old documents (2-6 months) | TZS 10,000; USD 10 | TZS 10,000; USD 10 |
| | Retriving documents (6 months and above) | TZS 15,000; USD 15 | TZS 5,000; USD 15 |
| | Confirmation/Audit/ Certificate of balance | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent | TZS 50,0,000; USD 25 or its equivalent |
| | Status enquiry / Reference Letters | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent per customer request | TZS 25,000; USD 25 or its equivalent |
| | Manual processing of salaries | TZS 1,000; USD1 or its equivalent | TZS 1,000; USD1 or its equivalent |
| | Closure of Account | TZS10,000 | TZS10,000 |
| | Dormant Account Reactivation | FREE | FREE |
| | Cash handling fee-COINS ONLY | 9% of the Deposit | 9% of the Deposit |
| 6 | Soiled notes | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| 7 | Coins | 3% of principal amount | 3% of principal amount |
| | **approved by:** | | |
| | **Signature:** | | **Signature:** |
| | Flavia Kiyanga | | Chomete Hussein |
| | **Ag: Chief Operating Officer** | | **Country Chief Finance Officer** |
| | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** | | **United Bank for Africa (Tanzania) Ltd** |

**Disclaimer: All fees are VAT exclusive.**

215020002

United Bank for Africa (Tanzania) Limited is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, one of Africa's leading financial institutions offering universal banking to more than 7 million customers across 750 branches in Africa , USA and Europe.

Africa: Tanzania, Kenya, Uganda, Benin, Liberia, Ghana, Gabon, Senegal, Cameroon, Zambia, Guinea, Sierra Leone, Chad, Burkina Faso, Cote d'Ivoire, Nigeria
Europe: London, Paris
USA: New York

UBA Africa's global bank

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madudu chanjo mifugo wahusika wawajibishwe

**WAZIRI** wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amefichua madudu ya kutisha katika biashara ya chanjo za mifugo na kumwagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kuandaa haraka mwongozo utakaosimamia mfumo mzima wa uzalishaji, uagizaji, usambazaji na uchanjaji wa mifugo.

Aidha, mwongozo huo unatakiwa kuweka bei elekezi itakayowezesha wafugaji kupata chanjo kwa gharama nafuu.

Mpina alitangaza hatua hiyo baada ya kubaini kuwa kwa miaka mingi wafugaji wamefanyiwa dhuluma kubwa kwa kuuziwa chanjo zaidi ya mara tano ya bei halisi licha ya baadhi ya chanjo hizo kuzalishwa na Taasisi ya Chanjo za Mifugo Kibaha (TVI), ambayo ni taasisi ya serikali iliyopewa jukumu la kurahisisha upatikanaji wa chanjo na kwa gharama nafuu.

Waziri Mpina alisema taifa limefikia hapo kutokana na kukosekana usimamizi madhubuti wa utoaji chanjo nchini hali iliyochangia kuwakatisha tamaa wananchi kuhudumia mifugo yao na kusababisha mingi kufa kwa kukosa chanjo, ambapo alisisitiza kuwa serikali haitakubali dhuluma hiyo iendelee.

Akizungumza baada ya kutembelea TVI na Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Mpina aliweka wazi jinsi wafugaji wanavyidhulumiwa akisema TVI inazalisha na kuuza chupa ya chanjo ya kimeta kwa Sh. 20,000 yenye uwezo wa kuchanja ng'ombe 100, ambapo kila ng'ombe mmoja hutakiwa kugharamia Sh. 200, lakini halmashauri, maofisa mifugo na wafanyabiashara wengine wanachanja kwa Sh. 5,000 kwa ng'ombe mmoja sawa na gharama ya Sh. 1, 000,000 kwa chupa.

Kwamba Chanjo ya mdondo TVI mnauza kwa Shilingi 22, lakini wao wanaokwenda kuchanja wanawatoza wananchi Shilingi 100 kwa kuku mmoja, wananchi wengi wamevunjwa moyo kuhudumia mifugo yao kutokana na utaratibu uliopo haueleweki na hauna msimamizi.

Vitendo hivi sio ufisadi tu bali ni dhuluma kubwa kwa wafugaji nchini na uhujumu wa uchumi wa taifa. Kimsingi vitendo hivi kama vitaachwa viendelee vitarudisha nyuma sekta ya ufugaji nchini.

Haiwezekani watu wachache ndani ya halmashauri, maofisa mifugo na wafanyabiashara wengine kufikiria maslahi yao badala ya maslahi mapana ya wafugaji nchi nzima kwa kuchanja mifugo kwa gharama kubwa ambazo ni kinyume.

Hatua ya Waziri Mpina ya kumwagiza Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kuandaa haraka mwongozo utakaosimamia mfumo mzima wa uzalishaji, uagizaji, usambazaji na uchanjaji wa mifugo ni nzuri pamoja na mwongozo huo unatakiwa kuweka bei elekezi itakayowezesha wafugaji kupata chanjo kwa gharama nafuu.

Hata hivyo, ipo haja kubwa ya kuwarejeshea matumaini wafugaji wetu ambao wameshakatishwa tamaa kutokana na kubebeshwa gharama kubwa za uchanjaji ambazo haziendani na gharama halisi.

Kuwarejeshea matumaini ni kuhakikisha kwamba serikali na taasisi zinazoshughulikia mifugo kuweka wazi gharama elekezi za uchanjaji mifugo ili kuwadhibiti wanaotumia mwanya huo kujinufaisha.

Aidha, hatua za kinidhamu na za kisheria zichukuliwe dhidi ya wale wote waliohusika na dhuluma hiyo, ambayo kwa kiasi kikubwa imewaathiri sana wafugaji.

Hatua hizi zikichukuliwa, bila shaka zitawarejeshea morali wafugaji, ambao wana mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu, kwa kuzingatia kwamba sekta ya ufugaji ina mchango mkubwa katika uchumi na ni tegemeo katika kufikia uchumi wa viwanda kwa kuzalisha malighafi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**RIZIKI NI MAFUNGU**
**WATU WENGI WANAAMINI KUWA RIZIKI INATOKA KWA MUNGU NA KILA MMOJA WETU ANA FUNGU LAKE. PAMOJA NA KUWA HIVYO, TUSIKAE DEBWERE. KUFANYA KAZI TENA KAZI HALALI NI SEHEMU YA FUNGU HILO. BILA KAZI HAKI YA KULA HAKUNA. NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



# Taasisi za kitaaluma zianike ufumbuzi wao kwa wananchi

Na Raphael kibiriti

**KATIKA** dunia ya leo, sayansi na teknolojia ina mchango mkubwa katika ustawi wa maisha ya binadamu, na kimsingi ni takriban katika kila hatua ya maisha yake.

Na ndiyo maana mojawapo ya viashiria vinavyoweza kwa ufasaha kutumika kama kipimo cha nchi kupiga hatua za kimaendeleo ni kuangalia ilivyofanikiwa katika uga huu.

Ongelea mataifa yote yenye uchumi mkubwa duniani, Marekani, China, Japan, Ujerumani, Uingereza, India, Ufaransa, Italia kwa kuyataja machache, maendeleo yao yamechangiwa na mafanikio makubwa ya sayansi na teknolojia.

Tunahitaji sayansi na teknolojia karibu katika kila hatua ya maisha, kwa mfano kutibu magonjwa kama vile saratani au kuweka miadi kwa ajili ya tiketi ya basi, treni, ndege au teksi.

Aidha, tunahitaji sayansi na teknolojia kutatua changamoto za kielimu, lishe, maji safi na salama, miundombinu na zingine zinazokwamisha maendeleo ya watu.

Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zimewekeza vilevile katika dhima nzima ya kuwa na wanasayansi wa kutoa ufumbuzi wa matatizo yanayoikumba jamii ya Kitanzania.

Toka enzi ya Mwalimu, Serikali imewekeza katika somo la sayansi na teknolojia shuleni na vyuoni kuliko na idara za fani mbalimbali za uga huo.

Hata hivyo, bado mchango wa wanasayansi nchini haujatumika kikamilifu kutatua changamoto zinazowakabili wananchi na taifa kwa ujumla wake.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba tafiti, bunifu na vumbuzi mbalimbali zilizofanyika hadi sasa nchini, zimebaki zimehifadhiwa katika mafaili ama makabati shuleni, vyuoni ama kwenye tume, vyama na taasisi za kitafiti.

Kumbe zilipaswa kusaidia wananchi kuboresha maendeleo ya kilimo, Tanzania ya viwanda, tiba na madawa, uhandisi, majisafi na majitaka, mazingira na maeneo mengine muhimu.

Ni kwa maana hiyo basi Muungwana anapongeza hatua iliyochukuliwa na wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) ya kuweka hadharani uvumbuzi wao kwa umma.

Wanafunzi wa vyuo hivyo wamevumbua teknolojia ya kudhibiti foleni katika huduma za umma, utakaoanza kutumiwa hospitalini na katika benki muda si mrefu.

Uvumbuzi huo ni zao la warsha ya wiki mbili ya hivi karibuni ya wanataaluma na wanafunzi kutoka vyuo hivyo nchini na Taasisi ya Teknolojia ya Massachusetts (MIT) yenye makazi yake nchini Marekani.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano wa DIT iliyoandaa warsha hiyo, Dk. Joseph Matiko, kupitia simu za mkononi, wagonjwa na wateja wa benki watakuwa wakichunguza hali ya msururu ilivyo kabla ya kwenda hospitalini au benki.

Ni katika kudhibiti mlundikano wa wagonjwa ama wateja hospitalini au benki na kwamba muda si mrefu wataiingiza teknolojia hiyo kwenye kampuni za simu ili zitoe namba maalumu za kupiga kupata huduma inayotakiwa.

Dk. Matiko anaongeza kwamba kwa upande wa hospitali, wagonjwa watakuwa na fursa pia ya kuchagua hospitali wanayoikusudia na kuuliza kama kuna daktari wa magonjwa yanayowakabili.

Muungwana anaona kitendo kilichofanywa na wanafunzi na vyuo husika cha kuweka uvumbuzi wao hadharani ili uanze kutumiwa na wananchi una tija.

Aidha, unafaa kuigwa na shule ama vyuo vingine vilivyo na vumbuzi zao kwenye makabati ama mafaili.

Muungwana anasema hivyo kwa sababu ana imani kwamba hakuna asiyejua tatizo la foleni hospitalini ama katika sekta za kibenki lilivyo.

Tuna matatizo mbalimbali kwa mfano ya wakulima nchini kuanzia kwenye changamoto ya mbolea, dawa, mbegu, masoko, mitambo rafiki ya kilimo, zote zikihitaji sayansi na teknolojia kwa ajili ya kukabiliana nazo.

Wakati umefika wa kuweka wazi tafiti, uvumbuzi na ubunifu unazofanywa na wanafunzi na vyuo vyetu nchini ili zitumike kwa ustawi wa wananchi na taifa kwa ujumla wake kama walivyofanya wanafunzi na vyuo vya SUZA na DIT.

## TANGAZO

MeTL GROUP
The People's Brand

BAJAJ MOTORCYCLES



# SAFARI YA KUSTAAJABU

MeTL inayo furaha kubwa kuwajulisha Watanzania wote kuwa MeTL sasa ni wasambazaji walioidhinishwa wa pikipiki za BAJAJI BOXER nchini Tanzania. Tunawakaribisha kwa furaha wote kwenye familia ya Metl.

MAWASILIANO

MOHAMMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED
P.O BOX 22196, BP ROUNDABOUT, GEREZANI STREET, DSM, TANZANIA
PHONE: +255 693 454 995 | TOLL FREE: 0800710060
EMAIL: BIKES@METL.NET

# Aua mke kwa panga kisa kulazimisha mtoto kwenda shule

**Na Ibrahim Yassin,** KYELA

MKAZI wa Kijiji cha Busale Kata ya Busale wilayani Kyela mkoani Mbeya, Zawadi Daudi (41), anadaiwa kuua mkewe, Hawa Kamwela (32), kwa kumcharanga kwa panga kwa madai kuwa anamlazimisha kumpeleka mtoto shule kuanza kidato cha kwanza.

Jirani wa mtuhumiwa, Said Mumba, alisema mgogoro kati ya mtuhumiwa na mkewe ulianza baada ya mtoto wao, Siri Zawadi (14), alipochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mkewe na mkewe kumweleza wafanye maandalizi.

Alisema wakati mama wa mtoto huyo akimweleza mumewe waanze maandalizi ya mtoto kwa kumnunulia mahitaji ya shule, mumewe alisema hana pesa na hayuko tayari kumpeleka mtoto shule, na kuwa baada ya hapo mwanamke huyo alikwenda kushtaki katika ofisi ya kata akitaka kujua sababu ya mumewe kukataa.

Aida Maonwa, mwenyekiti wa kijiji hicho, alisema alipata mshtuko baada ya mtuhumiwa kufanya mauaji hayo na kwamba chanzo chake ni mtuhumiwa kugoma kumpeleka mtoto shule kwa madai hana pesa za kumnunulia mahitaji.

Alisema baada ya kesi kufika ofisi ya kata, mtuhumiwa aliitwa, lakini hakufanya hivyo na alipotafutwa alikuwa akipiga chenga, akitaka shauri hilo lipelekwa mahakamani ambapo mahakama ilimtumia wito, lakini hakufika na alipofuatwa nyumbani hakuonekana.

Diwani wa kata hiyo, Adam Kapeta, alithibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kwamba kwa kushirikiana na vikao vya Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) wataanza kutoa elimu kwa wananchi hasa wazazi kuwapeleka watoto shule.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei pichani), alisema kuwa askari walikwenda eneo la tukio na kuuchukua mwili huo kisha kuupeleka hospitali, na kwamba katika uchunguzi wa kitabibu ilibainika aliuawa kwa kupigwa na vitu vyenye ncha kali.



Alisema baada ya vipimo waliruhusu familia kuuchukua mwili huo kwa ajili ya taratibu za mazishi, huku wakiendelea kumsaka mtuhumiwa.

"Jeshi la Polisi limejipanga kikamilifu kuhakikisha linamsaka mtuhumiwa huyo na kumfikisha mahakamani," alisema Matei.

# DC amsweka ndani diwani wa Chadema

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amemsweka ndani Diwani wa Kata ya Isyesye, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Ibrahim Mwampwani (Chadema), akimtuhumu kujichukulia sheria mkononi kwa kufunga ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo kutokana na kutoelewana.

Ntinika alichukua uamuzi huo jana baada ya Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Ester Mizel, kutoa taarifa ya diwani huyo kuvunja kufuli lililokuwa limetumika kufunga ofisi hiyo na kuifunga kwa kutumia kufuli lingine, hivyo kusababisha wananchi kukosa huduma.

Mizel alisema mgogoro kati yake na diwani huyo ulianza tangu alipohamishiwa kwenye kata hiyo, akidai kuwa alikuwa anampa vitisho kuwa atahakikisha anamwondoa kwenye ofisi hiyo.

Alisema diwani huyo alianza kutoa vitisho hivyo akidai kuwa maofisa watendaji hao wamepelekwa kwenye kata zao na Chama Cha Mapinduzi (CCM), ili wakwamishe shughuli za maendeleo wanazozifanya madiwani wa upinzani.

"Aliwahi kuniambia kuwa tumeletwa ili tuwakwamishe kwenye uchaguzi, hivyo akadai kuwa watatuchomea nyumba zetu na mimi mwenyewe nihakikishwe nalindwa muda wote kitu ambacho naamini serikali haiwezi kukifanya," alisema Ester.

Alisema mgogoro huo ulisababisha diwani huyo ajichukulie sheria mkononi kutokana na kutoelewana kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Sekondari ya Isyesye na kwamba waliwahi kuitwa na ofisa utumishi wa jiji kwa ajili ya kuhojiwa.

Kwa mujibu wa Mizel kwenye mahojiano hayo, Ofisa Utumishi alibaini kuwa tatizo ilikuwa mawasiliano na kwamba kwake hakukuwa na tatizo na kwamba endapo angebainika kuwa na tatizo angechukuliwa hatua.


SHIRIKA LA UMEME TANZANIA (TANESCO)

TAARIFA KWA UMMA



DOMINICK KAZINJA

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) linautaarifu Umma kuwa, Mfanyakazi wake Bw. Dominick Kazinja anatafutwa na mwajiri wake kwa tuhuma za kinidhamu.

Yeyote atakayemuona au mwenye taarifa zake, tafadhali tunaomba atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu au Ofisi ya TANESCO. **RB Namba BND/RB/1142/2018.**

**IMETOLEWA NA: OFISI YA UHUSIANO**
**TANESCO MAKAO MAKUU**
**JANUARI 22, 2018**

215019602

## HABARI KITAIFA

# Takukuru yawapa salamu wagombea

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Shinyanga, imewatahadharisha wagombea katika uchaguzi ujao wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu wanaotoa rushwa kuwa watashughulikiwa ipasavyo.

Imesema watu ambao wana tabia ya kukusanya watu na kuwapa chakula na fedha ili kuwarubuni wawachague hawataonewa huruma pindi watakapojulikana.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Kaimu Kamanda wa Takukuru Mkoa wa Shinyanga, Francis Luena, wakati akitoa taarifa ya utendaji kazi ya miezi mitatu kuanzia Oktoba hadi Desemba, mwaka jana, alisema taasisi hiyo imejipanga kutoa elimu ya rushwa kwa wananchi na wagombea wa uchaguzi kupitia mikutano ya hadhara.

Elimu ambayo itatolewa kwa wananchi na wagombea hao, kwa mujibu wa kamanda huyo, ni juu ya makosa ya rushwa wakati wa uchaguzi, Sheria ya Gharama za Uchaguzi Na. 6 ya mwaka 2010, na makosa yaliyomo kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Na. 11 ya mwaka 2007, ili kuhakikisha wagombea na hata washindi wa uchaguzi wanapatikana kihalali.

"Katika kipindi cha uchaguzi huwa kuna njia nyingi sana za utoaji rushwa kwa wagombea, hivyo tunapenda kuwatahadharisha kwamba tumejipanga na tuko vizuri hatutamwacha mtu salama. Wale ambao huwa wanapenda kufanya hafla ya vyakula kwa wananchi nao tutawabana kwa kuwa huko ni kufanya ushawishi ili wakuchague," alisema Luena.

"Natoa wito pia kwa wananchi mkoani Shinyanga kuwa mwaka huu ni wa uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa na baadhi ya wagombea wameshaanza kupitapita katika mitaa, vijiji na vitongoji. Taarifa hizo tunazo, hivyo nawaomba kuwa makini wasikubali rushwa bali wafanye uchaguzi sahihi kwa viongozi makini," aliongeza.

Naye Mwanasheria wa Takukuru mkoani Shinyanga, Sengeko Mndambi, alisisitiza kuwa kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi, hafla ya vyakula kuelekea kipindi cha kampeni pamoja na kusafirisha wananchi kwenye mikutano ni rushwa na kuwataka wagombea wote waepukane na vitendo hivyo ndipo watakuwa salama.

# Hasunga, rais wa ushirika duniani wateta mazito Dar

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, juzi alikutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Duniani (ICA), Dk. Ariel Guarco, katika ukumbi wa wizara, maarufu kama Kilimo I, jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo uliotanguliwa na ziara ya kutembelea maeneo mbalimbali ya vyama vya ushirika jijini Dar es Salaam, huku rais huyo akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa ICA, Bruno Roelants.

Katika msafara huo pia walikuwapo Rais wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika Afrika, Japhet Magomere na Katibu Mkuu wa Shirikisho la hilo barani Afrika, Chiyoge Sifa.

Katika mkutano huo, Hasunga alimhakikishia kiongozi huyo kuwa serikali ya awamu ya tano imedhamiria kuboresha ushirika ikiwa pamoja na kuondoa changamoto za muda mrefu kwenye vyama vya ushirika ikiwamo kushughulikia viongozi wabadhirifu.

**Dhana ya kuchagua viongozi wa ushirika wenye sifa ya kujua kusoma na kuandika imepitwa na wakati, hivyo kuna kila sababu ya kuchagua viongozi wenye weledi na utashi katika utendaji.**

Hasunga alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo iko katika mapitio ya sifa za viongozi wa vyama vya ushirika nchini, ili kupata viongozi watakaoongoza kwa weledi sekta ya ushirika.

Alisema dhana ya kuchagua viongozi wa ushirika wenye sifa ya kujua kusoma na kuandika imepitwa na wakati, hivyo kuna kila sababu ya kuchagua viongozi wenye weledi na utashi katika utendaji.

Hasunga pia alisema mfumo wa ushirika ni nyenzo muhimu ambayo ukitumika vizuri utasaidia kuondoa umaskini wa wakulima nchini na duniani kote, hivyo kuimarisha uanzishwaji wa viwanda kuleta tija katika kilimo, hivyo ni lazima kuwa na juhudi za makusudi kuwa na viongozi wenye weledi.

Waziri alisema wizara yake pia imeanza kupitia upya Sheria ya Vyama vya Ushirika ili kuwa na ushirika imara na wenye nguvu na tija kwa wakulima, kwa kuwa kufanya hivyo kutaongeza imani ya wananchi walioukata tamaa na ushirika.

Pia alisema miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya ushirika nchini ni kukosekana kwa taarifa sahihi za wanachama kuanzia vyama vya msingi hadi vyama vikuu vya ushirika jambo ambalo kwa muda mrefu limesababisha kuwa na ushirika usio na tija na manufaa kwa wakulima wanaotumia nguvu na rasilimali zao nyingi katika kilimo.

Naye Dk. Guarco alisema msingi wa ziara yake Afrika Mashariki pamoja na nchi zingine ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wake. Alianzia ziara yake nchini Kenya na baadaye Rwanda kabla ya Tanzania.

Alisema kuwa Tanzania ni miongoni kwa nchi zilizoko chini ya Jangwa la Sahara ambayo imepokea vyema dhana ya ushirika, huku serikali ikiunga mkono kwa kiasi kikubwa, hivyo ana imani kuwa miaka michache ijayo kupitia mfumo huo, wakulima watakuwa na mafanikio yasiyopimika.

Dk. Guarco alisema amezuru nchini Tanzania kwa ajili ya kuonana na kufanya mazungumzo na wana ushirika ikiwa ni sehemu ya kubaini na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto mbalimbali kwenye sekta hiyo.

Pia alisema ziara hiyo ni sehemu ya kuendeleza na kuimarisha uhusiano uliopo baina ya Tanzania na shirikisho hilo.



Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Jesca Mbogo (katikati mwenye miwani na shada), akipokelewa na vijana wa kikosi cha ulinzi cha chama hicho 'Green Guard' wilayani Muheza, mkoani Tanga, alipowasili katika Shule ya Msingi ya Mbaramo kukagua ujenzi wamabweni mawili ya wanafunzi wa elimu maalum. Mwenye baibui ni Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo na kulia ni Katibu wa UVCCM Wilaya ya Muheza, Salome Ziwakuu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# TFS yapewa tano uhifadhi misitu

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili, imeimwagia sifa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kwa kazi nzuri inayoifanya ya kuhifadhi na kulinda misitu nchini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Nape Nnauye, alitoa pongezi hizo baada ya kamati hiyo kufanya ziara ya siku mbili katika Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa. Katika ziara hiyo, kamati ilizungumza na wadau wa misitu nchini na kutembelea maeneo mbalimbali ya shamba la miti la Sao Hill.

Alisema misitu mingi ambayo bado iko katika sehemu mbalimbali za nchi ni ishara tosha ya kazi kubwa inayofanywa na TFS.

Kuhusu malalamiko kutoka kwa wadau wa misitu nchini pamoja na rushwa dhidi ya TFS, alisema yamepungua kwa kiasi kikubwa, ikiwa ni ushahidi tosha kuwa TFS inafanya kazi nzuri.

Pia mwenyekiti huyo alitaka Wizara ya Maliasili na Utalii iharakishe mchakato wa kuandaa sheria itakayoiwezesha TFS kuwa na mamlaka kamili ya kusimamia na kulinda misitu yote nchini.

Alisema wizara hiyo ikishafanya kazi yake ya kuandaa sheria hiyo ambayo itaiwezesha kamati kuchagiza bungeni, ili mchakato wa kufanya TFS kuwa mamlaka kusimamia misitu yote nchini uende kwa kasi zaidi.

"Kamati yangu inataka kuona misitu ya halmashauri na misitu ya vijiji inasimamiwa na TFS. Tunaamini uharibifu unaoendelea utapungua kwa kiasi kikubwa," alisema.

Katika hatua nyingine, Nape alipambanua kuwa kazi ya kamati yake ni kushauri, kukosoa na kupongeza pale mambo yanapofanywa vizuri.

"Watumishi walio wengi wakisikia ziara ya kamati basi wanahisi kutumbuliwa hivi ila sasa kwa kazi hii inayofanywa na TFS unaanzaje kutumbua?" Alihoji.

Naye Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, alimweleza Nape kuwa wizara inakusudia kuunda Mamlaka ya Misitu itakayokuwa na jukumu la kusimamia na kuhifadhi misitu yote nchini tofauti na ilivyo sasa.

# Nesi ahukumiwa jela miaka 12 kisa kughushi nyaraka

**Na Beatrice Shayo**

ALIYEJIFANYA Ofisa Muuguzi katika Hospitali ya Vijibweni Kigamboni, Thomas Ongito, amehukumiwa kwenda jela kifungo cha miaka 12 katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke jijini Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Temeke, Pilly Mwakasege, mshtakiwa huyo alishtakiwa kwa makosa manne ikiwamo kughushi nyaraka na kujipatia ajira kama Ofisa Muuguzi.

"Mshtakiwa amepatikana na hatia kwa makosa yote manne na kutakiwa kutumikia jela miaka mitatu kwa kila kosa. Hata hivyo, Mahakama ya Wilaya Temeke imeamuru mshtakiwa atumikie kifungo cha miaka mitatu kwa makosa yote," alisema.

Ilieleza kuwa awali alishtakiwa kwa makosa manne ya kughushi na kutumia nyaraka za kughushi kujipatia ajira kama Clinical Officer, kifungu cha 33, 335, 337 na 342 sheria ya kanuni za adhabu sura Na. 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

**Mshtakiwa alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke Oktoba 9, 2017 na kufunguliwa kesi namba 888/2017 mbele ya Hakimu Mkazi Mwaikambo.**

Mshtakiwa alikuwa Clinical Officer Hospitali ya Vijibweni Kigamboni tangu mwaka 2003, ambapo aliwasilisha cheti cha kidato cha nne kwa mwajiri wake, vile vile akawasilisha cheti cha kidato cha nne kingine katika Chuo cha IMTU.

Mshtakiwa alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke Oktoba 9, 2017 na kufunguliwa kesi namba 888/2017 mbele ya Hakimu Mkazi Mwaikambo.

Wakati huo huo, Takukuru Temeke imemfikisha katika Mahakama ya Wilaya ya Kigamboni mbele ya Hakimu Mkazi, Sundi Fimbo, na kumfungulia kesi namba 04/2019 Mshauri wa Baraza la Ardhi la Kata ya Vijibweni, Fatuma Furahani (42), kwa kosa la kuomba na kupokea hongo ya Sh. 80,000 kutoka kwa Osia Aron, ambaye alikuwa ana shauri katika baraza hilo ili aweze kuwashawishi wajumbe.

Hata hivyo, mshtakiwa alitimiza masharti ya dhamana na yuko nje kwa dhamana hadi Februari 5, 2019 kwa ajili ya usikilizwaji wa awali.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa Januari 17, mwaka huu Takukuru Temeke ilimfikisha katika Mahakama ya Wilaya Temeke mbele ya Hakimu Mkazi, Mariam Mfanga na kufungulia kesi namba 01/2019 aliyekuwa Diwani wa Kata ya Temeke mwaka 2015, Hamis Shaaban Nsombo, kwa kosa la ubadhirifu wa mali ya umma kiasi cha Sh. 8,000,000 alizopewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ndani ya kata kinyume cha sheria ya Takukuru.

Mshtakiwa alitimiza masharti ya dhamana na yuko nje hadi Februari 7, mwaka huu kesi itakapotajwa tena.



Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam akichagua mabegi katika eneo la Mnazi Mmoja jana. Kwa sasa mabegi yana wateja wengi kutokana na Januari kuwa mwezi wa wanafunzi wapya kuanza masomo na wengine kurejea shuleni baada ya kufunguliwa. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# TBS yaondoa sokoni nyaya zisizo viwango

**Na Mwandishi Wetu**

MAOFISA wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wamekamata na kuondoa kwenye soko boksi 13 za nyaya za kuunganisha huduma ya mawasiliano ya 'internet' aina ya Easenet CAT 6 Sem Copper baada ya kupimwa kwenye maabara ya shirika hilo na kuthibitika hazina viwango.

Nyaya hizo zilikuwa zikiuzwa kwenye duka la Sinocai jijini Dar es Salaam. Maofisa wa shirika hilo walifikia uamuzi wa kuhakiki nyaya hizo kwenye maabara za TB baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wateja wa duka hilo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, mkaguzi wa shirika hilo, Hamis Seleleko, alisema wamechukua hatua hizo baada ya kujiridhisha kwamba nyaya hizo hazikidhi matakwa ya viwango.

Alisema nyaya hizo zina urefu wa mita 305 kwa rola moja na zinatumika kuunganisha huduma ya 'internet'. Mbali na kuondoka kwenye soko la nyaya hizo, Seleleko, alisema kuna bidhaa za aina hizo wamezichukua kwenda soko kwa ajili ya kuzifanyia uchunguzi ili kujiridhisha kama zinakidhi viwango.

Alisema kama nyaya hazina viwango vinavyotakiwa kwa ajili ya kupitisha mawasiliano haziwezi kufanya kazi vizuri na badala yake kumsababishia mteja harasa.

Kwa upande wake Ofisa Viwango wa TBS, Miriam George, alisema kiwango kilichotumika katika kupima viwango vya nyaya hizo ni cha Kimataifa IEC 61156.5 . Aliwataka wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa nje ya nchi kuhakikisha wanafuata taratibu na sheria wanapoagiza bidhaa zao ili kuepukana na hasara.

Kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya Viwango vya mwaka 2009, wafanyabiashara wanaoingiza nchini au kuzalisha bidhaa ambazo hazikidhi viwango wanalazimishwa na sheria kuziteketeza kwa gharama zao wenyewe chini ya usimamizi wa mamlaka husika.

Kwa wale wanaoagiza bidhaa kutoka nje pindi zinapobainika kutokidhi viwango, wanakabiliwa na hatari ya kutozwa faini ya asilimia 15 ya thamani ya mzingo, kuzirudisha zilikotoka kwa gharama zao wenyewe au kuteketezwa nchini kwa gharama zao.

Hivi karibuni Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora, Lazaro Msasalaga, alisema wanatambua kuwepo kwa bidhaa za lazima kwenye soko ambazo hazina viwango na kwamba shirika hilo linatarajia kuzindua awamu ya pili ya msako wa kushtukiza wa bidhaa hizo ili kuziondoa kwenye soko.

# Wanakijiji walia huduma za afya

**Na Ibrahim Yassin,** LUDEWA

WAKAZI wa vitongoji vilivyopo kijiji cha Nsele Tarafa ya Mwambao wilayani Ludewa mkoani Njombe, wameiomba serikali kukamilisha ujenzi wa zahanati iliyoanzishwa na aliyekuwa Mbunge wa Ludewa, marehemu Deo Fillikunjombe.

Oscal Mwasyungulu, alisema ukosefu wa zahanati katika kijiji chao, umesababisha kero kubwa zinazosababisha vifo kwa watoto, wajawazito na wazee wanaotembea umbali wa kilometa 30 kufuata huduma za matibabu kwenye kata zingine.

Alisema baada ya uwapo wa vifo hivyo vilivyodumu tangu enzi za utawala wa mkoloni, waliwahi kumwangukia marehemu Fillikunjombe.

Aliongeza kuwa vijiji na kata zote zilizopo Tarafa ya Mwambao vimekuwa na changamoto kubwa ya vituo vya kutolea tiba na wengi wamekuwa wakikodi maboti kwenda Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kwenye Hospitali ya Matema Beach inayomilikiwa na Kanisa Katoliki.

Mariam Mwambeleko, alisema ni mwathirika namba moja baada ya dada zake wawili kujifungulia kwenye mitumbwi wakisafiri kwenda Hospitali ya Matema kupata tiba, lakini watoto walifariki wakiwa njiani.

Alisema ukosefu wa vituo vya kutolea tiba katika tarafa hiyo ni moja ya sababu ya wakazi hao kupoteza maisha, na kwamba waliwahi kutoa kilio kwa marehemu Fillikunjombe ambaye alianza kuijenga zahanati ya kijiji.

Alisema kufariki kwa Fillikunjombe ujenzi umekwama.

Elias Mwakila, Diwani wa kata hiyo, alisema kijiji hicho hakina zahanati, hivyo wananchi wamekuwa wakitembea umbali mrefu kusaka tiba na kwamba kupitia mabaraza ya madiwani amepeleka hoja hiyo ambapo anaamini itafanyiwa kazi.

Sade Deogratias, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, alikiri kijiji hicho kutokuwa na zahanati, lakini mkakati wa halmashauri ni kuhakikisha tarafa yote ya Mwambao vijiji vyote vinajengewa zahanati.

Alisema madiwani wanatakiwa kuhamasisha wananchi kuanzisha ujenzi na wao watunga mkono jitihada za wananchi kupaua majengo hayo na kuweka samani zote za ndani vikiwamo vifaa tiba na dawa itakayoondoa usumbufu kwa wananchi.

# Umeme wa uhakika wavutia uwekezaji Arusha

**Na Joseph Mwendapole,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme nchini (Tanesco), mkoani Arusha, limewaomba wawekezaji kwenda kuwekeza mkoani huko kutokana na kuwa na umeme wa kutosha wa kuendesha viwanda watakavyoanzisha.

Ombi hilo lilitolewa jana mkoani humo na Meneja wa Tanesco Arusha, Mhandisi Herini Mhina, ambaye alisema kwa sasa wanajitosheleza kwa umeme hivyo wawekezaji wanaokuja kuwekeza mkoani humo watakuwa na uhakika wa nishati hiyo.

Alisema wafanyabiashara wanapaswa kuunga mkono sera ya viwanda ya awamu ya tano kwa kwenda kuwekeza kwenye nyanja mbalimbali kwa sababu watakuwa na uhakika wa umeme.

"Kama tulivyosema awali tuna umeme wa kutosha na kwa mkoa tuna megawati 75, lakini uwezo wa kituo chetu ni megawati 120, kwa hivyo unaweza kuona kwamba tuna ziada ya megawati 50," alisema Mhandisi Mhina.

Mhina alisema uwekezaji huo utatoa matokeo chanya kuelekea uchumi wa kati ikizingatiwa hali nzuri ya upatikanaji wa umeme mkoani Arusha ambao ndio mkoa unaoongoza kwenye sekta ya utalii hapa nchini.

"Viwanda vitaleta matokeo mazuri na makubwa kwa sababu kiwanda kimoja kinaweza kikawa ni mahitaji ya wilaya nzima kwa hiyo viwanda vitasaidia sana kutupeleka kwenye uchumi wa kati kwa haraka sana, hivyo tunawashauri wawekezaji waone fursa kuwekeza na waje Arusha," alisema.

Mhandisi Mhina alisema mbali na umeme kuvutia viwanda vikubwa, wafanyabiashara wadogo na wakati wamekuwa wakinufaika na umeme huo wa uhakika, hivyo kuboresha shughuli zao za uzalishaji.

"Hapa Arusha umeme haukatiki katiki na ukitaka ushahidi wa hilo kawaulize wafanyabiashara wenyewe, ukiona umeme umekatika basi tumeukata wenyewe kwa ajili ya kufanya matengenezo sehemu fulani," alisema.

Zakaria Msatu ambaye ni Meneja wa Tanesco Wilaya ya Mirerani alisema viwanda vimeanza kunufaika na umeme wa uhakika wa mkoani Arusha na baadhi ya wawekezaji wameshaanza kuona manufaa ya kuwekeza mkoani humo.

Alitoa mfano wa wanufaika wa umeme wa shirika hilo kuwa ni mwekekezaji wa kiwanda cha kuzalisha Graphite kilichoko Mirerani ambacho kinapata umeme wa uhakika kutoka Tanesco ambao unatosheleza shughuli za uzalishaji kiwandani hapo.

Akizungumza kwa niaba ya mwekezaji wa kiwanda hicho, Meneja Rasilimali Watu Tumaini Ndugi, alilishukuru Shirika la Tanesco kwa kuwahakikishia huduma ya umeme wakati wa uzalishaji hali ambayo imekuwa nguzo kubwa ya kuleta ufanisi kwenye shughuli zake.

# Amchinja mwanawe kisa wivu wa kimapenzi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

NI unyama! Mama mzazi anadaiwa kumchinja mwanawe wa umri wa miezi sita kwa kile kinachodaiwa kuwa wivu wa mapenzi kati yake na mumewe.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Augustino Senga, alimtaja mtuhumiwa huyo kuwa Cesilia Paschal (29), ambaye ni mkulima na mkazi wa mtaa wa Kisimani, Kata ya Endiamtu, Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

Kamanda Senga alisema mtuhumiwa anadaiwa kumchinja kwa kisu shingoni mwanaye, Frola Theophil, mwenye umri wa miezi sita, Januari 20, mwaka huu, majira ya saa 12 jioni.

**Kwa mwezi tulikuwa tunakusanya Sh. milioni 12.3, hivyo tumezikosa japo kisheria kama CCM haturuhusiwi kukusanya mapato ila kwa sasa tumeomba gari ziwe zinapita pale na**

Alisema baada ya kutenda kosa hilo, Cesilia alimeza dawa mbalimbali za hospitali kwa lengo la kujiua.

"Chanzo cha tukio hili ni wivu wa kimapenzi kwa kuwa kabla ya tukio hilo inasemekana alikuta namba ya simu ya mwanamke iliyokuwa inampigia mume wake mara kwa mara, hali ambayo ilisababisha Januari 19 kugombana," alisema.

Alisema baada ya ugomvi mume wake aliondoka na hakurudi nyumbani hadi baada ya kujulishwa tukio hilo la kuchinjwa kwa mwanawe.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Hai kwa uchunguzi zaidi.

Alisema mtuhumiwa baada ya kutenda unyama na kunywa dawa alikimbizwa kituo cha afya cha Mirerani, ambako madaktari walifanikiwa kumtapisha.

Kamanda alisema polisi wanaendelea na uchunguzi na ukikamilika mtuhumiwa atafikishwa mahakamani.

Wakati huohuo, mtu mmoja aliyefahamika kwa jina la Mandera Nada (28) mkazi wa kijiji cha Bagish, wilayani Mbulu, amesombwa na maji na mwili wake kukutwa unaelea mtoni huko Bargish.

Kamanda Senga alisema tukio hilo lilitokea Januari 18, majira ya saa 5:00 asubuhi na mwili wake umehifadhiwa katika hospitali ya wilaya.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Baraza la Biashara la Afrika Mashariki (EABC), Peter Mathuki (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, baada ya mkutano wa kifungua kinywa ulioandaliwa na baraza hilo, kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), na kujadili changamoto za vikwazo vinavyochangia biashara kushuka katika nchi za Afrika Mashariki. Kulia ni Mkurugenzi wa Huduma kwa Wanachama wa TPSF, Louis Accaro na Mkurugenzi wa EABC, Abdulsamad Abdulrahim. **PICHA: JOHN BADI**

# Ashauri serikali kubadili sera ya ajira

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imeshauriwa kubadili sera yake ya ajira ili kuweza kuwaajiri walimu katika nafasi za maofisa watendaji wa kata, vijiji na maendeleo ya jamii ambako kuna uhaba wa watumishi.

Ushauri huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru, Dk. Wilson Mahera, alipokuwa akizungumzia suala la uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi katika shule za halmashauri yake.

Dk. Mahera alisema hayo juzi wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Loata Sanare, kukagua ujenzi wa madarasa ya sekondari kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza

Alisema, shule nyingi zimepokea idadi kubwa ya walimu wa masomo sanaa na biashara isipokuwa ya sayansi.

Alisema walimu hao hawana vipindi vya kufundisha kutokana na wingi wao na kulazimika kukaa.

"Nashauri kuliko walimu hao kukaa bila kufundisha huku wakiendelea kupokea mishahara ni vyema sera ya ajira ingewaruhusu kutumika katika nafasi hizo alizozitaja hapo juu," alisema.

Alisema kwa sasa halmashauri yake ina upungufu mkubwa wa watendaji wa vijiji na kata hali ambayo itailazimu serikali kuajiri, hivyo ni vyema wakawaajiri walimu wenye sifa ambao tayari wako katika ajira badala ya kuajiri wengine wapya.

Alisema baada ya kuziba nafasi hizo za ajira mpya za watendaji hao pamoja na maofisa maendeleo ya jamii kwa kuwachukua walimu, serikali itaweza kuziba nafasi zao kwa kuajiri walimu wapya wa masomo ya sayansi.

Alisema jambo hilo linawezekana kabisa kwa kuwa sifa zinazotakiwa kwa waajiriwa wa nafasi hizo za watendaji na maofisa maendeleo ya jamii ni pamoja na taaluma ya ualimu.

Aliongeza kuwa kiwango cha elimu walicho nacho walimu hao ambayo ni shahada ya kwanza na hata astashahada jambo ambalo litawawezesha kuja na mipango mizuri katika nafasi hizo kwa kushirikiana na walimu wengine wenye sifa kama hizo.

Akijibu ushauri huo, Mwenyekiti Sanare alisema anaunga mkono sera hiyo kufanyiwa marekebisho ili fedha za serikali zinazotumika kulipa mishahara hiyo zitumike kihalali kwa waajiriwa hao kufanya kazi.

Alisema atalifikisha serikalini kupitia vikao vyake vya chama, ili liweze kufanyiwa kazi haraka na kupata watumishi katika nafasi hizo za watendaji na maofisa maendeleo ya jamii ambako kuna uhitaji mkubwa wa watumishi hao.

# Wafugaji wa kisasa walilia soko la maziwa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

KUZOROTA kwa soko la maziwa yatokanayo na mifugo inayofugwa kisasa katika Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, kunaweza kuvunja moyo kwa wafugaji maeneo mbalimbali nchini.

Hayo yalielezwa jana na Mratibu wa Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV), Isack Kitururu, wakati wa mafunzo ya namna bora ya uandaaji wa mpango mkakati wa uboreshaji wa masoko hasa katika uongezaji wa thamani.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Jukwaa la Masoko na Mawasiliano la ABC BROS, kwa ushirikiano na SNV.

**Kutokana na uzalishaji wetu hivi viwanda bado havitoshi... tunahitaji viwanda zaidi viweze kutusaidia kukusanya maziwa yote hayo kwa faida ya walaji...**

Kwa mujibu wa Kitururu, Mkoa wa Kilimanjaro, soko la maziwa lipo na kinachotakiwa ni kuweka mikakati kuandaa bidhaa bora kabla ya kumfikia mlaji.

"Sisi kutokana na warsha tuliyoitoa leo ni dhahiri kuwa ni lazima kuwapo kwa soko la uhakika la kuchukua maziwa yote yanayozalishwa na wakulima kwa kuzingatia ubora, usafi na usalama," alisema Kitururu.

Akifungua warsha hiyo, Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Wilaya hiyo, Elia Machange, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, alisema mpaka sasa wana uwezo wa kuzalisha lita milioni 36 kwa mwaka, licha ya kuwa bado wana viwanda viwili vya usindikaji wa maziwa yao.

Alisema kwa sasa wanashirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali, ili kuhakikisha vyama vya ushirika vya maziwa vinaundwa.

"Kutokana na uzalishaji wetu hivi viwanda bado havitoshi...tunahitaji viwanda zaidi viweze kutusaidia kukusanya maziwa yote hayo kwa faida ya walaji... ingawa kuna mwekezaji ambaye yupo tayari kuwekeza kiwanda chake mkoa wa jirani, ambapo ametuhakikishia kukusanya maziwa yetu yote kutokana na kupata soko Uarabuni, " alisema Dk. Machange.



Muuza mchicha akiwa anaelekea kuwatafuta wateja katika harakati za kujiongezea kipato eneo la Buguruni jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kulipa ada ya umiliki wa visima

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

OFISA wa Maji wa Bonde la Mto Pangani (PBWO), Segule Segule, ametoa rai kwa wananchi wa Mikoa ya Kanda ya Kaskazini kuanza kulipa sehemu ya ada ya umiliki wa visima vya maji, ili wapewe ushauri wa kitaalamu kuhusu matumizi yake.

Alitoa rai hiyo jana, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu operesheni ya Wizara ya Maji kuwatambua wamiliki wa visima vya maji ambao hawajasajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Segule ameeleza kwamba bado kuna changamoto kubwa ya ulipaji wa ada kidogo ya uchimbaji wa visima kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Maji, Namba 11 ya Mwaka 2009 kifungu cha 43.

Alisema kwa sasa wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kuwa na vibali wanapotaka kuchimba visima kwa ajili ya maji ya matumizi ya nyumbani, viwandani au kilimo ili waweze kupata ushauri wa kina kutoka kwa wataalamu wa namna bora ya kuchimba bila kugusa maji taka.

"Tunawaomba wananchi kufika kwenye ofsi zetu kupata wataalamu watakaowawezesha kuchimba visima vyenye ubora kwa kuwa kuna umbali wa visima ambavyo haturuhusu, hivyo ni vyema wakafika kwa ajili ya ushauri," alisema.

Mmoja wa wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, Aneti Samson, alisema hajaona umuhimu wa kuchimba kisima chake halafu akakilipia fedha.

"Kabla ya serikali kutaka tulipe kodi kwa matumizi ya maji yetu tunaochimba kwa gharama zetu basi wangeweka utaratibu maalumu utakaompa mwananchi afueni katika kuchimba hayo maji au wagawe mashine za kuvutia maji," alisema.

Omary Shabani, alisema ulipaji wa kiwango walichopangiwa kingeweza kulipika ikiwa tu elimu ya kutosha ingetolewa kwa wananchi na ushauri hasa maeneo ya vijijini, ili kusaidia mkanganyiko uliopo.

# Wananchi waiangukia serikali iwasaidie bwawa

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

BAADHI ya wakulima wa kijiji cha Kiingia Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wameiangukia serikali na kuomba kuharakisha mradi wa ujenzi wa bwawa la Orumu, ili liwasaidie katika shughuli zao za kilimo cha umwagiliaji.

Mradi huo ulioanza Desemba mwaka 2018 ambao unatarajiwa kukamilika Mei, 2019, utagharimu zaidi ya Sh. milioni 400 ikiwa ni fedha za ndani kutoka Serikali Kuu.

Rafael Kisaka ambaye ni mkulima, alisema ikiwa mradi huo utakamilika kwa wakati utaweza kuwasaidia kuvuna maji ya mvua ili wayatumie kwenye kilimo cha mboga na matunda na kukuza uchumi wa wilaya.

"Mradi huu wa bwawa ikiwa utakamilika kwa wakati utasaidia kukuza pato la wilaya pamoja na kuongeza ajira kwa vijana na wanawake wanaolima na kisha kusubiria mvua zinyeshe," alisema Elisaria Marandu.

Kwa upande wake meneja mradi kutoka Tume ya Umwagiliaji ya Taifa Kanda ya Kilimanjaro, Marthine Mgangaluma, alisema kwa sasa bwawa hilo limejaa matope.

Alisema wanatarajia kujenga tuta kubwa la mita 85 lenye upana wa mita 25 na kina mita 6 litakaloweza kubeba maji lita 58,950.

"Hadi kufikia sasa tumefanya kazi hiyo kwa kipindi cha mwezi mmoja tu na kazi imekamilika kwa asilimia saba hii ni kutokana na changamoto za maji na wingi wa tope lililopo eneo hili tunaendelea kujitahidi ili kuweza kukamilisha kwa muda uliotolewa lengo likiwa ni kuwasaidia wakulima," alisema.

Akizungumza Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu, baada ya kutembelea mradi huo, alisema wao kama wasimamizi wa miradi ya maendeleo wanalazimika kutembelea eneo husika ili kujionea hali halisi.

"Hizi ni fedha za serikili na tunapaswa kuzisimamia ipasavyo katika miradi inayoelekezwa katika halmashauri lengo likiwa ni kuwasaidia wananchi wa hali ya chini kunufaika na serikali yao na kuziba mianya ya rushwa na ufujaji wa mali za serikali," alisema.

Naye Mhandisi Msimamizi kutoka kampuni ya kizalendo ya Shekemu Construction Co.Ltd, Fikirini Gabacholi, aliiambia Nipashe kuwa licha ya kuweka jitihada za kukamilisha mradi huo kwa wakati lakini bado wanakabiliwa na changamoto ya miundombinu ya barabara.

Alisema katika miundombinu iliyopo hairuhusiwi kupitisha magari makubwa yanayopeleka malighafi katika eneo la mradi, hali inayosababisha kutumia magari madogo ambayo pia yanapoteza muda na kusababisha hasara.

Ukurasa 18



**MAMBO YATAJULIKANA 2020 KAMA NAWANIA UBUNGE AU SIVYO**

## MAKALA:

Rais Ramaphosa kuibuka shujaa ama kukiangusha chama ANC?



Ukurasa 14

## KIMATAIFA:



**Ujerumani yaadhimisha miaka 100 tangu kuanzishwa demokrasia**

Ukurasa 20


# siasa

JUMATANO JANUARI 23, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




**'Utanashati' wa kujitoa EU walea ugaidi Ireland Kaskazini, uzalendo Scotland**

Ukurasa 15

# DRC yapuuzia upinzani kutoka nje, yajiandaa kumwapisha Tshisekedi

**Na Michael Eneza**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), imedhihirisha mfumo wake wa kidemokrasia kwa kungoja uamuzi wa Mahakama ya Kikatiba nchini humo kuhusu tangazo la matokeo ya uchaguzi wa rais hapo Desemba 30 ambalo kiongozi wa upinzani Felix Tshisekedi alitangazwa mshindi.

Mgombea wa 'pamoja' wa upinzani, Martin Fayulu, alisema kulikuwa na ujanja katika kujumlisha kura na Kanisa Katoliki lililokuwa na waangalizi wa kura zaidi ya 40,000 kote nchini lilisema linatilia shaka tangazo hilo la aliyeshinda na kuashiria kuwa ni Fayulu aliyepata kura nyingi zaidi.

Uamuzi wa mahakama hiyo

ENDELEA UK 16



Rais Joseph Kabila wa DRC

UCHAMBUZI

Na Mashaka Mgeta

# UCHAGUZI MKUU 2019

## Rais Ramaphosa kuibuka shujaa ama kukiangusha chama ANC?



Rais Cyril Ramaphosa (kulia), akiwa na rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma. **PICHA: MTANDAO**

UCHAGUZI Mkuu wa Afrika Kusini unatarajia kufanyika Mei mwaka huu, upinzani mkubwa ukitarajiwa kutoka kwa vyama vitatu vinavyoshindana kutokana na kuungwa mkono na wananchi, japo kwa viwango tofauti.

Pamoja na hayo, uchaguzi huo unamweka katika wakati mgumu Rais Cyril Ramaphosa, anayekiongoza chama tawala cha African National Congress (ANC), aliyechukua madaraka kutoka kwa Rais aliyejiuzulu, Jacob Zuma.

Akionekana kuwa mwanasiasa anayeweza kuziba nyufa zilizoachwa kupitia kashfa za mtangulizi wake, Zuma, Rais Ramaphosa, anaingia katika uchaguzi huo huku hali ikiwa si shwari sana katika chama chake.

Taarifa za kuporomoka kwa uchumi wa taifa hilo lenye maendeleo makubwa Kusini mwa Afrika na mzozo uliogubika ndani ya chama hicho, ukihusishwa na kugombania madaraka, ni miongoni mwa changamoto zinazomkabili Rais Ramaphosa kupata matokeo mazuri kwenye uchaguzi huo.

Hata hivyo, bado ANC inayosadikiwa kuungwa mkono na asilimia 80 ya raia wa Afrika Kusini, ina nafasi nzuri dhidi ya washindani wake wa karibu, chama cha Democratic Allience (DA) chenye wazungu na waasia wengi na Economic Freedom Fighter (EFF) cha James Malema.

Rais Ramaphosa, aliyetokea katika shirikisho la wafanyakazi na mfanyabiashara mwenye 'ukwasi wa kutupwa' nchini humo, ndiye mwenye mamlaka ya kutangaza tarehe rasmi ya uchaguzi huo.

Kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita wa mwaka 2014, ANC ilishinda kwa asilimia 62, DA ikapata asilimia 22 na EFF kikaambulia asilimia sita.

Lakini kura ya maoni iliyofanyika Oktoba mwaka jana, ilionyesha kuwa ikiwa uchaguzi huo ungefanyika katika kipindi hicho, ushindi wa ANC ungeshuka kufikia asilimia 48 kama ambavyo wa DA ungeshuka hadi asilimia 11 huku EFF ikipanda kutoka asilimia sita hadi 11.

**DAFTARI LA WAPIGA KURA**

Hivi sasa daftari la wapiga kura nchini Afrika Kusini linaonyesha kuwapo watu milioni 26.1 walijioandikisha.

Shirika la Habari la SA News liliripoti kuwa Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi (IEC) nchini humo, Glen Mashinini, anasema Rais Ramaphosa alionyesha dhamira ya kutangaza uchaguzi kufanyika kabla ya mwisho wa Mei, mwaka huu.

"Tume imemhusisha Rais...na kinachofuata ni Rais kutangaza nia ya kufanyika Uchaguzi Mkuu kabla ya mwezi Mei," anasema Mashinini.

Kwa mujibu wa Katiba ya nchi hiyo, kipindi cha uwakilishi wa wabunge katika Bunge la Taifa na mabaraza ya majimbo kitafikia ukomo wake Mei 6, mwaka huu na Uchaguzi Mkuu unapaswa kufanyika ndani ya siku 90 baada ya ukomo huo.

**WAPIGAKURA WAPYA**

Mashinini, anasema uandikishaji majina mapya katika mchakato wa kuboresha daftari la wapigakura ufanyika Januari 26 na 27 mwaka huu.

Anasema kuna vituo 22,932 kwa ajili ya utekelezaji wa mchakato huo, vitakavyofunguliwa kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa 11 jioni na anaamini kwamba angalau wapigakura wapya milioni moja watajiandikisha.

Mashinini anasema mchakato wa maboresho ya daftari la wapigakura, utawafikia pia wafungwa na mahabusu waliopo gerezani nchi nzima kama moja ya haki zao za msingi.

"Kwa maana ya upigajikura, wafungwa wanaruhusiwa kujiandikisha kupigakura kwenye wilaya ambayo gereza alimofungwa lipo,"anasema.

> "Kuna ushahidi wa dhahiri duniani kote unaoonyesha kuwapo uhusiano kati ya ukuaji uchumi na uungwaji mkono kwenye uchaguzi,"

IEC inatarajia kuchapisha na kusambaza atlasi yenye matokeo ya uchaguzi wa manispaa uliofanyika 2016, ikiwa na takwimu kutoka kwenye majimbo, manispaa, kata na vituo vya upigajikura na zinaweza kutumiwa na vyama vya siasa kujitathimini ama kuvitathimini vyama vingine namna walivyofanikiwa katika uchaguzi huo.

Atlasi hiyo inatarajiwa kuwa nyenzo muhimu kuvisaidia vyama vya siasa kupanga na kuboresha mikakati yao ya kampeni kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu ujao.

**CHANGAMOTO KWA RAMAPHOSA NA ANC**

Rais Ramaphosa na chama tawala cha ANC wana kazi kubwa ya kurejesha imani ya raia wa Afrika Kusini, wasioridhishwa na kudidimia kwa uchumi wa taifa hilo.

ANC inayojulikana pia kama 'Chama cha Nelson Mandela', iliingia madarakani kwa mara ya kwanza mwaka 1994, ulipokoma utawala wa makaburu wa Afrika Kusini.

Chama hicho kilipata matokeo mabaya katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa 2016, kisha mabadiliko ya uongozi kutoka kwa Rais 'aliyeachia ngazi' Jacob Zuma kwenda kwa mrithi wake, Ramaphosa mapema mwaka jana.

Chama kikuu cha upinzani cha Democratic Alliance (DA) na kile cha 'watukutu' cha EFF wanatarajia kuongeza ufuasi na kupata matokeo mazuri zaidi katika uchaguzi huo.

Miongoni mwa sababu zinazotegemewa 'kuvibeba' vyama hivyo ni madai ya kushamiri kwa ukosefu wa ajira uliopanda kufikia takribani asilimia 28 na kukosekana kwa usawa unaohusishwa na ubaguzi wa rangi.

Kwenye uchaguzi wa wabunge uliofanyika 2014, kati ya viti 400, ANC ilishinda 249, DA ikapata viti 89 na EFF ikashinda viti 25. Vyama vingine sita vilivyosalia viligawana viti vilivyobaki.

ANC ni chama kikubwa chenye wafuasi wengi weusi (Waafrika) kikikadiriwa kuenea kwa takribani asilimia 80 ya raia wote wa Afrika Kusini.

Hata hivyo, kinakabiliwa na kashfa za rushwa na uongozi dhaifu ukichochewa na kiongozi wa chama hicho aliyejizulu katika nafasi ya Urais, Zuma.

Kwa upande wake, DA inaaminika kuwa na wafuasi wengi weupe (wazungu na waasia). Ni chama kinachohitaji kuungwa mkono na Waafrika Kusini weusi ili kushinda uchaguzi. Pengine ndio maana kiongozi wake, Maimane ni mweusi.

Chama cha EFF chenye misingi iliyojikita katika sera za uchumi na kijamii, miongoni mwa mambo mengine, kinasimamia azma ya kuwapora mali wazungu na waasia wa Afrika Kusini pasipo kuwalipa fidia.

Rais Ramaphosa anaendelea kutafuta muafaka wa kudumu utakaoboresha mamlaka yake ndani ya ANC, baada ya mgogoro mkubwa wa uongozi katika chama hicho.

Jitihada hizo zitafanikiwa ikiwa ANC itavuka matarajio yake katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, hata kama viti vya ubunge itakavyoshinda vitakuwa vichache ikilinganishwa na ilivyokuwa katika uchaguzi wa 2014.

ANC iliwahi kuingiwa hofu ya kushiriki uchaguzi huo kutokana na uchumi wa taifa hilo 'kuvurugika'.

Mkuu wa Kamati Ndogo ya Mageuzi ya Uchumi ya ANC, Enoch Godongwana, akasema kama ilivyo kimataifa, kuporomoka kwa uchumi wa nchi kunaathiri uungwaji mkono katika uchaguzi.

"Kuna ushahidi wa dhahiri duniani kote unaoonyesha kuwapo uhusiano kati ya ukuaji uchumi na uungwaji mkono kwenye uchaguzi," anasema.

Godongwana, anasema wataendelea kuhofia uchaguzi huo ikiwa hapatakuwa na mabadiliko katika 'mtikisiko wa uchumi' hadi uchaguzi huo utakapofanyika.

"Ndio maana tunaitaka serikali iingilie kati,"anasema na kuongeza kwamba hakuna chama kinachoweza kufurahia kuingia katika Uchaguzi Mkuu wakati uchumi wa nchi ukiporomoka.

"Tunapaswa kufanya juhudi zote kuhakikisha kwamba hatuingii kwenye uchaguzi huku uchumi ukiwa unadorora," anasema kiongozi huyo wa ANC.

**TAKWIMU**

Hoja hiyo ilitokana na taarifa iliyotolewa na Taasisi ya Takwimu nchini humo (Stats SA) kwamba pato la ndani lilishuka kwa asilimia 0.7 katika robo ya pili ya mwaka jana.

Hali hiyo ilifuatia ile ya robo ya kwanza iliyokuwa asilimia 2.2, kisha robo mbili mfululizo za kutokuwapo ongezeko, ikahalalisha dhana ya kuporomoka

Inaendelea Uk.17



Waziri Mkuu wa Uingereza, Theresa May. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# 'Utanashati' wa kujitoa EU walea ugaidi Ireland Kaskazini, uzalendo Scotland

**Na Nimi Mweta**

ATHARI za mparaganyiko wa kisiasa unaotokana na kukataliwa kwa mkataba wa kujitoa Uingereza katika Umoja wa Ulaya (EU) zimeanza kuonekana, kwa kupanda joto la kujitenga kwa madola-jimbo yanayounda taifa hilo.

Tukio moja la kufungua macho kuwa hali inaanza kubadilika katika mahusiano ya serikali ya Uingereza na majimbo hayo ni kuanza tena kufufua ugaidi ndani ya kundi la kigaidi la Irish Republican Army ambalo lilifikia muafaka na serikali ya Uingereza miaka saba iliyopita, na makundi ya siasa nchini humo yanaamini mkataba huo hautakuwa hatarini kutokana na vuguvugu jipya la kujitenga. Magaidi wanaona hali inakuwa njema kwao.

Hakuna uwezekano wa usalama kuwa hatarini kwa upande wa Scotland, ambako chama chake cha Scottish National Party kinaunga mkono kubaki katika EU, au sera za chama cha upinzani cha Labour cha kuwa na umoja wa forodha na Umoja wa Ulaya.

Jitihada za wanaharakati wa Scotland za kujitoa kuwa sehemu ya Uingereza ili nchi hiyo iwe taifa huru ambalo ni sehemu ya EU kama Ireland ilivyo ziligonga mwamba kwa mara nyingine katika kura ya maoni mwaka 2014 ambako upande unaotaka Scotland ijitenge ulipata kura asilimia 44.7, na wa kubaki Uingereza asilimia 55.3, kufuta wazo hilo. Tatizo la sasa lilikuja baadaye.

Katika kura ya maoni kuhusu Uingereza kujitoa EU mwaka 2016, majimbo yote 32 ya Scotland yalipiga kura kubaki katika umoja huo, kwa asilimia 68 ya kura zote huku waliotaka Uingereza ijitoe wakipata asilimia 38 tu.

Katika mazingira hayo, suala la kujitoa Uingereza katika EU linaleta majaribu; katika utii wa wanasiasa wa Scotland kwa serikali ya Uingereza, kwani wanaona watapata matatizo makubwa iwapo hatua hiyo itafikiwa.

Hata hivyo, chama hicho hakikuunga mkono pendekezo la chama cha Labour katika kupiga kura ya kutokuwa na imani na serikali ya Theresa May baada ya mkataba aliofikia na EU kukataliwa na Bunge majuzi.

Katika mjadala vurumai unaoendelea kila kukicha katika Bunge la Uingereza, kinachofanyika sasa ni kutafuta mpango mbadala unaokubalika miongoni mwa makundi tofauti ya Bunge (vyama vya siasa) kuhusu nini cha kufanya, licha ya kuwa hapatakuwa na mpango tofauti utakaokubaliwa na EU.

Ina maana kuwa kinachojadiliwa sasa ni jinsi ya kujiandaa kujitoa bila mkataba (hivyo kuwa nchi nyingine tu inayotaka kufanya biashara na EU na hivyo kukutana na vizingiti kila mahali).

Ni mazingira hayo ambayo yanaiogopesha Scotland ambako tabaka la wakulima wanaouza bidhaa tofauti nchi za EU ni sehemu muhimu ya wapiga kura, kama ilivyo kwa Ireland Kaskazini.

Inavyoelekea Waziri Mkuu May anaweza kuacha kutangaza kuanza kutumika kwa sheria ya kujitoa EU ikiwa ndiyo gharama ya kulipa kwa serikali hiyo ili kulinda umoja wa Uingereza dhidi ya chokochoko za kujitenga kwa Ireland Kaskazini, au wapiga kura Scotland kuanza kujifikiria upya ndani ya Uingereza.

Ukisikiliza majadiliano bungeni, unapata picha kuwa suala la kujitoa EU hata bila mkataba uliokubalika ni utanashati wa kisiasa, aina ya kiburi cha wanasiasa wa kihafidhina kilichoko madarakani, lakini suala la kutojitoa bila mkataba halisi ni la kufa na kupona.

Makundi tofauti yanayounga mkono chama cha Labour na hata SNP ya Scotland, kwa vile ni Waingereza na wana kiburi kiasi fulani kuhusu kudhibiti mipaka ya nchi, wanaunga mkono kujitoa EU, kiaina.

> Kinachoonekana ni kuwa, Waziri Mkuu May atakosa nguvu kuacha hali ya sasa iendelee, asiitishe kipengele cha kujitoa EU, kwani atawavuruga wafuasi wa vikundi tofauti.

Ndani ya utanashati huo wa kujitoa ambao ndiyo hoja kuu ya wahafidhina lakini ni hoja ya ziada tu kwa wafuasi wa Labour, ambao zaidi ni makundi ya wafanyakazi na wakulima (siyo maskini, ni wawekezaji mashambani) hitaji la kutojitoa bila mkataba ni kali sana.

Ni kama kiwewe kwao, na hawataki kabisa kusikia kuwa mpango wa kujitoa uendelee bila mkataba unaolinda maslahi hasa ya wakulima (na hata wauzaji wa bidhaa nyingi tu za viwandani ambazo zinalinda ajira za mamilioni ya wafanyakazi).

Waziri Mkuu May ambaye ni mhafidhina naye anatanguliza utanashati wa kuheshimu kura ya maoni ya 2016 iliyofikia uamuzi wa kujitoa, kuwa kura hiyo ni mwisho wa suala hilo haiwezi kurudiwa. Ila ameshindwa kupata mkataba wa kuitekeleza kura hiyo ya maoni.

Pamoja na mkataba wake na EU kushindwa kwa kura nyingi bungeni, 432 dhidi ya 202 zilizoounga mkono, Waziri Mkuu May bado alishinda kura ya kutokuwa na imani na serikali yake, wakati wanaounga mkono wakiwa ni pamoja na zaidi ya wabunge 100 walioukataa mkataba na EU.

Awali, May alishinda kura ya maoni ya wabunge wa Conservative wakiongozwa na wahafidhina 'siasa kali; walikuwa wanapinga uelekeo wa kufikia mkataba na EU waliouona ni mbovu, kwani Uingereza haitoki huko haraka.

Ndiyo wanaofurahia, chini kwa chini, kujitoa bila mkataba wakitazamia kuwa itachukua muda mfupi kuzoea hali hiyo, kwani watalaamu wa mrengo wa kulia wanasema hapatakuwa na tatizo la maana endapo Uingereza itatoka bila mkataba halisi.

Kwa vile haiwezekani May akafikia mpango mbadala wa jinsi ya kujitoa EU ambao unakubaliwa na Bunge la Uingereza halafu na EU yenyewe, ina maana atahitaji 'kusuka au kunyoa' kuhusu suala hilo, na hapo ndipo tishio la ugaidi linapokuwa na umuhimu, au kujitoa Scotland katika Uingereza.

Ingekuwa hakuna tatizo la hayo majimbo-dola mawili, iwe ni England yenyewe tu inayoamua, ingekuwa rahisi May kufuata hisia za utanashati wa kuheshimu matokeo ya kura ya maoni Juni 2016, kuwa lazima yatekelezwe ili kuheshimu demokrasia, n.k.

Lakini iwapo tishio litaonekana kuwa ni la kweli, basi May anaweza akaacha kila kitu kiendelee kana kwamba hapakuwa na kura ya maoni, halafu liwe ni tatizo la uongozi wake katika chama hafidhina cha Conservative.

Kuna uwezekano pia wa kupata matatizo kiasi fulani bungeni iwapo May atafikia uamuzi wa kutoendelea na mpango wa kujitoa, pamoja na kuwa hisia zake yeye binafsi zinazochomoza katika kujibu maswali bungeni ni kuchagua kati ya kujitoa EU kwa mkataba alioufikia kama ulivyo, au kujitoa bila mkataba.

Suala la kutojitoa, kufanya kura ya maoni kwa mara ya pili, ni masuala anayoyakataa lakini mizania ya kisiasa inaonyesha kuwa hofu ya kujitoa bila mkataba ni kubwa zaidi miongoni mwa matabaka ya wafanyakazi na wakulima nchini humo (inavyodhihirishwa na kinachosemwa na chama cha Labour pamoja na vyama au vikundi vya Ireland Kaskazini na Scotland).

Halafu pia kuna suala la tafsiri ya dhana ya ujasiri katika suala hilo, kama ni kujitoa bila mkataba halafu yaanze mazungumzo na washika dau tofauti kwa mikataba ya biashara, au kuacha hali ya sasa iendelee.

Kinachoonekana ni kuwa, Waziri Mkuu May atakosa nguvu kuacha hali ya sasa iendelee, asiitishe kipengele cha kujitoa EU, kwani atawavuruga wafuasi wa vikundi tofauti.

Inavyoelekea atadiriki kuingia katika hali ya kujitoa Machi 19 kama inavyotazamiwa, kwani ataungwa mkono na sehemu isiyo ndogo ya wabunge wake, na hao wanaotingisha kiberiti wanaweza wasiweze kufanya madhara makubwa. Ni jambo analoweza kulishughulikia.

MAKALA

# DRC yapuuzia upinzani kutoka nje, yajiandaa kumwapisha Tshisekedi

Inatoka Uk.13

umepuuza hoja hizo na kuthibitisha ushindi huo.

Taarifa za alasiri Januari 21 zilisema kuwa utawala wa Rais Joseph Kabila, anayeondoka madarakani umekubali kusogeza mbele kwa siku mbili kuapishwa kwa Tshisekedi, kufanyike kesho Alhamisi badala ya Jumanne kama ilivyokuwa imepangwa.

Bado haijaeleweka ni vigezo gani hasa vilivyotumika na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (CENI) kwa upande mmoja halafu na Kanisa kwa upande wa pili kufikia tamati tofauti kuhusu aliyeshinda uchaguzi wa rais, lakini inaelekea suala hilo halitakuwa gumu kupita kiasi.

Suala ni kuwa, wengi wanaona tatizo ni kati ya mgombea wa utawala wa Kabila, Emmanuel Shadary na upinzani, na siyo muhimu kupita kiasi ni yupi kati ya wagombea wawili wa upinzani aliyepata kura nyingi, kwani ushahidi ni rahisi kukusanywa, kutawanywa.

Kwa upande mmoja hatua za utawala wa Kabila katika kipindi cha kupiga na kuhesabu kura, za kufunga mawasiliano ya mtandao na kituo cha redio ya kimataifa ya Ufaransa, kunaweza kuwa kumesaidia kupunguza hamasa kuhusu matokeo ya uchaguzi.

Suala ni kuwa wapiga kura walikuwa wanangoja kama mgombea wa utawala ndiye atakayetangazwa mshindi, hali ambayo kwa jumla ingeweza kusababisha vurugu, ila aliposhinda mpinzani hali imekuwa tulivu, na baada ya tangazo la Mahakama ya Katiba huduma ya mtandao, redio ya RFI zikarudishwa.

Itachukua muda kwa makundi ya wanaharakati kulinganisha walichojumlisha na walichofikia.

Kutokana na kuyakinishwa kwa ushindi wa Tshisekedi na Mahakama hiyo, rai ya kuundwa kwa serikali ya umoja wa kitaifa au ya vyama vyote kwa pamoja iliyotolewa na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) halafu pia na Umoja wa Afrika (AU) iliwekwa pembeni na haikuwa inasikika zaidi.

Moja ya sababu za hali hiyo ni kuwa hapakuwa na vurugu za wafuasi wa Fayulu kutokana na suala hilo, hali inayoashiria kwamba kuna uelewano kati ya wafuasi wa wagombea hao wawili wa upinzani, licha ya msuguano wa kina, nani anafaa kuwa mgombea kati yao.

Inatokana na hali ya kampeni kuwa dhidi ya mgombea wa utawala na siyo mgombea wa upinzani.

Umoja wa Afrika ulifuta kupeleka ujumbe DRC baada ya uamuzi wa Mahakama, huku wataalamu wakisema umoja huo hauna lolote unaloweza kufanya, na kuwa msukumo wowote kuhusu suala hilo itabidi utokane na wananchi wenyewe, yaani kwa maandamano.

Hapakuwa na mazingira yaliyoonyesha wazi kujijenga, sababu mojawapo ikiwa ni kutokuwepo ushahidi wa wazi nani aliyeshinda, nje ya Tume ilichotangaza na shaka iliyotolewa na Kanisa Katoliki.

Tofauti kati ya tangazo na hisia za Kanisa ndiyo zinaanza kusambaa baada ya mtandao kufunguliwa tena, hivyo itategemea serikali inayoingia madarakani itachukua gia gani kuhusu suala hilo.

> CRG inasema kuwa hapakuwa na uwezekano wowote kuwa Tshisekedi angepata asilimia 38 ya kura katika uchaguzi huru na haki, kwani sana sana angeishia asilimia 21.3 hadi asilimia 25 na siyo zaidi ya hapo.



Majaji wa Mahakama ya Katiba nchini DRC. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Mgombea anayedai kuibiwa kura za urais, Martin Fayulu.

Jukwaa moja linaloshughulikia kuzuia machafuko barani Afrika, lilisema kuwa, matokeo yaliyotangazwa yanaweka mbegu za mifarakano mbele ya safari.

Idadi ya vyombo vya habari barani Ulaya inaongezeka, ikisisitiza kuwa data (takwimu) za uchaguzi (kupiga kura) zilizopatikana wakati wa kuhesabu kura zilionyesha kwa njia isiyopingika kuwa Fayulu alishinda uchaguzi huo.

Jarida la mtandao la Business Live la Afrika Kusini likaandika kuwa, takwimu zinaonyesha udanganyifu mkubwa katika badiliko la kwanza la utawala tangu Kabila achukue urais karibu miaka 18 iliyopita.

Hapakuwa na utetezi huru wa kuainisha ushindi wa Tshisekedi.

Jarida la 'African Arguments' la mtandao pia lilishangazwa na tangazo la ushindi wa Tshisekedi, kwani mlinganisho wa matokeo kwa majimbo ulionyesha kuwa Shadary alikuwa na uwezo wa kushinda jimbo la Maniema (Manyema) wakati Tshisekedi angeweza kushinda Kivu ya Kusini, Kasai Mashariki na Kasai Magharibi, na mengine yote yaliegemea upande wa Fayulu.



Rais Mteule wa DRC, Felix Tshesekedi.

Yaliyobaki ni majimbo ya Bandundu, Congo Bondeni, Katanga, Kinshasa, Kivu ya Kaskazini na jimbo la Mashariki, hali inayoashiria kuwa, licha ya kura kutopigwa maeneo ya Mashariki ya nchi hiyo kutokana na ugonjwa wa Ebola halafu eneo jingine kwa mapigano ya kiraia (uasi) bado ushindi wa Tshisekedi haupimiki kwa urahisi kwa takwimu zilizopo. Inadhaniwa ni ujanja ujanja tu.

Hali ya kipindi cha kupiga kura ilionyesha wazi kuwa mamlaka za kusimamia uchaguzi nchini humo hasa zilikuwa zinalenga kampeni ya Fayulu kuizuia na kuikwamisha, kwa mujibu wa taarifa hizo.

Majukwaa ya kitaaluma kama Crisis Response Group (CRG) tayari yalikuwa nchini humo na kuandaa taarifa za awali kuhusu kilichojiri, na mjadala kuanza kuhusu usahihi wa takwimu za CENI.

Baadhi ya watalaamu wanaounga mkono takwimu zilizotolewa na CENI walisema kuwa matazamio ya ushindi wa Fayulu yalitokana na kutotilia maanani wapiga kura vijijini, lakini CRG inakanusha madai hayo.

Inasema kura za maoni na vielelezo vilivyotumika vinaonyesha kuwa asilimia 41 ya raia wa DRC miongoni mwao ni wakazi wa mijini, wakati takwimu za Benki ya Dunia (WB) zinaonyesha kuwa ukaaji wa mijini nchini Congo umefikia asilimia 43, hivyo inaelekea wakazi wa vijijini walipendelewa.

CRG inasema kuwa hapakuwa na uwezekano wowote kuwa Tshisekedi angepata asilimia 38 ya kura katika uchaguzi huru na haki, kwani sana sana angeishia asilimia 21.3 hadi asilimia 25 na siyo zaidi ya hapo.

Wanasema hata angeongezwa swahiba wake Kamerhe ambaye walikampeni pamoja, bado hakuna uwezekano wa kufikia asilimia 38 ya kura bila vyombo vya kusimamia kura, kuhesabu na kutangaza kufuata mpangilio tofauti ulioamuliwa na wenye madaraka.

Takwimu zilizotumiwa na CRG zilioanishwa na kundi la kitaaluma la BERCI nchini DRC halafu na taasisi ya kuandaa kura za maoni ya IPSOS nchini Ufaransa, hazipingani kwa yale wanayoshuhudia kuhusu mwelekeo wa kupiga kura ulivyokuwa DRC, kinyume na tangazo la matokeo.




Kiongozi wa chama cha Economic Freedom Fighter (EFF), James Malema. **PICHA: MTANDAO**

## Rais Ramaphosa kuibuka shujaa

Inatoka Uk.14

kwa uchumi wa nchi hiyo.

ANC iliyoyumba katika kipindi kifupi cha kabla ya kuondoka kwa Zuma, ilipoteza uungwaji mkono katika uchaguzi wa 2016, kiasi cha kushindwa katika manispaa za Tshwane, Johannesburg na Nelson Mandela Bay iliyozishikilia tangu mwaka 1994.

Hivyo, chama hicho tawala kinajaribu kurejesha taswira na hadhi yake kupitia utendaji kazi wa Rais Ramaphosa kwa chama na nchi.

Lakini historia inaweza 'kuihukumu' ANC kutokana na mapokeo kuwa vyama vikubwa vya siasa vinaanguka kutokana na kugombania madaraka, kushamiri kwa rushwa, uongozi dhaifu na mafarakano kama inavyodaiwa kuwamo ndani ya chama hicho.

Kama ufanisi wa ANC utakuwa chini ya matarajio yake, ni dhahiri kwamba utamdhoofisha Rais Ramaphosa na huenda akang'olewa.

**DA YAPASWA KUTANUA WIGO**

Kwa upande wake, ili kuwa chama thabiti kwa ajili ya kuunda serikali, DA itabidi kutanua wigo wa ngome ya wapigakura inayowategemea zaidi kutoka makundi ya kijamii (wazungu na waasia) wanaokadiriwa kuwa asilimia 20 tu ya raia wote.

Chama hiki kinaamini kwamba siku ya kufanyika uchaguzi huo ni muhimu sana katika maisha ya raia wa Afrika Kusini.

Katika mkutano wake wa uchaguzi wa mwaka jana ambao haukuwaibua 'viongozi wapya', hoja ya kuwapo ajenda ya kisiasa kwa wakati ujao iliibua mjadala mkubwa, ikiakisi masuala kama mageuzi ya sera ya ardhi na ushiriki wa makundi ya kijamii katika nafasi za uongozi.

Pia ilijadiliwa namna bora ya kujenga taswira ya DA kuelekea uchaguzi wa mwaka huu.

Kiongozi aliyepita bila kupingwa, Mmusi Maimane akasema, "DA lazima iwe imara na isigawanywe kwa msingi ya rangi."

**EFF NA MAGEUZI YA SERA**

Mbali na kupata nafasi nyingi katika vyombo vya habari kutokana na uwasilishaji ujumbe kwa jamii, chama cha EFF bado kimebaki kuwa 'kichanga.'

Vinginevyo, kama DA, EFF na vyama vingine vidogo vitaunganisha nguvu zao, na ikiwa ANC itapata matokeo yaliyo chini ya asilimia 50 basi uundwaji wa serikali ya muungano wa vyama ni jambo ambalo linaweza kutokea.

Hata hivyo, kama ilivyo kwingineko katika chaguzi za kidemokrasia, kuwapo madarakani kunatoa faida kwa mgombea na chama tawala na ANC inanufaika kwa kuwa na wafuasi wengi weusi.

Tangu kuondoka kwa Zuma madarakani, EFF imerejea katika masuala ya ardhi na kuilazimisha ANC kurekebisha mbinu zake katika mageuzi katika sekta hiyo. Hivyo ndivyo inavyotarajiwa kuingia katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

**PROFESA**

Mcebisi Ndletyana, Profesa Mwandamizi wa Siasa katika Chuo Kikuu cha Johannesburg, anasema nafasi ya EFF 'kutawala' masuala katika uchaguzi wa mwaka huu ni jambo lililo wazi.

Anasema lengo kubwa tangu kuanzishwa kwake 2013, EFF ililenga zaidi 'ANC ya Zuma' na kuongeza, "sasa ni ANC ya Rais Ramaphosa, inaweza kuwawia vigumu."

Profesa Ndletyana, anasema EFF ilijipambanua kwa utetezi wa makundi ya kijamii yaliyopo pembezoni na wasiokuwa na ajira, wakifananishwa na wapiganaji wanaopata maagizo kutoka kwa wenye hasira na wanaojihisi hawanufaiki kwa namna yoyote na rasilimali za umma, hivyo wanapambana na mfumo.

**MCHAMBUZI**

Mchambuzi wa siasa nchini humo, Ralph Mathekga, anakubali hoja ya mkakati wa EFF kuharibu mfumo na kutafuta kuungwa mkono.

Anaamini kwamba uchaguzi wa mwaka huu, kunaweza kutokea mabadiliko ya sera ya uzawa kwa EFF.

"Tutaona kama ndivyo ama sivyo kwa wapigakura kuwaunga mkono ama kuwakataa, EFF wataamua ama waendelee nayo ama waiache," anasema.

Hata hivyo, Mathekga anatarajia EFF itaongeza kiwango cha kuungwa mkono kwa takribani asilimia 10 ya wapiga kura.

"Hatuoni kama EFF itaongeza mara dufu kiasi cha kuungwa mkono kwa asilimia 16 ama kwenda hadi asilimia 20, lakini kama asilimia 10 hivi inawezekana," anasema.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia 0754691540**

# Mzozo Burundi, Rwanda udhibitiwe kuiokoa EAC

Na Mwandishi Wetu

MSHIKAMANO kati ya mataifa yanayounda ukanda kama ilivyo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ni jambo lenye maana pana katika ustawi na uendelevu wake.

Mafarakano kati ya wanaounda ushirikiano wa kikanda hayana tija na kwa sehemu kubwa yamekuwa miongoni mwa vyanzo vya kuvunjika kwa ushirikiano ama jumuiya husika.

Lakini katikati ya hali hiyo, jumuiya za kikanda zina umuhimu mkubwa wa kuwaunganisha watu wa maeneo husika katika nyanja za uchumi, siasa, kijamii, miongoni mwa mengine mengi.

Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika mwaka 1977 kabla ya kuibuliwa tena ikiwa na nchi wanachama tatu na zimefikia tano sasa, inatikiswa, inayumba na mara kadhaa inaonekana kupotea njia. Lakini lazima isimame.

Mzozo unaokolea hivi sasa kati ya Burundi na Rwanda, nchi zenye eneo dogo ndani ya EAC, si tu kwamba zinayaweka mataifa hayo katika uhusiano duni, lakini pia unaathiri utendaji na utekelezaji wa masuala yanayohusu jumuiya hiyo.

Taarifa iliyotangazwa na Shirika la Utangazaji la DW la Ujerumani inaeleza kuwa, mzozo wa kidiplomasia kati ya mataifa hayo unahusu tuhuma za Burundi kwamba Rwanda inavisaidia vikundi vya uasi kwenye ardhi yake.

Msemaji wa chama tawala nchini Burundi cha CNDD/FDD, Gerase Daniel Ndabirabe, akakaririwa kupitia redio ya taifa akimshutumu vikali Rais wa Rwanda, Paul Kagame kuwa ni chanzo cha matatizo ya Burundi.

Tuhuma hizo na zinazofanana na hizo si ngeni kusikika kila unapotokea mzozo wa kidiplomasia kati ya nchi wanachama wa EAC kama ilivyo kwa ukanda mwingine ukiwamo wa Maziwa Makuu.

Hata Rwanda yenyewe imewahi kwa nyakati tofauti, kuzielekeza shutuma zake dhidi ya Burundi kama ilivyo kwa mataifa mengine kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Uganda, zikihusishwa na vikundi vya waasi.

Mwendelezo wa kadhia kama hizo umewahi kuushawishi Umoja wa Mataifa (UN) kufanya uchunguzi na kuchapisha ripoti iliyoonyesha kwamba makundi yenye silaha yanayopambana dhidi ya serikali ya Rwanda yanapata msaada kutoka Burundi na Uganda.

Baada ya taarifa hiyo, serikali ya Rwanda inayoongozwa na Rais Kagame ikasema haitavumilia uchokozi huo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda ambaye pia ni Msemaji wa Serikali, Dk Richard Sezibera, akasema kundi lenye silaha la FDLR linahusika na 'chokochoko' za nchini humo, na pasipo kuzitaja Burundi na Uganda, akasisitiza kwamba wanalifuatilia tatizo hilo kwa namna ya kipekee.

FDLR ndiyo inayoshutumiwa kuhusika katika mauaji ya Rwanda ya mwaka 1994 na kwamba inaendesha harakati zake Mashariki mwa DRC.

Pia kikundi kingine ni RNC cha Kayumba Nyamwasa aliyewahi kuwa mkuu wa majeshi ya Rwanda akiwa sasa uhamishoni nchini Afrika Kusini, ambalo kama ilivyo FDLR, Dk. Sezibera anasema yanapata misaada ya hali na mali kutoka nchi mbili za kanda ya Maziwa Makuu.

Lakini kwa upande wake, Burundi inadai kuwa kikosi cha majini cha Rwanda kinahusika na utekaji wa wavuvi wanne wa Burundi katika Ziwa Rweru lililopo jimbo la Kirundo.



Rais Pierre Nkurunziza wa Burundi (kushoto) na Rais Paul Kagame wa Rwanda.. **PICHA: MTANDAO**

> Rais Nkurunziza aliongeza, "Burundi haina nia ovu, bali Rwanda ina nia ovu na hilo tutaendelea kulisemea."

Taarifa iliyoandikwa hivi karibuni kwenye mtandao wa twitter ya Wizara ya Ulinzi ya Burundi ilieleza, "....tukio hilo lilitokea saa 5 usiku kwa saa za Burundi na wakati huo huo kikosi cha jeshi la majini la Rwanda kikachukua vifaa vya uvuvi vya wavuvi wa Burundi na kuondoka navyo."

Tukio hilo linaripotiwa wakati ambapo hali ya mzozo kati ya mataifa unazidi kukua na kuathiri uhusiano wao hasa kidiplomasia kiasi kwamba Rais wa Burundi, Pierre Nkurunziza, akaandika barua kwa Mwenyekiti wa EAC, Yoweri Museveni, akiomba kuitishwa kwa mkutano wa dharura wa wakuu wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo ili kusaidia kupatikana kwa suluhu ya mzozo huo.

Barua hiyo ya Rais Nkurunziza iliyoandikwa Desemba 4, mwaka jana, ikaishutumu Rwanda kuandaa na kusimamia mapinduzi ya kijeshi yaliyoshindikana mwaka 2015.

"Rwanda ni nchi pekee katika ukanda wetu (EAC) iliyo msingi wa kuzorota kwa utulivu nchini kwangu na hivyo simuoni kama ni mshirika wetu isipokuwa adui," alieleza Rais Nkurunziza.

Hata hivyo, serikali ya Rais Kagame imekuwa ikikanusha shutuma hizo mara kwa mara, ikiiasa Burundi kutozitupia lawama nchi majirani zake kwa matatizo ya ndani ya nchi hiyo.

Septemba mwaka jana, polisi wa Burundi walisema 'majangili yasiyofahamika' kutoka Rwanda yalimuua kijana wa Kirundi, Ngendakumana Daniel (27) na mkewe Nikiza Elizabeth katika jimbo la Kayanza lililopo Kaskazini mwa nchi hiyo inapopakana na Rwanda.

Mapema Julai mwaka jana, serikali ya Rwanda nayo ilisema majangili yenye silaha kutoka msitu wa Nyungwe uliopo mpakani na Burundi, yaliwapiga risasi watu watano na kuwaua wawili miongoni katika kijiji kimoja Kusini mwa nchi hiyo.

Kwa namna ya pekee, kudhoofika kwa uhusiano wa Burundi na Rwanda kulishamiri zaidi tangu 2015, wakati Burundi ilipoituhumu Rwanda kutoa mafunzo kwa wakimbizi ili waipindue serikali ya Rais Nkurunziza.

Nayo Rwanda ikaituhumu Burundi kwa kuwatunza waasi wa FDLR wanaoshukiwa kwa mauaji ya halaiki ya mwaka 1994, walengwa wakiwa ni watusi na wahutu wenye msimamo wa kati.

Akizungumzia maombi yake kwa EAC, Rais Nkurunziza alizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake, jimbo la Ngozi, akielezea msimamo wa tuhuma dhidi ya Rwanda.

"Tunaitaka EAC iingilie kati masuala haya yanayohusu kufadhili vikundi vyenye silaha ... watu wanauawa na haiwezi kuchukuliwa kuwa jambo dogo," akasema Rais Nkurunziza.

Rais Nkurunziza aliongeza, "Burundi haina nia ovu, bali Rwanda ina nia ovu na hilo tutaendelea kulisemea."

Kwa Rais Kagame, anaamini kwamba shutuma dhidi yake ni 'uchokozi' unaofanywa na Burundi.

Waziri wa Mambo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wa Rwanda, Olivier Nduhungirehe akapuuzia rai ya Burundi kwa EAC kwamba inalenga kutumia mizozo yake ya kisiasa ndani kupindisha mwelekeo wa jumuiya hiyo kwa wanachama wake.

Kwa hali hiyo, ni dhahiri kwamba EAC inapaswa si tu kuzungumzia mzozo huo, bali kuchukua hatua zitakazowezesha kuondoa vyanzo vya mfarakano unaotishia uhai wa jumuiya hiyo.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu namba +255 754 691540**



Felix Mkosamali akihutubia wananchi wa jimbo lake la Muhambwe, enzi za ubunge wake. **PICHA: MTANDAO**

# MKOSAMALI:

## Mambo yatajulikana 2020 kama nawania ubunge au sivyo

**Na Sabato Kasika**

FELIX Mkosamali ni miongoni mwa wanasiasa walioukwaa ubunge wakiwa vijana wenye umri mdogo.

Katika mlolongo huo wamo pia akina John Mnyika wakati huo akiwa jimbo la Ubungo na sasa yuko Kibamba, mkoani Dar es Salaam kupitia Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Wabunge wengine vijana ni Zitto Kabwe, aliyekuwa kijana zaidi katika uchaguzi wa mwaka 2005 jimbo la Kigoma Kaskazini wakati huo akiwa Chadema, Vincent Nyerere (Chadema) Musoma Mjini na David Kafulila wa NCCR-Magezi aliyeshinda jimbo la Kasulu Kaskazini mwaka 2010.

Nikirejea kwa Mkosamali, ni kwamba alikuwa ni miongoni mwa wabunge vijana machachari waliokuwa na michango na hoja mbalimbali zilizosisimua vikao vya Bunge la 10, lakini kwa sasa hasikiki kwenye siasa za nchi hii.

Mwanasiasa huyu kijana alikuwa ni mbunge wa jimbo la Muhambwe mkoani Kigoma kupitia chama Cha NCCR-Mageuzi, kuanzia mwaka 2010, lakini katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 hakufanikiwa kutetea nafasi hiyo.

Tangu wakati huo amekuwa kimya, ambapo katika mahojiano na gazeti hili anasema wakati mwingine mtu anaweza kuwa kimya kwa ajili ya kujifunza au mtu anapaswa kuwa kimya kutazama wengine, lakini hajaacha siasa.

Pamoja na kuwa na umri mdogo, inawezekana watu walidhani kwamba ni mpole na mkimya, lakini alikuwa na uwezo wa kutumia sauti yake nzito kujenga hoja nzito bila ya uoga wowote mbele ya Bunge na tena kwa kujiamini.

Wapo watu waliovutiwa na michango yake bungeni na kutamani kumuona kila mara akichangia, lakini sasa hawaipati tena, kwasababu siyo mbunge.

Katika maswali aliyoulizwa na gazeti hili, mwanasiasa huyo amezungumza mambo mengi ikiwamo hali halisi ya siasa nchini.

Soma mahojiano ya Nipashe na mwanasiasa huyu kijana:

**SWALI: Nini kilikuvutia hadi ukaingia katika siasa?**

**JIBU:** Sababu kubwa ni kwamba ninapenda siasa, ndio maana nikaingia huko na nilianza siasa nikiwa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino (SAUT), Mwanza mwaka 2010. Niliwania ubunge na kushinda nikiwa bado mwanafunzi na nilihitimu masomo yangu ya chuo mwaka 2011.

**SWALI: Ilikuaje ulipoingia bungeni kwa mara ya kwanza na pia rafiki yako alikuwa nani?**

**JIBU:** Nilichukulia kama hali ya kawaida tu ingawa wengine walinichukulia tofauti, wapo walionipenda pia. Kuhusu rafiki, ni kwamba wabunge wote walikuwa rafiki zangu na tulifanya kazi vizuri kwa ajili ya maendeleo ya taifa hili bila kujali kwamba wao ni wakubwa na mimi ni mdogo... cha msingi ni hoja zinazogusa maendeleo ya Watanzania.

**SWALI: Kwa uzoefu wako kuna tatizo gani katika chama chako ambacho zamani kilikuwa na nguvu kubwa lakini sasa hazipo? Pia nguvu ya upinzani ni ipi na udhaifu wake ni upi?**

**JIBU:** Kwanza kabisa mimi si kiongozi wa chama bali ninashauri mambo ya kisheria, hivyo suala la kushuka kwa chama waulizwe wao. Kuhusu upinzani ni kwamba una nguvu kubwa ndio maana unabanwa na vyombo vya dola. Lakini pia tatizo liko katika suala la kushindwa kujenga umoja kutokana na ubinafsi wa baadhi ya watu.

**SWALI: Ni mwanasiasa gani hapa nchini unavutiwa naye?**

**JIBU:** Wanasiasa wa Tanzania ambao wamewahi kuongoza serikali wana mtazamo wa CCM, hivyo siwezi kuvutiwa na yeyote... ninapenda wanasiasa wasioyumbayumba, wasiotanguliza njaa na kufikiri kwa kutumia tumbo na sipendi wanasiasa wanaojipendekeza. Binafsi siwezi kuhamia CCM. Labda nikukumbushe kuwa kuna wakati watu waliwahi kuulisha umma 'matango pori' eti nimehama kutoka NCCR- Mageuzi... huo ulikuwa uongo mtupu. Ninajua ni kwanini niko upinzani. Ninaamini katika upinzani imara, ninaamini katika nchi kuwa na katiba mpya, ninaamini katika haki za binadamu.

**SWALI: Unaionaje Tanzania bila Mwalimu Julius Nyerere, Baba wa Taifa...nani anafuata nyayo zake?**

**JIBU:** Tanzania inakosa kitu kikubwa sana kwa kutokuwepo kwa Baba wa Taifa hili Mwalimu Nyerere. Yeye alipenda ukweli, alikuwa wa kawaida na alipenda kujisahihisha na kujifunza. Kwa hilo swali lingine sina jibu sahihi.

**SWALI: Kwa sasa wewe si mbunge, unafanya shughuli gani? Je, una mpango wa kuwania ubunge mwaka 2020?**

**JIBU:** Mimi ni mkuu wa Idara ya Sheria wa Chama cha NCCR-Mageuzi na pia wakili wa kujitegemea. Hivyo niko kwenye siasa kama kawaida ingawa sisikiki sana kama nilivyokuwa mbunge, kwani watu wengi walikuwa wakiniona katika mijadala mbalimbali bungeni. Kwa upande wa ubunge ni kwamba wakati ukifika kila kitu kitakuwa wazi ninagombea au sigombei.

**SWALI: Kwa sasa kuna sakata la CAG na Spika Job Ndugai, una maoni gani?**

**JIBU:** CAG anajua anachokifanya na hakuna wa kumbabaisha... anaweza kufanya kazi nchi yoyote, hivyo Spika anapaswa kujua kwamba kwa sasa kuna ongezeko kubwa la wasomi hapa nchini kuliko ilivyokuwa siku za nyuma.

MAKALA



Berlin barabara ya Alexanderplatz mnamo mwaka 1919..**PICHA: MTANDAO**

# Ujerumani yaadhimisha miaka 100 tangu kuanzishwa demokrasia

WAKATI mataifa mbalimbali duniani yakitamani mfumo mzuri wa kidemokrasia katika mustakabali wa nchi zao, wengine wanafurahia mfumo huo uliodumu kwa miaka mingi, ikiwamo Ujerumani.

Mwishoni mwa wiki, Januari 19, 2019, nchi ya Ujerumani iliadhimisha mwaka wa 100 tangu kuanzishwa demokrasia baada ya bunge kupitisha katiba ya kisasa katika mji wa Mashariki wa Weimar mnamo mwaka 1919.

Wajerumani walipiga kura hata katika enzi ya ufalme, lakini ukweli ni kwamba siyo wote waliokuwa na haki hiyo. Baada ya utawala wa kifalme kuangushwa, Bunge ndilo lililokuwa mhimili wa mamlaka na lilipitisha katiba ya kisasa lakini alikuwapo adui mkubwa wakati huo, Adolf Hitler.

"Kila kitu ni kwa ajili ya umma na kitafanywa na umma". Hayo ni maneno aliyotamka kiongozi wa chama cha Demokratik, SPD, Bw. Philpp Sheidemann kutokea kwenye Roshani ya Bunge mnamo mwaka 1918.

Bw. Scheidemann aliitangaza Jamhuri iliyokuwa ya muda siku hiyo, lakini wananchi waliruhusiwa kupiga kura miezi miwili baadae yaani siku kama ya leo ( 19 Januari) miaka 100 iliyopita.

> “ Kutokana na chama cha kikomunisiti kujiweka kando ya uchaguzi, wasocial democrats na chama huru cha USPD walinufaika. Chama cha SPD kilishinda katika takriban sehemu zote.

Wakati huo, lilikuwepo Baraza la mpito ambalo ndilo lilikuwa linaongoza serikali chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa chama cha SPD, Friedrich Ebert. Jukumu lake lilikuwa kuiongoza serikali ya mpito baada ya utawala wa mfalme kuangushwa na kupeleka nchi kwenye njia ya utawala wa Demokrasia ya Bunge.

Lakini maelfu ya watu walikufa katika mchakato huo kutokana na hali iliyokaribia kusababisha vita vya wenyewe kwa wenyewe vya nchini Ujerumani. Miongoni mwa waliokufa alikuwa Rosa Luxembourg na Karl Liebknecht walioanzisha chama cha kikomunisti katika mwaka mpya.

Wakomunisti hao mashuhuri waliuliwa siku nne kabla ya kufanyika kikao cha Bunge la Katiba. Mauaji hayo hayakuwa nyota njema katika kuzaliwa kwa demokrasia nchini Ujerumani.

Mnamo mwezi wa Desemba mwaka 1918 bunge la Ujerumani lililokuwa linadhibitiwa na wademokrats, liliamua kujiengua lenyewe na hivyo kutoa fursa ya kupigwa kura ya haki na ya siri kwa mara ya kwanza katika historia ya Ujerumani.

Na kwa mara ya kwanza wanawake pia waliruhusiwa kushiriki katika kupiga kura au kusimama katika chaguzi. Hatua nyingine muhimu iliyochukuliwa ilikuwa ni kupunguza umri wa kuruhusu kupiga kura kutoka miaka 25 hadi 20.

Lakini matumaini ya chama wademokrats ya kupata kura za kutosha kuunda serikali peke yao haukutimia. Chama hicho kilipata asilimia 37.9 ya kura. Kiwango hicho hakikutosheleza kuunda serikali, chama hicho kilipaswa kushirikiana na wahafidhina, wakatoliki na chama cha mrengo wa kushoto wa wastani, DDP.

Chama cha kikomunisti hakikushiriki katika uchaguzi kwa sababu ingelimaanisha kuyasaliti mapinduzi. Kiongozi mashuhuri wa chama hicho, Rosa Luxembourg aliwashauri wenzake kutoususia uchaguzi. Mwanasiasa huyo alitambua kuwa chama cha SPD kilikuwa na nguvu kubwa zaidi miongoni mwa tabaka la wafanyakazi.

Kutokana na chama cha kikomunisiti kujiweka kando ya uchaguzi, wasocial democrats na chama huru cha USPD walinufaika. Chama cha SPD kilishinda katika takriban sehemu zote.

Mtaalamu wa historia, Marcel Bois akasema sehemu kubwa ya Ujerumani ilikuwa ni rangi nyekundu, wasocial demokrats walishinda takriban kwenye maeneo yote ya uchaguzi. Pia katika eneo la viwanda la Halle-Merseburg, chama cha USPD kilishinda na upande wa mashariki, kuna maeneo ambayo chama cha DNVP kilichopambana na chuki dhidi ya wayahudi kilikuwa na nguvu zaidi.

Wiki mbili baada ya uchaguzi, bunge la taifa lilikutana kwa mara ya kwanza, siyo mjini Berlin bali katika mji wa Weimar. Yalifuatia matukio muhimu baada ya kikao cha Bunge hilo. Mnamo mwaka 1920, Adolf Hitler alianzisha chama chake cha NSDAP na kilipata nguvu miaka 10 baadae kutokana na mgogoro wa kiuchumi.

Hatua nyingine muhimu ni kugawanya mamlaka katika mihimili ya Bunge, dola na mahakama ambapo mpaka leo Ujerumani inaongozwa katika msingi huo ila tu mamlaka ya Rais sasa yamebakia kuwa ya uwakilishi tu na siyo ya utendaji tangu mwaka 1949. ( DW)

# RC aagiza uharakishwaji wa ujenzi wa machinjio

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila ameuagiza uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kukamilisha haraka ujenzi wa machinjio ya kisasa inayojengwa katika eneo la Utengule ili kuwanusuru watumiaji wa kitoweo hicho na maradhi.

Chalamila alitoa agizo hilo baada ya kutembelea machinjio ya zamani iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na kubaini kuwa eneo hilo ni finyu na ni chafu hivyo linahatarisha afya za wananchi wanaofanya kazi katika eneo hilo.

Alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Stephen Katemba kusimamia kwa ukaribu na kuhakikisha machinjio hiyo mpya inakamilika na kufunguliwa ili ile ya zamani ifungwe.

**Machinjio hiyo ya zamani ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 kwa siku na kwamba ile ya kisasa inayojengwa itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe wengi zaidi.**

"Nimepata taarifa kuwa mnaijenga machinjio hii kwa zaidi ya shilingi milioni 900 ambazo ni kodi za wananchi, sasa hakikisheni fedha hizo zinapatikana na ujenzi unafanyika kwa viwango vinavyotakiwa ili tuwaondoe wananchi kwenye hii machinjio chafu," alisema Chalamila.

Aidha aliutaka uongozi wa Machinjio hiyo kuhakikisha wanadhibiti maji machafu wanayoyatumia yasitiririke kwenye Mto Mbalizi ambao unatumiwa na baadhi ya wakazi wa maeneo hayo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

Alitoa agizo hilo baada ya kupata malalamiko kutoka kwa wananchi ambao walidai kuwa wasimamizi wa machinjio hiyo hawajali afya za watu wengine.

Ofisa Mifugo na Uvuvi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Titus Mbijili alisema ujenzi wa machinjio ya kisasa ulianza mwaka 2009 baada ya kubaini kuwa eneo la awali ambalo linatumika mpaka sasa ni dogo na haliendani na mahitaji.

Alisema kwa sasa ujenzi huo ulikwama kutokana na kukosa fedha za kuendeleza huku akisisitiza kuwa fedha zikipatikana wakati wowote watamalizia na kuifungua.

Alisema machinjio hiyo ya zamani ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 kwa siku na kwamba ile ya kisasa inayojengwa itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe wengi zaidi.

"Kilichosababisha ujenzi usiendelee ni kukosekana kwa fedha lakini kwa sasa tayari tumefanya utaratibu wa kuendelea na ujenzi ili tukiimaliza tuifunge ya zamani ambayo mazingira yake sio rafiki," alisema Mbijili.

Baadhi ya wananchi wanaofanya kazi katika machinjio hiyo ya zamani waliiomba serikali kuharakisha haraka ujenzi huo ili waepukane na maradhi yanayoweza kuibuka kutokana na uchafu wa eneo hilo.

## Wananchi vijiji 21 watakiwa kuvuta subira

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

SERIKALI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imewataka wananchi wa vijiji 21 vya Wilaya hiyo vilivyokuwa vinatakiwa kuondolewa kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kuwa wavumilivu wakati utekelezaji wa agizo la Rais Dk. John Magufuli la kuvirasimisha likifanyiwa kazi.

Maelezo hayo yalitolewa juzi na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Oliver Sulle wakati wa Kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo ikiwa ni wiki moja baada ya Magufuli kuagiza zaidi ya vijiji na vitongoji 300 nchini vilivyokuwa vinatakiwa vioondolewe kwenye maeneo ya hifadhi viachwe.

Aidha Sulle, alimshukuru rais kwa uamuzi huo kwa madai kuwa utasaidia kupunguza migogoro ya ardhi katika Wilaya hiyo ambayo kwa mkoa wa Mbeya inaongoza kwa kuwa na migogoro ambayo baadhi ilikuwa inasababishwa na tafsiri ya Tangazo la Serikali namba 28 la mwaka 2008 (GN. 28)

Alisema migogoro hiyo ilikuwa inawasumbua watendaji wa Halmashauri hiyo kwa madai kuwa walikuwa wanaulizwa maswali kwenye mikutano ya wananchi huku wakikosa majibu ya kuwapa lakini agizo la rais limeleta suluhisho.

"Tumepata taarifa kuwa baadhi ya watu ambao walishaondolewa wanataka waanze kurudi bila maelekezo ya serikali, hao niwambie kuwa watakuwa wanavunja sheria hivyo tunawataka wawe wapole wasubiri maelekezo ya serikali," alisema Sulle.

Alisema kwa mujibu wa maagizo ya rais ni kwamba ndani ya mwezi mmoja kila kitu kiwe tayari na hivyo wao kama viongozi wamejipanga na wapo tayari kushirikiana na wananchi katika kuhakikisha maelekezo hayo yanatekelezwa. Baadhi ya madiwani waliipongeza Serikali ya awamu ya tano kwa utendaji kazi wake ikiwemo kutatua migogoro isiyokuwa ya lazima na kufanya uwekezaji wenye tija ikiwemo kufufua Shirika la Ndege la Taifa (ATCL).

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Salumu Bahati alisema tangu mwaka 2008 wananchi wa wilaya hiyo walikuwa hawaishi kwa amani kutokana na tafsiri ya Gn28 iliyokuwa inamega ardhi kubwa ya wananchi na kupelekea vijiji vingine kufutika.

Alisema maelekezo yaliyotolewa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Taifa ambaye pia ni Rais Dk. Magufuli limefungua ukurasa mpya wa maisha ya wananchi wa vijiji hivyo ambao asilimia kubwa ni wakulima.

Alisisitiza kuwa kwa sasa Halmashauri itaandaa utaratibu mzuri baada ya maelekezo ya wizara zilizoagizwa na rais ili wananchi wapewe maelekezo ya namna ya utekelezaji wake.

"Hawa wananchi walifikia muda wakawa wanaichukia serikali yao kutokana na GN 28 lakini naamini baada ya maelekezo ya rais hawa wananchi watakuwa na amani na wataiamini serikali yao," alisema Bahati.

Aidha alisema uimarishaji wa usafiri wa anga utasaidia kuimarisha pia sekta ya utalii kwa kuzitumia ndege hizo kuwasafirisha watalii kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi.



Muuza sambusa akiwa katika harakati za kutafuta wateja mitaani, huku akiwa na chombo chenye kuhifadhia usafi wa bidhaa hiyo eneo la Ilala jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Balozi wa Japan aahidi ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu,** RUNGWE

BALOZI wa Japan Nchini Tanzania, Shinichi Goto amesema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania kutatua changamoto zinazowakabili wananchi hususan katika sekta ya elimu.

Akizungumza Wakati akikabidhi jengo jipya la hosteli ya wasichana katika shule ya Sekondari ya kata ya Masoko wilayani Rungwe ambalo limejengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Japan, Balozi Goto alisema kuwa lengo la ushirikiano huo ni kuendeleza na kudumisha uhusiano uliopo baina ya Tanzania na Japan.

"Japan itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuboresha miundombinu ya elimu na changamoto nyingine zinazowakabili wananchi kwa lengo la kudumisha ushirikiano na undugu uliopo baina ya nchi zetu," alisema Balozi Goto.

Alisema ofisi yake ilikubali kujenga hosteli ya wasichana katika Shule ya Sekondari ya Masoko baada ya kupokea maombi maalum kutoka kwa Naibu Spika, Dk. Tulia Akson ambaye aliwaeleza kuwa wanafunzi wanosoma shuleni hapo wanatembea umbali mrefu kwenda shuleni.

Alisema msaada huo ni sehemu ya utekelezaji wa sera za nchi yake ambayo ilishaamua kwa dhati kuwa na uhusiano wa kindugu na Tanzania.

Akizungumza wakati akipokea jengo hilo, Naibu Spika Dk. Tulia Akson alisema kukamilika kwa bweni hilo kutakuwa ni mkombozi kwa wanafunzi hususani wa kike ambao wanatembea umbali wa zaidi ya kilometa 20 kufuata elimu shuleni hapo.

Dk. Tulia alisema kuwa wanafunzi wa shule hiyo wanashindwa kufanya vizuri kwenye masomo kutokana na uchovu wanaoupata kutokana na safari ndefu ya kufuata elimu.

Hata hivyo alisema kuwa athari ni kubwa zaidi kwa wasichana ambao wanakutana na vishawishi vingi wakiwa njiani kwenda na kutoka shuleni na kwamba wakati mwingine hali hiyo huchangia kupata mimba kabla ya kumaliza masomo yao.

Alisema pamoja na msaada huo wa kujengewa bweni la wasichana, bado uhitaji ni mkubwa kwa vile hosteli iliyojengwa kwa msaada wa Japan inao uwezo wa kuhudumia wanafunzi 48 tu wakati shule hiyo inao wanafunzi wengi zaidi wenye uhitaji.



HABARI DODOMA

# CCM yakunjua makucha kutafuta ufumbuzi tatizo

**Na Augusta Njoji,** KONGWA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Dodoma, kimeagiza Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa kukamilisha mradi wa maji ifikapo Februari 19 mwaka huu.

Hatua hiyo itasaidia wananchi kuondokana na changamoto ya maji inayowakabili kwa muda mrefu.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa CCM mkoani humo, Godwin Mkanwa, katika ziara ya Kamati ya Siasa Mkoa alipokuwa akikagua utekelezaji wa ilani ya chama hicho wilayani humo.

Alisema katika ilani yake ya uchaguzi ya mwaka 2015-2020 , CCM iliahidi upatikanaji wa maji karibu na wananchi, hivyo ni jukumu la halmashauri kukamilisha mradi huo.

Alisema wananchi wa Kongwa wanateseka kwa kukosekana kwa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi yao.

**Katika uboreshaji wa vituo vya afya wamepata Sh.milioni 800 kwa ajili ya kituo cha afya cha Mlali na Ugogoni, ujenzi wa vituo hivyo upo vizuri.**

"Mradi huu ukikamilika ni mkombozi wao, niwaahidi hadi kufikia Februari 19, maji yataanza kutoka," alisema.

Kadhalika, aliitaka halmashauri hiyo kuweka mfumo wa kielektronki katika kukusanya malipo ya maji katika mji wa Kongwa na Kibaigwa ili kuzuia upotevu wa fedha.

Kwa upande wake, Mhandisi wa Maji Kongwa, Kaitaba Lugakingira, alisema ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 85 na utakapokamilika utazalisha lita za ujazo milioni 1.147 kwa siku.

"Na utatoa huduma ya maji kwa wakazi takribani 31,252 wa kata za Kongwa na Ugogoni, hii itafanya vyanzo vyote vya maji yaani vya zamani na vipya kuwa na uwezo wa kuzalisha lita za ujazo milioni 3.097 kwa siku ambayo ni sawa na asilimia 128," alisema mhandisi huyo.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo kwa sasa hakuna changamoto zozote zilizopo na Mkandarasi Hematec Investment Limited anayejenga mradi huo amekwishalipwa fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.166 kwa awamu nne.

Naye, Mkuu wa Wilaya hiyo, Deogratius Ndejembi, alieleza jitihada za wilaya katika kusimamia miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya.

Alisema katika uboreshaji wa vituo vya afya wamepata Sh.milioni 800 kwa ajili ya kituo cha afya cha Mlali na Ugogoni, ujenzi wa vituo hivyo upo vizuri.

"Sisi wilaya, jicho letu lipo kwenye miradi ili kuhakikisha wanapata huduma iliyokusudiwa," alisema.



Baadhi ya wageni kutoka nchini China walioshiriki mashindano ya kuimba na kucheza kwa lugha ya Kichina, wakifurahia wanafunzi wa Kitanzania (hawapo pichani) kwenye mashindano ya kuwatafuta washiriki, yaliyofanyika jijini Dodoma, maonyesho hayo yatafanyika Beijing China, mwaka huu kwa kushirikisha nchi mbalimbali duniani. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wakulima kanda ya kati wapewa somo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKULIMA kanda ya kati wameshauriwa kuwekeza katika kilimo cha biashara na chakula kwa kupanda mbegu bora ili kupata mavuno mengi.

Pamoja na hilo, wakulima wamehimizwa kuwatumia wataalamu wa kilimo badala ya kulima kwa mazoea kwa kuwa hali hiyo husababisha kukosa mavuno ya kutosha.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la TAG Eden Christian Centre uwanja wa ndege Dodoma, Issack Baraka, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya ibada.

Alisema ni vyema wakulima wakatumia mvua zinazonyesha kupanda mbegu bora ambazo zitawawezesha kupata mavuno mengi.

"Mvua hizi zinazoendelea kunyesha pandeni miti ya matunda na kivuli ili kulinda mazingira ambayo yatakayowezesha kupata mvua za kutosha," alisema.

Aidha, aliwataka wanafunzi wa shule ya msingi na sekondari kusoma kwa bidii ili waweze kufanya vizuri kwenye masomo yao.

"Tunategemea ufaulu mzuri ambao utakaowafanya kwa upande wa wazazi na walezi kufurahia matunda mkizingatia kuwa wazazi hao tayari wametimiza wajibu wao," alisema.

Hata hivyo mchungaji huyo alilitaka kanisa lake kuendelea kuliombea taifa na serikali yake ili amani na mafanikio ya kimaendeleo yaendelea kudumu kwa Watanzania wote bila kujali itikadi zozote.

Kwa upande wake, mwanafunzi kutoka Chuo cha Mipango Dodoma, Leticia Athumani, aliwataka waumini wa kanisa hilo kuunga juhudi zinazofanywa na viongozi wa dini na serikali ambao wamekuwa wakikemea vitendo viovu.

Alisema viongozi wa serikali na dini wamekuwa wakikemea vitendo, hivyo hawana budi kuunga mkono juhudi hizo.

# Serikali yaombwa kudhibiti wanaotapeli yatima

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kudhibiti taasisi, mashirika na watu binafsi wanaojipatia mamilioni ya fedha na misaada kwa wafadhili kwa ajili ya watoto yatima, lakini haiwafikii walengwa.

Ombi hilo lilitolewa jana na watoto wanaolelewa katika kituo cha Shirika la Malezi Endelevu (SHIME) jijini Dodoma, kwa niaba ya wenzao wakati walipokuwa wakipokea misaada mbalimbali iliyotolewa na wanavyuo kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

Akizungumza mtoto Raheli Rafael alisema kupitia wizara husika inatakiwa kuhakikisha wanadhibiti utapeli wa aina hiyo.

Alisema kumekuwa na vituo hewa vya kulelea watoto yatima na kujipatia mamilioni bila kuwafikia yatima.

Alieleza kuwa pamoja na juhudi za makusudi zinazofanywa na serikali kwa ajili ya kuhakikisha watoto yatima wanapata haki sawa kwenye mahitaji yao, bado kuna utapeli unaofanywa baadhi ya taasisi, mashirika na watu binafsi kwa udanganyifu huo.

"Hivyo sisi kama watoto yatima kwa niaba ya wenzetu tunamuomba Rais wetu ambaye yupo mstari wa mbele kudhibiti vitendo hivyo viovu, kwa kuangalia kwa jicho la upana vituo vya kulelea watoto yatima kutokana na kuwapo kwa udanganyifu wa matapeli," alisema.

Kwa upande wake, Moses Tobias, alisema kuwa bado kuna changamoto kwenye vituo vya kulelea watoto kutokana na kuwapo kwa watu binafsi, taasisi na mashirika kuwa na vituo vinavyoishia mifukoni mwao.

Alisema wakati wakihitajika kusaidiwa katika mahitaji yao ya kimsingi ikiwamo elimu, afya, malazi, mavazi na chakula bado kuna baadhi ya watu wana vituo vyao vipo mifukoni ambavyo wamekuwa wakijipatia mamilioni ya fedha.

Kwa upande wake, mmoja wa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), Ida Theophil, aliiomba serikali kuwekeza kwenye vituo vya watoto yatima ili kuwapunguzia ugumu wa kupatiwa misaada mbalimbali.

Alisema kuwa serikali ikiwekeza kwa kufadhili mahitaji muhimu kwenye hivyo vituo vitaweza kujisimamia wenyewe na kuwabaini wale wanaojihusisha na uanzishaji wa vituo visivyosajiliwa kwa mujibu wa kisheria.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Shirika la Malezi Endelevu (SHIME), Zawadi Mgeni, alivishauri vituo hivyo kusajiliwa ili vitambuliwe serikali kwa lengo la kubaini vinavyowahujumu watoto hao.

# Tamwa yapongeza ugatuzi madaraka

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imepongezwa kwa kufanikisha mpango wa ugatuzi wa madaraka, umesaidia kuharakisha maendeleo kwa wananchi katika sekta mbalimbali za maendeleo na ustawi wa jamii.

Hayo yalisemwa na Ofisa Mwandamizi wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tamwa), upande wa Zanzibar, Asha Abdi, wakati akizungumza na washiriki ambao walifanya kazi na mradi wa kushahijisha uwajibikaji katika ngazi mbalimbali (Paza), ambao unatekelezwa kwa pamoja na Chama cha Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (Wahamaza).

Ofisa huyo alisema kupitia utekelezaji wa mpango wa ugatuzi, umesaidia huduma nyingi za jamii kupelekwa kwa moja kwa moja katika Halmashauri za Serikali za Wilaya.

Alieleza kuwa ugatuzi umeleta mabadiliko katika sekta ya elimu ikiwamo ujenzi wa majengo ya shule yanayozingatia sifa kwa makundi mbalimbali ikiwamo watu wenye ulemavu.

Aidha, alisema katika mradi wa kushajihisha na kujenga uwajibikaji katika Halmashauri za Serikali za Mitaa, wananchi wanaibua kero na changamoto zinazowakabili katika shehia zao.

"Faida ya ugatuzi tumeziona ambapo sasa huduma muhimu za jamii zimekuwa zikifikishwa moja kwa moja kwa wananchi pamoja na kupata fursa ya kuwasilisha kero na changamoto zinazowakabili katika vikao vya pamoja na uongozi wa halmashauri," alisema.

Akiwasilisha taarifa ya tathmini ya awali ya mradi wa (PAZA), mwanaharakati Asha Aboud Mzee, alisema wananchi wa vijijini Unguja na Pemba sasa wamejenga uelewa mkubwa wa kuibua changamoto zinazowakabili kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Alisema mradi ulifanya kazi katika wilaya sita za Unguja na Pemba, ambapo kero za maji, ujenzi wa shule ziliibuliwa na wananchi.

"Mafanikio makubwa ya utafiti wa mradi wa (PAZA) umeonyesha kwamba sasa wananchi wamekuwa na uelewa mkubwa na kujenga ushirikiano kati yao na viongozi wa halmashauri za serikali za mitaa katika kuwasilisha kero zao," alisema.

Kwa upande wake Katibu wa Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Wasioona Wilaya ya kati Unguja, Yunus Kassim Khatib, aliupongeza mradi huo ambao umesaidia kuzipatia changamoto zinazowahusu wanafunzi wenye ulemavu ikiwamo kurekebishwa kwa miundombinu ya shule.

"Mradi huu hatutausahau kwa sababu umezipatia ufumbuzi changamoto nyingi zilizokuwa zikiwakabili walemavu kwa kuboresha miundombinu ya shule na kuweza kufikiwa kirahisi," alisema.

# Serikali yaahidi kushirikiana na taasisi ajira kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema kuwa serikali itaendelea kushirikiana na taasisi binafsi kukabiliana na changamoto ya ajira kwa vijana.

Akifungua mafunzo ya siku tatu ya ufugaji kuku kwa vijana wa mikoa miwili, alitaka hatua hiyo ipunguza idadi ya vijana wanaokaa vijiweni bila ya kufanya kazi.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo serikali ya mkoa kupitia mpango wa kuwawezesha vijana unaotekelezwa kupitia Taasisi ya MIMI na WEWE kwa makundi ya vijana kutoka shehia mbalimbali watapatiwa kuku kwa ajili ya kuanzisha miradi ya ufugaji ili wajipatie kipato.

**Ufugaji wa kuku unahitaji uthubutu na kwamba kupitia kwa maofisa wa kilimo na mifugo wataendelea kutoa ushauri wa kitaalamu pamoja na kuyakagua mabanda ya vijana hao.**

Aliwataka vijana hao kuzingatia mafunzo watakayopatiwa ili kuufanya mradi huo kuwa endelevu na wenye tija kwao na jamii kwa ujumla.

Aidha, alisema kuwa kabla ya kutolewa kwa mafunzo kwa vijana hao, vijana 12 walipatiwa mafunzo ili waweze kuwafundisha wenzao.

Alisema hatua hiyo ni hatua ya tatu katika utekelezaji wa mradi huo, ambapo awali taasisi hiyo iliandaa majengo, kununua kuku pamoja na kuandaa wakufunzi wa mafunzo hayo, jambo ambalo limesaidia kuimarisha uelewa wa vijana katika kujitegemea.

Ofisa Kilimo na Mifugo Mkoa wa Mjini Magharibi, Ali Omar Makame, aliwapongeza vijana hao kwa kukubali kushiriki katika mafunzo hayo na kuwataka kuwa tayari kujiunga na ushirika wa wafugaji wa kuku utakaoanzishwa.

Alisema ufugaji wa kuku unahitaji uthubutu na kwamba kupitia kwa maofisa wa kilimo na mifugo wataendelea kutoa ushauri wa kitaalamu pamoja na kuyakagua mabanda ya vijana hao.

Kwa upande wake msimamizi wa mafunzo hayo, Rashid Mohammed Othman, alisema mafunzo hayo yanahusisha zaidi ya vijana 100 kutoka mabaraza ya vijana, madarasa ya itikadi ya vyama mbalimbali na wenyeji wa kijiji cha Mbaleni wanapofugwa kuku hao ili kuongeza fursa ya ajira kwa vijana.



Wanafunzi wa darasa la kwanza wa shule ya msingi wakitembea pamoja kutoka shuleni. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Waziri atoa mwezi mmoja kumaliza uchafu

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Serikali za Mitaa, Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, ametoa mwezi mmoja kwa mabaraza ya manispaa zote za Mkoa wa Mjini Magharibi kukaa pamoja na kuweka mikakati ya kumaliza tatizo la uchafu katika maeneo mbalimbali ya miji.

Waziri Haji alitoa agizo hilo kufuatia kuwapo kwa uzalishaji mkubwa wa taka katika maeneo ya miji na kupelekea uchafuzi wa mazingira na kuibua maswali mengi yanayoulizwa katika vikao mbali mbali vya baraza ikiwa ni pamoja na kuharibu mandhari ya miji.

Akizungumza wakati akiwa katika ziara ya kukagua ujenzi wa dampo la kisasa katika eneo la Kibele alisema, serikali imeingia gharama ya kuwekeza katika manispaa, hivyo ni vyema wahusika kuwa makini katika kusimamia miradi ya maendeleo hasa katika suala la usafi.

Akizungumzia kuhusu ujenzi huo aliwaagiza viongozi wa baraza ya manispaa kukaa pamoja na mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi wa dampo hilo, ili kufanya naye mazungumzo na kuhakikisha linatumika kwa utupaji wa taka.

Aidha, waziri huyo aliwaagiza Wakuu wa Mkoa Kusini Unguja na Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi kwenda kukagua eneo litakalotumika kwa utupaji wa maji katika kijiji cha Cheju Chuchumile Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Katika hatua nyingine waziri huyo aliwaagiza madiwani wa Mkoa wa Mjini Magharibi kushirikiana kwa karibu na watendaji, maofisa na wakurugenzi wa Manispaa za Mkoa huo kufanya kazi kwa ushirikiano.

Aliwataka madiwani hao kulipa umuhimu wa kipekee suala la usafi na kuacha mivutano isiyokuwa ya lazima na kuweza kuleta ufanisi katika utekelezaji wa shughuli zao na utoaji wa huduma kwa jamii.

Wakati huo huo, Waziri Kheri aliwataka wafanyabishara wa maduka eneo la Darajani kuwa tayari kuhama kwa muda kupisha ukarabati wa maduka yao ambayo yanaonekana kuchakaa ili yalete sura nzuri.

Alieleza kuwa serikali kwa makusudi imeamua kuyafanyia ukarabati maalum maduka hayo ambayo yapo katika kiungo kikubwa cha utalii.

Akitoa maelezo ya kitaalamu kuhusu ujenzi wa dampo la kisasa la kuhifadhia taka, Mkuu wa Mipango Miji na Ujenzi wa Baraza la Manispaa ya Mjini, Mzee Khamis Juma, alisema ujenzi huo wa kisasa umezingatia mahitaji yote muhimu ikiwamo miundombinu na kuwa na maeneo maalum ya ofisi, karakana na mashine za kusarifu taka.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

**PROJECTS CREATE EMPLOYMENT** AND GENERATE MONEY:Learn project proposal DESIGNING,Find project DONORS,Establish project NGO:0787 505108/ 0769 505108/0716 581562

## MAGARI/VIPURI

**GARI HONDA CRV YA MWAKA 2007 INAUZWA.** INATEMBEA NA IKO KATIKA HALI NZURI SANA. BEI MAELEWANO PIGA 0755834730 AU 0755260247

## NYUMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo Ligula Mtwara Township Area 3200 SQ FEET. Kwa mawasiliano piga simu: 0746 348946 / 0685 831772.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**JACOB A. NDIMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.540/036** kilichotolewa na Shule ya Sekondari Maposeni mwaka 1993.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**SO/RB/4357/2016**

115017302

## KUPOTEA KWA VYETI



**Beatrice Emily Mallya** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.327/4 kilichotolewa na Shule ya Sekondari Minja mwaka 1987. Na kadi ya mpiga kura, Barua ya kuthibitishwa kazini na Barua ya ajira.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa:**
**AR/RB/477/2019**

115017502

## KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

**SALMA SALUM ABDALAH** anatangaza kupotelewa na kadi ya TRAILER yenye namba za usajili **T. 334 DDX.** CHASSIS **NO; C017560.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MS/RB/0122/2019.**

115018902

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**GODWIN TRAELY MUSHI,** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Yenye namba za usajili **T 901 DFF,** aina ya TOYOTA Mark X Chassis namba. **GRX1203062098,** Engine namba. **4GR4008098,**

Yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa Polisi:
**KJN/RB/957/2019**

115019202

## KUPOTELEWA NA KADI YA TRAILER

**VANILA ENTERPRISE COMPANAY** anatangaza kupotelewa na kadi ya TRAILER aina ya York Trailer yenye rangi yal MULTICOLOUR namba za usajili T378 ANE Chassis namba AO38459 Engine no-.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**Taarifa ya polisi:**
**DOM/TR/RB/111/2019**

115019402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No.16/2019**

**Ombi la BAHATI MOHAMED MKUMBUKWA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MOHAMED MKUMBUKWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 29/01/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.
tarehe 22/01/2019.

115020102

**MAHAKAMA YA MWANZO MAKANGWA**
**WILAYA YA CHAMWINO DODOMA**
**MIRATHI NAMBA 02 2019**

KATIKA MAKAMA YA MWANZO MAKANGWA WILAYA YA CHAMWINO DODOMA OMBI LA ISAYA MNYANGHALI WA MVUMI MISSION DODOMA KUTEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU VERIAN MNYANGHALI ALIYEKUWA ANIISHI MVUMI MISSION DODOMA.

MTU YEYOTE MWENYE PINGAMIZI KATIKA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO TANZANIA BARA NA KISIWANI, UNATAKIWA ULETE PINGAMISI HILO KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MAKANGWA DODOMA

KABLA MSI MAMIZI HAJATEULIWA KUWA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU HUYO NDANI YA MIEZI MITATU.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA MAHAKAMA YA MWANZO MAKANGWA LEO 15/01/2019

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MAKANG'WA

115019302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

Usimamizi wa mirathi **No.18/2019**

Ombi la **MSAFIRI ALLY SAID** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **ALLY SAID**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/02/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/01/2019.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MOROGORO

215019102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**Kumb.Na MADAI NA 436/2018**

**YAH: KESI YA MADAI NA 01 YA 2019**

**MADAI............................HADIJA MUMBA**

**DHIDI YA**

**MDAIWA............................SEIF SALUMU**

Unaamriwa na mahakama ya mwanzo mjini mwanza kufika tarehe 24/01/2019 saa 2:00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyounguliwa hapa mahakamani.endapo hutafika mahakamani, shauri litasikilizwa na kutolea uamuzi bila wewe kuwepo.

115020202

## KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI

**JOHN IGOTI JOHN** anatangaza kupotelewa na kadi za magari. Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 160 DLS TOYOTA RAV 4**. Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 313 ATY MITSUBISHI FUSO**. Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 620 AUR TOYOTA HILUX.**

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo **cha polisi.**

**Taarifa ya polisi:**
**KAH/TR/RB/64/19.**

115018702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GODFREY GABRIEL NZALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 546 AET**, aina ya MITSUBISHI FUSO Chassis namba **FK417J740477.** Engine namba 6D16753428.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**OB/RB/711/2019.**

115018802

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**BAKIR NURDIN MOHAMMEDALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA DUET. yenye namba za usajili **T917 AVM.** CHASSIS NO. **M100A015238.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

**Taarifa Polisi.**
**TR/RB/197/2019.**

215018002


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2018
(Kiasi kwa Shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA 31.12.2018 | ROBO MWAKA ILIYOPITA 30.09.2018 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,744 | 4,218 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 17,681 | 12,035 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 23,377 | 11,996 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 27,664 | 50,458 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | 11 | 10 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 98,411 | 88,211 |
| 12 | Mali Nyingine | 2,763 | 2,506 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,279 | 1,333 |
| **16** | **Jumla ya Mali** | **174,929** | **170,769** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,272 | 1,272 |
| 18 | Amana za Wateja | 132,158 | 128,833 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 137 | 139 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 41 | 24 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 20 | 6 |
| 27 | Dhima Nyingine | 2,494 | 1,615 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **136,122** | **131,888** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **38,807** | **38,880** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 937 | 810 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 21,938 | 22,939 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,948 | 2,021 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,984 | 3,111 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **38,807** | **38,880** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 7,248 | 10,947 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 6,567 | 7,088 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,396 | 1,545 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 22% | 23% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 7% | 8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76% | 69% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 56% | 52% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 85% | 88% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3% | -2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2% | -1% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2018
(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA SASA 31.12.2018 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 31.12.2017 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,262 | 3,517 | 13,582 | 14,177 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,218 | 1,292 | 4,676 | 4,845 |
| **3** | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,044** | **2,225** | **8,906** | **9,332** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | (0) | - | 1,259 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 606 | 406 | 1,018 | 1,427 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **568** | **584** | **1,931** | **1,959** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 54 | 159 | 349 | 530 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 463 | 425 | 1,519 | 1,423 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 51 | - | 64 | 6 |
| **7** | **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,457** | **1,245** | **4,902** | **5,647** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 712 | 352 | 1,869 | 1,613 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 51 | 121 | 281 | 711 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 694 | 772 | 2,753 | 3,323 |
| | 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| **8** | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **549** | **1,158** | **3,658** | **4,217** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 622 | 360 | 1,710 | 1,381 |
| **10** | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **-73** | **798** | **1,948** | **2,836** |
| **11** | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **-73** | **798** | **1,948** | **2,836** |
| **13** | Idadi ya Waajiriwa | **50** | **50** | **48** | **48** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (7) | 80 | 195 | 284 |
| **15** | **Idadi ya Matawi** | 4 | **4** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.39% | 0.52% | 1.17% | 2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.75% | 2.00% | 5.24% | 8% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 55.79% | 44.00% | 42.58% | 50% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 1.62% | 2.00% | 4.76% | 20% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO ILIYOISHIA 31.12.2018
(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA YA SASA 31.12.2018 | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA 30.09.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.12.2018 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.12.2017 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 632 | 356 | 3,658 | 4,217 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | | | | |
| | -Hasara katika Mali | 660 | 141 | 1,246 | 1,680 |
| | -Prior Period Adjustment | 1 | 378 | (260) | - |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (10,805) | (399) | (13,420) | (32,568) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 3,325 | 3,940 | 6,566 | 2,561 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 908 | (6,277) | (1,557) | 2,640 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 5,465 | (855) | 3,992 | (632) |
| | -Kodi Iliyolipwa | (428) | (557) | (1,710) | (1,612) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | 8,983 | (445) | 1,707 | 1,593 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **8,742** | **(3,718)** | **222** | **(22,121)** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | (1) | (39) | (45) | (276) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | (11,380) | (1,400) | (6,044) | 2,080 |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(11,382)** | **(1,439)** | **(6,089)** | **1,804** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| IV | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **(2,640)** | **(5,157)** | **(5,867)** | **(20,317)** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 34,100 | 39,257 | 37,328 | 57,644 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **31,460** | **34,100** | **31,460** | **37,328** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2018
(Kiasi kwa shilingi milion)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **22,272** | **4,068** | **781** | **-** | **37,120** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,948 | - | - | - | 1,948 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 84 | (84) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (156) | - | 156 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (261) | - | - | - | (261) |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **23,887** | **3,984** | **937** | **-** | **38,807** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | 10,000 | - | 21,461 | 2,317 | 507 | - | 34,285 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 2,836 | - | - | - | 2,836 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (1,751) | 1,751 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | (274) | - | 274 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **22,272** | **4,068** | **781** | **-** | **37,120** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.12.2018**

Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir (Mkurugenzi Mtendaji) | | 16th January, 2019 |
| Deogratias Edward Ndushi Mkuu wa Fedha | | 16th January, 2019 |
| Mwita Mohamed Mwita (Mkaguzi wa Ndani) | | 16th January, 2019 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 16th January, 2019 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava | | 16th January, 2019 |

## HABARI MICHEZO




# HAZARD:

## Bado nataka kucheza Real Madrid

**LONDON, ENGLAND**

EDEN Hazard amesisitiza kwa mara nyingine tena mpango wake wa kutua katika Klabu ya Real Madrid, na kubainisha wazi kwamba angependa siku moja kuichezea klabu hiyo.

Akizungumza na Jarida la michezo la Ufaransa mapema wiki hii, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji amesema bado angependa kwenda Real Madrid, akibainisha kuwa alitaka kuondoka pale Stamford Bridge baada ya kombe la Dunia.

"Nimeshinda kila kitu England, kuanzia kombe la Ngao ya jamii, lakini hilo halimaanisha kwamba naondoka.

"Mara zote nimekuwa nikisema nataka kucheza sehemu nyingine tofauti na England. Lakini kuna vitu ambavyo vinaniwezesha mimi kubaki."

Alipoulizwa uwezekano wa kwenda Real Madrid, akajibu: "Kwanini isiwe hivyo? Unajua vizuri kabisa. Unauliza swali ambalo jibu lake unalijua.

"Baada ya kombe la dunia, nilitaka kuondoka, lakini mwisho wa siku nilibakia Chelsea na nacheza katika moja ya misimu yangu bora zaidi hapa, hadi sasa."

Wakati huo huo, Hazard amepuuzia kwamba atakwenda kujiunga na timu ambayo itafundishwa na Zinedine Zidane, ambaye awali aliwahi kusema yeye ndiye aliyemvutia kwenye soka wakati akiwa mdogo.

"Kuhusu Zinedine Zidane, hilo ni tofauti. Kama akienda Manchester kesho kwa mfano, mimi sitakwenda kule."

## Henry aomba radhi kwa kumwita mchezaji bibi

**MONACO,** Ufaransa

KOCHA wa timu ya Monaco, Thierry Henry (pichani chini), ameomba radhi kwa kumuita beki wa Strasbourg 'Bibi' wakati timu yake ikipigwa 5-1, akisema kwamba hiyo siyo mara yake ya kwanza kulitumia neno hilo.

Henry amelazimika kuomba radhi hiyo baada ya kumtusi beki huyo wa Strasbourg, Kenny Lala kwa kumuita bibi wakati wa mchezo wao siku ya Jumamosi, ukiwa ni mchezo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Henry amejutia kosa hilo baada ya kunaswa na kamera akimwita mchezaji huyo wa Strasbourg, Lala 'bibi' kwenye mchezo wao wa Ligue 1 ambao waliambulia kichapo hicho kibaya cha mabao 5-1.

Tukio hilo lilitokea kabla ya kipindi cha kwanza kumalizika wakati Strasbourg ikiongoza kwa mabao 2-1, ambapo Lala aliuchelewesha mpira ndipo Henry akanaswa na runinga ya Ufaransa akitumia lugha ya matusi kwa mchezaji huyo.

"Ndiyo, najutia kwa maneno yangu, ila siyo mara yangu ya kwanza wakati mwingine natumia hata kwa lugha ya Kiingereza," amesema Henry.

"Nilikuwa nimeghadhibika, samahani sana lakini na mimi ni binadamu."

Henry ameanza kibarua cha kuifundisha Monaco Oktoba mwaka jana huku akifanikiwa kushinda michezo minne pekee tangu alipochukua jukumu hilo.



# Ronaldo apandishwa kizimbani kwa kukwepa kodi

**MADRID,** Hispania

CRISTIANO Ronaldo jana Jumanne aliwasili mjini Madrid ambapo anakabiliwa na mashtaka ya kukwepa kulipa kodi ambayo huenda yakasababisha kupigwa faini ya euro milioni 18.8.

Jaji alikataa ombi la mchezaji huyo kuhudhuria kesi hiyo kupitia kanda ya video ama hata kuingia katika jumba hilo kwa kutumia gari ili kuzuia kuandamwa na vyombo vya habari.

Alitarajiwa kukiri mashtaka hayo katika makubaliano ambayo yatamlazimisha kuhudumia kifungo cha mezi 23 jela au kulipa faini.

Mchezaji huyo wa Juventus ambaye aliichezea klabu hiyo usiku wa kuamkia mashtaka hayo aliwasili akiwa anatabasamu.

Wakili wake alikuwa amehoji kwamba kutokana na umaarufu wake, alipaswa kutumia lango kuu la mahakama kutokana na hali ya usalama.

Ronaldo ambaye ni mshindi mara tano wa Ballon d'Or na kuwa miongoni mwa wachezaji bora duniani, anatuhumiwa kwa kukwepa kulipa kodi nchini Hispania kati ya mwaka 2011 na 2014, wakati alipokuwa akiichezea klabu ya Real Madrid.

Kesi hiyo inaangazia mikataba ya haki za picha zake.



Viongozi wa mashtaka wanasema kuwa fedha hizo zilipitishwa kupitia kampuni zinazotozwa kodi ya chini katika mataifa ya kigeni ili kukwepa kulipa kodi iliohitajika.

Mwaka 2017, wakati madai hayo yalipotangazwa rasmi, viongozi wa mashtaka walisema kuwa ulikuwa ukiukaji wa ahadi yake nchini Hispania.

Lakini wakili wa Ronaldo alisema kuwa kutoelewana kuhusu kile kilichohitajika na kile ambacho hakikuhitajika chini ya sheria za Hispania na kuzuia jaribio lolote la kukwepa kulipa kodi.

Makubaliano hayo yaliofanyika Juni mwaka jana yaliafikiwa na mamlaka ya ushuru nchini Hispania.

Ronaldo sio mchezaji wa kiwango cha juu wa pekee kukabiliana na mkono wa mamlaka ya ushuru nchini Hispania.

Mchezaji mwezake wa zamani, Xabi Alonso pia aliwasili mahakamani siku hiyohiyo kwa mara ya kwanza akishtakiwa na shataka kama lake la makosa ya haki za picha zake ya takriban euro milioni 2.

Nyota wa Barcelona Lionel Messi alinusurika kifungo kwa mashtaka kama hayo yanayohusisha haki za picha zake, akilazimika kulipa mamilioni kama faini na ushuru.

Neymar da Silva Santos Junior alikuwa katikati ya mgogoro wakati Barcelona ilipopigwa faini ya mamilioni ya fedha baada ya kushtakiwa kwa kukwepa kulipa kodi lakini akazuia kukiri shtaka hilo.

Mchezaji wa Real Madrid Marcelo Vieira alikiri mashtaka ya kukwepa kulipa kodi na kukubali kuondolewa kifungo cha miaka minne jela kufuatia hatua yake ya kutumia kampuni za kigeni kumpitishia takriban Yuro nusu milioni ya mapato yake.

## HABARI MICHEZO



# RONALDO
## atetewa na Allegri kukosa penalti

**TURIN,** Italia

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri hakuonekana kukerwa baada ya Cristiano Ronaldo kukosa pealti, lakini alihisi mshambuliaji angeweza kufunga.

Ronaldo alipata penalti katika kipindi cha pili wakati Juve wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Chievo kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, Jumatatu.

Douglas Costa, Emre Can na Daniele Rugani ndio walifunga mabao hayo kwa Juve na kuiwezesha kuongoza msimamo kwa pointi tisa zaidi.

Allegri alisema timu yake kushinda lilikuwa jambo la muhimu na sio Ronaldo kukosa penalti, ingawa alihisi kwamba mshambuliaji huyo angeweza kufunga kwenye kipindi cha kwanza.

"Inatokea kukosa penalti na sio jambo la ajabu," alisema akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Sidhani kama hii ni mara ya kwanza kwa Ronaldo kukosa penalti kwenye maisha yake ya soka. Jambo la muhimu ni kwamba timu ilishinda."

Aliongeza: "Yeye (Ronaldo) alitaka kufunga katika kipindi cha pili, kiufundi alicheza vizuri.

"Katika kipindi cha kwanza, alikuwa na haraka mno ya kutaka kufunga. Katika kipindi cha pili alipocheza soka kwa utulivu alikuwa na nafasi mbili au tatu za kufunga."

Ronaldo kwa sasa anaongoza kwenye orodha ya ufungaji mabao kwenye Serie A akiwa na mabao 14 msimu huu.



# Emery ana imani Ozil kubaki Arsenal

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amesisitiza kwamba, Mesut Ozil (pichani), bado ana majaliwa ya kuendelea kuwa hapo Arsenal.

Ozil hakutumika kwenye mchezo wa ushindi wa 2-0 Jumamosi dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa Ligi Kuu, akiwa pia alikosa mchezo dhidi ya West Ham.

Na sasa kocha huyo wa zamani wa Sevilla anaamini kuwa mchezaji huyo wa zamani wa Ujerumani, ambaye ndiye mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi hapo Arsenal, bado anaweza kuendelea kubakia hapo kwenye dimba la Emirates.

"Alikuwa tayari kucheza Jumamosi, lakini tuliamua kumuacha benchi," alisema Emery akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilizungumza na yeye pia na nilimtaka akiwa tayari kwa ajili ya mchezo wa Chelsea, kwenye mchezo ujao wachezaji wote watakuwa kwenye kikosi.

"Dhidi ya Chelsea walicheza vizuri, nina imani kubwa na yeye, nafikiri angefanya vizuri na kwenye mchezo ujao kila mchezaji atakuwa tayari kwa ajili ya mchezo ujao na naamini atakuwa kwenye ubora wake."

Kikosi hicho cha Emery sasa kinakabiliwa na mcheo dhidi ya Manchester United kwenye raundi ya nne ya kombe la FA, Ijumaa.

# BOATENG
## akamilisha usajili Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imekamilisha usajili wa kushtukiza wa kiungo mshambuliaji wa zamani wa AC Milan, Kevin-Prince Boateng (pichani chini), akisajiliwa kwa mkataba wa awali wa mkopo hadi mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 anarudi tena kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, kwa mara ya pili baada ya kukaa pale Las Palmas msimu wa 2016-17, na Barca ina kipengele cha kumsajili kwa ada ya euro milioni 8 mwishoni mwa msimu akionesha kiwango cha kuridhisha.

Barca kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ghana umekuja kama mshituko hasa baada ya kiungo huyo kwa sasa kutokuwa kwenye fomu nzuri, baada ya kucheza katika klabu za Las Palmas, Eintracht Frankfurt na Sassuolo kwa miaka michache iliyopita.

Kocha Ernesto Valverde amekuwa akitumaini kuimarisha safu yake ya ushambuliaji wakati huu wa kipindi cha usajili wa dirisha dogo la Januari, hasa baada ya kuondoka kwa Paco Alcacer aliyetimkia Borussia Dortmund na Munir El Haddadi aliyejiunga na Sevilla mwezi huu.

Kumekuwa na machaguo kadhaa kwa ajili ya kuchukua wachezaji wa mkopo, ambapo wachezaji kama Carlos Vela wa LAFC, Radamel Falcao wa Monaco na nyota wa Chelsea, Willian wamekuwa wakihusishwa.

Boateng alitabiriwa kuwa na mafanikio makubwa wakati akianza kucheza soka la kulipwa kwa kuonesha kiwango cha juu pale Hertha Berlin na baadae akajiunga na Tottenham, lakini mambo yalimuendea tofauti pale jijini London.


Mwaka mmoja baadae Portsmouth ilimsaidia kuweza kusajiliwa na Milan na alikuwa kwenye kikosi kilichotwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Italia msimu wa 2010-11.

Licha ya mara kwa mara kuonesha uwezo wake wa kucheza na mpira, Boateng bado hajaweza kutimiza kile ambacho alitarajiwa wakati akiwa bado kijana mdogo pale Hertha.

Hata hivyo, kujiunga kwake Barca kumempa nafasi nyingine ya kurudisha nafasi yake ya kucheza na atakuwa na nafasi nzuri ya kupigania namba kwenye nafasi ya kiungo.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BELLERIN NJE MSIMU MZIMA ARSENAL

**LONDON,** England

BEKI wa kulia wa Arsenal, Mhispania Hector Bellerin, atakuwa nje kwa kipindi chote cha msimu kilichobaki kutokana na jeraha la goti alilopata wakati wa mechi dhidi ya Chelsea Jumamosi iliyopita.

Bellerin, 23, atakuwa akipigania kuwa fiti kwa ajili ya msimu ujao, hivyo kilichobaki sasa ni kuona kama atakuwa nje kwa kipindi gani wakati huu akitarajiwa kufanyiwa vipimo zaidi kwa siku zijazo.

Muda wa chini uliotarajiwa kwa Bellerin kuwa nje ni takriban miezi sita, hivyo Kocha Mkuu wa Arsenal, Unai Emery sasa atapaswa kutafuta mbadala wa beki wa kulia kwa kipindi kilichobaki cha msimu.

Na kufuatia Ainsley Maitland-Niles, Stephan Lichtsteiner na Carl Jenkinson kuwa fiti, Arsenal inaweza isihangaike kujaribu kusajili mbadala wa Bellerin katika dirisha hili dogo.

Bellerin ni mchezaji wa tatu Arsenal kupata majeraha makubwa msimu huu. Tayari walishampoteza beki Rob Holding, ambaye alikuwa nje kwa kati ya miezi sita na tisa kutokana na jeraha la goti, na mshambuliaji Danny Welbeck, ambaye ni majeruhi wa kifundo cha mguu tangu Novemba.

Kadhalika, Arsenal imethibitisha kuwa Sven Mislintat, mkuu wa kitengo cha usajili , ataondoka mwezi ujao.

Mislintat alihusika sana katika uteuzi wa kocha Emery kurithi mikoba ya Arsene Wenger na alikuwa kichocheo kikubwa katika usajili wa Pierre-Emerick Aubameyang.

## KWA UFUPI

### MORATA KUTUA ATLETICO
STRAIKA wa Chelsea, Alvaro Morata, anatarajiwa kujiunga na Atletico Madrid kwa mkopo kwa kipindi chote kilichobaki cha msimu, huku kukiwa na uwezekano wa kumnunua jumla Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 26. **(Sky Sports)**

### POGBA KUJADILI MKATABA
KIUNGO wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, 25, yupo tayari kukaa chini na uongozi kuzungumzia suala la mkataba mpya. **(Sun)**

### RODRIGUEZ ATATHAMINIWA ARSENAL
ARSENAL inachunguza uwezekano wa kumsajili kiungo wa Real Madrid na Mcolombia James Rodriguez kwa mkopo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa sasa anacheza kwa mkopo Bayern Munich. **(Independent)**

### HAZARD AIKATAA UNITED
EDEN Hazard, 28, amesema hatajiunga na Manchester United hata kama Zinedine Zidane atatua kuinoa klabu hiyo na akafunguka kubaki **Chelsea. (Star)**

### BARTERN YATUA MAN CITY
BAYERN Munich inataka kutoa ofa ya pauni milioni 10 kwa straika wa Manchester City na Wales, Rabbi Matondo, 18, ambaye atakuwa nje ya makataba mwishoni mwa msimu. **(Sun)**

### MARTIAL, UNITED KUMALIZANA
STRAIKA wa Manchester United, Anthony Martial, 23, anakaribia kukubali mkataba mpya na miamba hiyo ya Old Trafford. **(ESPN)**

### ARNAUTOVIC AGOMEWA KUONDOKA
WEST Ham imemwambia mshambuliaji Marko Arnautovic, 29, watamruhusu kuondoka majira ya joto, lakini haitamuuza katika dirisha hili la Januari - hata kama Muaustralia huyo atakataa kucheza. **(London Evening Standard)**

### 'RABIOT AACHWE ASEPE TU'
NAHODHA wa Paris St-Germain, Thiago Silva, amesema haitakuwa kosa kumwacha kiungo Mfaransa Adrien Rabiot kuondoka klabuni hapo. Kiungo huyo anawindwa na klabu kibao za Ligi Kuu England. **(Telefoot, via Talksport)**

### AUDERO KUMRITHI CECH
ARSENAL inataka kwenda kumsajili kipa wa Juventus na Italia U-21, Emil Audero, 22, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Sampdoria, ili kuwa mbadala wa Petr Cech anayestaafu. **(Gianluca Di Marzio, via Metro)**

### CITY, PSG VITANI KWA DE JONG
MANCHESTER City itapata ushindani katika mbio za kumsajili kiungo wa Ajax na Uholanzi, Frenkie de Jong, 21, baada ya Paris St-Germain nayo kuingia katika mchakato wa kuisaka saini yake. **(Metro)**

### SPURS KUMUUZA JANSSEN
MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy yupo tayari kuchukua pauni milioni tano kumuuza straika Vincent Janssen, 24, mwezi huu, ambaye walimsajili kwa pauni milioni 17. **(Telegraph)**

### WEST HAM KUMKOSA ZAPATA
WEST Ham imekataliwa ofa yao ya pauni milioni 35.28 iliyotoa kwa Atalanta ili kumpata mshambuliaji Mcolombia Duvan Zapata, 27. **(Tuttosport, via Calciomercato)**

### CARDIFF KUMFUATA MAJA
CARDIFF inaandaa ofa kiasi cha pauni milioni mbili kwa Sunderland ili kumpata straika Josh Maja, lakini 'Black Cats' hao wanataka pauni milioni nne. **(Sun)**

## HABARI MICHEZO

## Sababu Ligi Kuu Zanzibar kuzorota

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KUTOKUWAPO kwa udhamini kwenye Ligi Kuu ya Zanzibar na baadhi ya klabu kukosa wadhamini, ni sababu kubwa ya kutokuwapo kwa ushindani na kuzorota ligi hiyo, imeelezwa.

Akizungumza mbele ya Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar walipokutana na klabu zinazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza ili kufahamu changamoto wanazokutana nazo, Mkurugenzi wa Ufundi wa timu ya JKU, Masoud Atai Masoud, alisema kukosekana kwa wadhamini kunafanya mchezo wa soka visiwani hapa kuendelea kuporomoka.

Masoud, alisema Ligi Kuu ya Zanzibar kwa sasa imepunguza mvuto na ushindani kwa klabu kama ilivyokuwa miaka ya nyuma kutokana na kukosa wadhamini kuanzia kwenye ligi hiyo hadi katika klabu zinazoshiriki Ligi Kuu.

Alisema changamoto ya udhamini inachangia kwa kiasi kikubwa kudumaza soka la Zanzibar na wachezaji kutokutoa kipaumbele katika mpira wa hapa nyumbani kwa sababu ya kutokuwa na kitu kinachopatikana katika ligi hiyo pale msimu unapomalizika.

“Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar anapopatikana hana zawadi yoyote anayopata kuanzia kombe au fedha, bali anakuwa na jina tu la bingwa basi, sasa hii inasababisha wachezaji kutoona mpira ni ajira ambayo wanaweza kujiajiri,” alisema Masoud.

Aidha, alisema asilimia kubwa ya timu za Zanzibar hali zao za kiuchumi ni mbaya hii ikitokana na kutokuwa na vyanzo vya mapato katika hali ambayo inawapa wakati mgumu hata kuziandaa timu zao pale zinapokabiliwa na michuano ya nje ya Zanzibar.

“Klabu hazina pesa za maandalizi, muda mwingine baadhi pia zinashindwa hata kusajili wachezaji wazuri kutoka nje ya Zanzibar hii inatokana na kutokuwa na fedha ya kujiendesha na hii pia inasababisha wachezaji wetu wazuri wanashindwa kukaa nao na kwenda nje ya Zanzibar,”alisema

Hata hivyo, mkurugenzi huyo ameiomba kamati hiyo pamoja na wizara husika inayoshughulikia michezo kuangalia uwezekano wa kutafuta wadhamini watakao weza kuidhamini ligi hiyo, pamoja na kuzungumza na wafanyabiashara waliopo hapa Zanzibar ili waweze kuzidhamini klabu za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza.

# OKWI: KIPIGO AS VITA KIMETUFUMBUA MACHO

**Na Faustine Feliciane**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Emmanuel Okwi, amesema kipigo cha mabao 5-0 walichokipata kutoka kwa AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kwenye mchezo wa Kundi D wa Ligi ya Mabingwa Afrika, kimewafumbua macho kuelekea mechi ijayo ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili baada ya kuwasili nchini wakitokea Congo, Okwi, alisema kupoteza mchezo huo wa ugenini dhidi ya AS Vita kumewafanya kujipanga zaidi kuelekea kwenye mechi ijayo dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Alisema mechi ijayo ambayo watakuwa ugenini dhidi ya Al Ahly, wataongeza umakini zaidi na kwamba anaamini benchi la ufundi limeona makosa yao na watayafanyia kazi kabla ya mchezo huo wa mwezi ujao.

“Tulipambana sana, lakini makosa tuliyoyafanya yametugharimu, kocha naamini atafanyia kazi makosa yetu ili kuweza kuwa makini zaidi kwenye mchezo unaofuata, kipigo tulichokipata kimetuamsha na kutupa uchungu kuelekea kwenye mchezo ujao,” alisema Okwi.

Aidha, alisema anafahamu kama wachezaji wanafahamu kuwa wamewaangusha mashabiki wao wanaowasapoti kwa nguvu zote.

“Mashabiki wetu wanapaswa kufahamu matokeo tuliyoyapata Congo ni sehemu ya mchezo na tutahakikisha hatuwaangushi tena,” alisema Okwi.

Matokeo waliyoyapata Simba mbele ya AS Vita yameifanya kuporomoka mpaka nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Kundi D ikiwa na pointi tatu sawa na AS Vita iliyopo nafasi ya pili, hiyo ikiwa ni kutokana na tofauti kubwa ya mabao ya kufunga na kufungwa, huku Al Ahly ikiongoza kwa alama nne na JS Saoura wakiburuza mkia wakiwa na pointi moja.

Simba itasafiri kuelekea Misri tayari kuwakabili Al Ahly kwenye mchezo utakaochezwa Februari 2, mwaka huu saa 3:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.




Wachezaji wa timu ya Kikapu ya DTB Tanzania, wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kuibuka washindi wa jumla wa michuano ya kikapu kwa taasisi za fedha (Bankers Basketball League) kwa msimu wa 2018/2019. Mechi ya fainali ya michuano hiyo, ilifanyika Jumamosi iliyopita katika viwanja vya Gymkhana, jijini Dar es Salaam, ambapo DTB iliinyuka NMB kwa pointi 90-73. Benki nyingine zilizoshiriki kwenye michuano hiyo ni pamoja na Azania, CRDB, TADB na NBC. **MPIGAPICHA WETU**

# ‘Ubingwa Ligi Kuu bado kitendawili’

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa klabu ya Yanga na timu ya Taifa ‘Taifa Stars’, Sekilojo Chambua, amesema kwa namna ligi inavyokwenda na baadhi ya timu kuwa na viporo vingi ni ngumu kutabiri bingwa wa Ligi Kuu msimu huu.

Chambua, alisema tofauti na msimu uliopita, msimu huu idadi ya mechi ni nyingi kwa kila timu hivyo licha ya timu nyingine kuwa na mechi nyingi mkononi bado huwezi kutabiri timu itakayotwaa ubingwa.

Alisema kama ingekuwa ligi ya msimu uliopita, sasa hivi Yanga wangekuwa kwenye nafasi kubwa ya kutabiriwa kuwa mabingwa msimu huu.

“Ukiangalia kwa sasa, Yanga inaongoza ligi, lakini Azam wapo nyuma yao wana mchezo mmoja mkononi na wamepishana kwa pointi tisa, Simba wanamichezo sita mkononi..., sasa kwa mazingira hayo huwezi kusema timu fulani itakuwa bingwa,” alisema.

Aidha, alisema anaamini timu zote za juu kwenye msimamo, Yanga , Azam na Simba wananafasi ya kutwaa ubingwa msimu huu.

Simba ina viporo vya mechi sita ambapo kama watafanikiwa kushinda vyote watakusanya pointi 18 na kuwa na jumla ya pointi 51, pointi mbili pungufu na Yanga iliyocheza michezo 20.

Mechi za ligi kwa timu za Yanga, Simba, Singida United na Mbao FC zimesimama kupisha michuano ya SportPesa iliyoanza jana kwenye Uwanja wa Taifa.

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.Yanga | 20 | 17 | 2 | 1 | 38 | 14 | 53 |
| 2.Azam | 19 | 13 | 5 | 1 | 27 | 8 | 44 |
| 3.Kinondoni MC | 22 | 8 | 10 | 4 | 29 | 16 | 34 |
| 4.Simba | 14 | 10 | 3 | 1 | 28 | 5 | 33 |
| 5.Lipuli | 22 | 8 | 9 | 5 | 17 | 13 | 33 |
| 6.Mbao | 23 | 8 | 10 | 5 | 16 | 19 | 33 |
| 7.Coastal Union | 21 | 6 | 10 | 5 | 20 | 21 | 28 |
| 8.Kagera Sugar | 21 | 6 | 10 | 5 | 19 | 20 | 28 |
| 9.Alliance | 23 | 7 | 7 | 9 | 19 | 27 | 28 |
| 10.Mtibwa Sugar | 18 | 8 | 2 | 8 | 19 | 15 | 26 |
| 11.Mbeya City | 21 | 7 | 5 | 9 | 24 | 26 | 26 |
| 12.JKT Tanzania | 22 | 5 | 10 | 7 | 10 | 15 | 25 |
| 13.Stand Utd | 22 | 7 | 4 | 11 | 21 | 29 | 25 |
| 14.Ruvu Shooting | 23 | 6 | 7 | 10 | 19 | 31 | 25 |
| 15.Mwadui | 23 | 6 | 6 | 11 | 24 | 22 | 24 |
| 16.Singida United | 21 | 6 | 6 | 9 | 15 | 20 | 24 |
| 17.Ndanda | 21 | 5 | 7 | 9 | 12 | 25 | 22 |
| 18.Biashara Utd | 22 | 4 | 8 | 10 | 13 | 21 | 20 |
| 19.African Lyon | 23 | 4 | 7 | 12 | 15 | 27 | 19 |
| 20.TZ Prisons | 21 | 2 | 11 | 9 | 12 | 21 | 17 |

Michezo
Jumatano Januari 23, 2019
Nipashe

## Bellerin nje msimu mzima Arsenal



HABARI UK. 30

**NUSURA JELA...**



Mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, akiwa amejawa na tabasamu huku akimshika mkono mpenzi wake, Georgina Rodriguez, wakati wakitoka Mahakama ya Madrid jana, ambapo aliepuka kifungo cha miezi 23 jela, lakini akikubali kulipa faini kiasi cha pauni milioni 16.9 (Sh. bilioni 50 za Tanzania) kwa kosa la kukwepa kodi. Nchini Hispania kifungo kisichozidi miaka miwili hakipaswi kutumikiwa gerezani isipokuwa kwa kosa la uhalifu. **PICHA: DAILY MAIL**

# AL AHLY YAMTESA AUSSEMS, SIMBA

### ●●● Waivaa Leopards SportPesa Cup leo, akili hesabu zikiwa Misri, Mbelgiji asema...

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebaki siku 10 kabla ya mchezo wao wa ugenini wa Ligi ya Mabingwa Afrikia dhidi ya Al Ahly ya Misri, Kocha wa Simba, Patrick Aussems, anaisoma vilivyo timu hiyo ya Misri lengo likiwa ni kupata matokeo mazuri ugenini baada ya timu yake kupoteana ikiwa DR Congo.

Aussems amesema kwa kutambua umuhimu na ugumu wa mchezo huo anapitia mikanda ya video ya wapinzani wao hao kuangalia namna ya kujipanga kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye mchezo huo utakaochezwa Februari 2, mwaka huu jijini Cairo, Misri.

Kocha huyo raia wa Ubelgiji aliliambia Nipashe jana kuwa anafahamu ni mambo gani wachezaji wake walikosea kwenye mchezo wao uliopita dhidi ya AS Vita walipopoteza kwa mabao 5-0.

"Tunashiriki michuano ya SportPesa.., pamoja na kuwa tunashiriki kwa lengo la kutwaa ubingwa, pia nitatumia michuano hii kurekebisha mapungufu niliyoyaona kwenye mchezo uliopita," alisema Aussems.

Alisema hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni ngumu na lengo lao ni kuona timu inafika robo fainali ya michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Bado Simba ina nafasi pamoja na kupoteza mchezo dhidi ya AS Vita, tunajipanga kwa kufanya mazoezi huku pia tukirekebisha mapungufu niliyoyaona, Al Ahly ni timu nzuri na ndio maana naifuatilia," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Simba imeshinda mchezo mmoja kwenye kundi lake dhidi ya JS Saoura na kupoteza mechi moja dhidi As Vita na inashika nafasi ya tatu nyuma ya Vita huku timu zote zikiwa na pointi tatu katika kundi hilo ambalo linaongozwa na Al Ahly yenye alama nne na JS Saoura wakiburuza mkia kwa pointi yao moja baada timu zote kushuka dimbani mara mbili.

Katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), vinara wawili wa kila kundi kutoka makundi manne, watatinga robo fainali.

Simba itashuka katika dimba la Taifa leo kuvaana na AFC Leopards ya Kenya kwenye michuano ya SportPesa ambayo Gor Mahia ni bingwa mtetezi kufuatia kulitwaa taji hilo mara mbili mfululizo.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao mwaka jana walifungwa katika mechi ya fainali na Gor Mahia, wamepania kufanya vizuri kwenye michuano hiyo ili kukata tiketi ya kucheza na Everton ya England.

Mbali na fedha na kombe, bingwa wa michuano hiyo hucheza na Everton ambayo nayo inadhaminiwa na Kampuni ya SportPesa kama ilivyo kwa Simba, Yanga na Singida United za Tanzania.

## Kilichoiua Yanga SportPesa Cup

**Na Faustine Feliciane**

MAKOSA waliyoyafanya mabeki wa Yanga kipindi cha kwanza yameigharimu timu hiyo na kuondolewa kwenye michuano ya Sportpesa baada ya kukubali kipigo cha mabao 3-2 kutoka kwa Kariobangi Sharks ya Kenya.

Yanga jana ilionekana kuidharau Sharks huku kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera akianza mchezo na mshambuliaji mmoja na kujaza viungo wengi katikati.

Zahera aliwaanzisha kwa pamoja, Abdallah Shaibu 'Ninja' kama kiungo mkabaji pamoja na Feisal Salum huku pia Haruna Moshi Boban akishuka katikati kusaidia viungo na mbele akisimama Heritier Makambo.

Yanga walifanya shambulizi la nguvu dakika ya pili tu ya mchezo, lakini Makambo alishindwa kuukwamisha wavuni mpira baada ya kupokea pasi ndefu ya Kelvin Yondani, lakini mpira ukatoka nje.

Sharks walianza kupata bao la kwanza dakika ya 10 kupitia kwa Abuya Duke kwa shuti kali nje ya eneo la hatari ambalo lilimshinda kipa wa Yanga, Klaus Kindoki kabla ya kuandika la pili dakika ya 36 kwa shuti kali kupitia kwa Abege George.

Mabadiliko yaliyofanywa na Zahera kipindi cha pili kwa nyakati tofauti kwa kuwatoa Ninja, Moshi na kuingia Deus Kaseke na Amissi Tambwe yaliongeza kasi kwa Yanga na kufanikiwa kupata bao la kwanza dakika ya 86 kupitia kwa Tambwe kabla ya Sharks kuongeza la tatu kupitia kwa Duke baada ya mabeki wa Yanga kujichanganya.

Zikiwa zimesalia dakika mbili mpira kumalizika, Makambo aliipatia Yanga bao la pili, baada ya kuingia bao hilo kulitokea tafrani kufuatia kipa wa Sharks kuung'ang'ania mpira na ndipo vurugu za wachezaji wa timu zote zilipotokea na mchezo kusimama kwa dakika sita.

Hata dakika 10 za mwisho mwamuzi wa mchezo huo, George Gotagota, alionekana kuelemewa na mchezo akiruhusu faulo nyingi.

Kwa matokeo hayo ya jana, Yanga imeungana na Singida United kuaga mashindano hayo kufuatia timu hiyo ya mjini Singida nayo kukubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Bandari FC ya Kenya katika mchezo wa mapema jana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >